

# Mpendwa Wangu

Adrian Ebens

# Mpendwa Wangu

© 2020 Adrian Ebens

Fatheroflove.info
adrian@life-matters.org

fatheroflove.info

**Maranathamedia-kenya.com**

Kwa Lorelle

Mwandani wangu, msaidizi na
rafiki mpendwa wa duniani

# Yaliyomo


Utangulizi ........................................................................ 6

Sehemu ya Kwanza. Mwaliko ........................................................ 8

1. Bwana Harusi ...................................................................... 8

2. Kishawishi ........................................................................ 12

3. Mkanganyiko ....................................................................... 17

4. Lango ............................................................................. 22

5. Madhabahu ya Shaba ................................................................ 26

Kingilio I ........................................................................... 32

6. Birika ya Shaba ................................................................... 33

7. Mkanganyiko Zaidi ................................................................. 37

Sehemu 2. Uchumba .................................................................. 46

8. Pazia ya Kwanza ................................................................... 46

9. Nuru ya Ulimwengu ................................................................. 53

10. Mkate wa Uzima ................................................................... 58

Kiingilio II ......................................................................... 63

Sehemu 3. Kusita Kati ya Mawazo Mawili .............................................. 64

11. Vita Baina ya Mwili na Roho ...................................................... 64

12. Drama ya Utambulisho Uliobadilishwa .............................................. 69

13. Michezo ya Akili .................................................................. 73

14. Nyumba ya Kadi .................................................................... 79

Kiingilio III ........................................................................ 85

Sehemu 4. Kuokolewa na Mpendwa Wangu ................................................ 86

15. Eliya ............................................................................. 86


16. Vyote kwa Pamoja Vinapendeza ...................................................... 93

17. Moto Usafishao .................................................................... 99

18. Apollyoni ........................................................................ 106
19. Msaidizi ........................................................................ 111
Kiingilio IV ........................................................................ 117
Sehemu 5. Patakatifu Pa Patakatifu ................................................ 119
20. Kuchumbiwa na Zama za Kale .................................................. 119
21. Mbele ya Sanduku la Agano ..................................................... 123
22. Furaha ya Mpendwa Wangu ...................................................... 128
Hitimisho ........................................................................ 135

# Safari ya kuelekea Patakatifu Pa Patakatifu



# Utangulizi

Nasikia sauti ya nyayo zake, kupumua kwangu kunaongeza kasi kwa matarajio.

Naisikia sauti yake kama sauti ya maji mengi. Ni kama zeri tamu kwa roho yangu. Mpendwa wangu anaita. Inaweza kuwa ni mimi ambaye anaita? Tumaini kama hilo la thamani linawezaje lelewa katika kifua changu? Dhana hii inatokea wapi? Mbona nihesabiwe kuwa nastahili utambuzi wake–Mfalme huyu mkuu, Mwana Mpendwa wa Baba?

Nithubutu kutumaini? Haitadhihirisha ujinga wa akili yangu? Sitachekelewa kwa dharau kwa ndoto zangu za kitoto? Huyu ni Mfalme mkuu na shupavu, nguvu na kiburi cha Babake mkuu; inawezekanaji kuwa anaita kwa ajili yangu?

Sikiliza! Unasikia katika utulivu? Anaita tena! Sauti yake, tamu zaidi, inapenyeza katika upepo mwanani wa usiku, ikitafuta mpendwa wake. Oh moyo wangu, usiiruhusu shaka! Usijiweke wazi kwa mishale yenye dharau! Anaita kwangu; ndio, kwangu anaita. Nalisikia jina langu! Hakika ananiita!

Oh Mpendwa wangu, niko hapa! Kila ufumwele wa utu wangu unatikisika kwako. Chote nilicho nacho ni chako. Imani inachukua bawa na kuongeza ujasiri juu ya milima mikuu iliyofunikwa na waridi na katika mabonde yenye manukato ya maua mazuri.

Namuona! Kutoka kwa pahali pangu pazuri pa mukuyu, hauwezi muona? Mpendwa wangu anakuja; tumaini la vizazi vyote linakuja! Oh mpendwa Mzee wa Siku, nipe nguvu; moyo wangu unazimia kwa furaha; nalemewa na furaha! Naharakisha ombi langu kwako kwa mkono wa Mpendwa wangu.

Oh binti Yerusalemu, furahi pamoja nami, kwa kuwa naona katika yeye zawadi isiyo na kifani; Oh ni jinsi gani nampenda! Mfalme huyu mkuu aliyepakwa manukato ya manemane na ubani, anaibuka kutoka kwa ukungu. Nageuza kichwa changu kumwangalia, kama kweli, ananitafuta.

Kisha naamka. Niko wapi? Nini kilitendeka? Hii yote imekuwa ndoto? Nimejidanganya kwa matumaini ya kitoto? Hakika, ananitafuta! Nina uhakika nalo. Jipe moyo mpendwa wangu. Amini, ndio, amini kwamba anakutafuta.

# Sehemu ya Kwanza. Mwaliko

## 1. Bwana Harusi

Baba anainuka kutoka kwa kiti chake cha enzi na katika gari la moto anaingia Patakatifu pa Patakatifu pa Hekalu la Mbinguni. Viti vya enzi vinawekwa, na Mzee wa siku anaketi. Nabii Danieli, akitazama hili katakia maono, anadhihirisha kuwa mavazi yake ni meupe kama theluji, na nywele zake ni kama sufu safi. Mamilioni ya malaika wanamzunguka; baadhi yao wanahusishwa moja kwa moja katika yale ambayo yanaendelea na wengine wanatazama tukio hili kuu kwa matarajio.

Mwana wa Adamu, tangu alipoondoka duniani, amekuwa akihusika katika kazi yenye thamani ya upatanisho wa wana na binti wa Adamu walioanguka. Dua ya watakatifu hupaa kwa Baba na ombi la msamaha, neema, nguvu, ujasiri, nuru, faraja, na furaha. Yesu kwa uaminifu huwasilisha maombi kwa Baba yake na kutetea damu yake kwa niaba ya ndugu zake kutoka duniani.

Baba huona Roho wa Mwanawe akiingia katika mioyo ya wenye dua; akishuhudia upendo wao kwa Mwanawe na imani kwa neno lake kwamba "Ili kila mtu amwaminiye awe na uzima wa milele," (Yohana 3:15) Baba wa nuru kwa Rehema hutuma roho wa kufariji wa Kristo na uponyaji, neema, upendo, uwezo, na furaha.

Ingawa kazi takatifu ya upatanisho ya Kristo ilifichwa na falsafa kuu ya nguvu za pembe ndogo, mamilioni ya roho bado zinapata kuifikia neema kupitia Kristo, Bwana wao na Mkombozi. Kuteremka kupitia karne ya Zama za Giza watakatifu wa Mungu wangejitokeza wazi kwa enzi ya neema, wakijua kwamba Mwana wa Mungu "adumu daima kuomba kwa ajili yao." (Waebrania 7:25).

Katika sehemu kadhaa kwenye Maandiko Mungu aliacha ushahidi wa wakati ambao mabadiliko muhimu yangetendeka katika kazi ya

upatanisho ya Kristo. Paulo alinena kwa Felix kuhusu "hukumu itakayokuja" (Matendo 24:25). Yohana aliona mjumbe akiruka katikati ya mbingu akitangaza wakati ambao "Saa ya hukumu yake imekuja" (Ufunuo 14:6, 7). Pia aliona hekalu la Mungu lililoko mbinguni likifunguliwa, na sanduku la agano lake likaonekana kwa umeme, sauti na radi miongoni mwa vitu vingine. (Ufunuo 11:19)

Kwa maandalizi ya saa hii ya hukumu, nchi iliangazwa na ujumbe kutoka mbinguni ambao ulionyesha kuwa Kristo alikuwa anakuja. Mfumo wa unabii ulikuwa umewekwa wazi kabisa na William Miller miongoni mwa wengine ambao walifuatilia wakati wa kutakaswa kwa Patakatifu kuwa mwaka wa 1844. Vituo vyote vya Kimishonari ulimwenguni vilihubiri habari kuwa Kristo anakuja! Kristo hakika alikuwa anakuja lakini sio duniani kumchukua bibi harusi wake, ila kwa Baba yake kuamua nani atakaye kuwa Bibi harusi. Harusi haifanyiki baada ya Marejeo ya Pili bali kabla!

Wanawali wenye hekima ambao walilia "Tazama bwana harusi anakuja" waliwezeshwa kutambua kutokuelewa kwao kwa mahali ambapo Bwana harusi alikuwa akienda. Na kwa hivyo tunasoma:

> Nikaona katika njozi za usiku, na tazama, mmoja aliye mfano **wa mwanadamu akaja pamoja na mawingu ya mbingu akamkaribia huyo mzee wa siku**, wakamleta karibu naye. (14) Naye akapewa mamlaka, na utukufu, na ufalme, ili watu wa kabila zote, na taifa zote, na lugha zote, wamtumikie; mamlaka yake ni mamlaka ya milele, ambayo hayatapita kamwe, na ufalme wake ni ufalme usioweza kuangamizwa. Danieli 7:13-14.

Yesu alipokuwa akibebwa katika wingu na kuletwa karibu na Mzee wa siku, dhana nzima ya utakaso kwa wakristo ilibadilishwa. Hadi wakati huu wale ambao waliamini ndani ya Kristo walikuwa na wazo ndogo kwamba wakati utafika ambapo kazi ya msamaha wa dhambi itakoma *kabla ya* kuja kwa Kristo kudai bibi harusi wake.

> Angalieni, namtuma mjumbe wangu, naye ataitengeneza njia mbele yangu; naye Bwana mnayemtafuta **atalijilia hekalu lake ghafula; naam, yule mjumbe wa agano mnayemfurahia**, angalieni,

> anakuja, asema Bwana wa majeshi. (2) **Lakini ni nani atakayestahimili siku ya kuja kwake? Au ni nani atakayesimama atakapoonekana yeye?** Kwa maana yeye ni mfano wa moto wa mtu asafishaye fedha, ni mfano wa sabuni ya mtu afuaye nguo; (3) **naye ataketi kama asafishaye fedha na kuitakasa,** naye atawatakasa wana wa Lawi, atawasafisha kama dhahabu na fedha; nao watamtolea Bwana dhabihu katika haki. (4) Wakati ule ndipo dhabihu za Yuda na Yerusalemu zitakapopendeza mbele za Bwana, kama katika siku za kale, na kama katika miaka ya zamani. (5) **Nami nitawakaribieni ili kuhukumu**; nami nitakuwa shahidi mwepesi juu ya wachawi, na juu ya wazinzi, na juu yao waapao kwa uongo; na juu yao wamwoneao mwenye kuajiriwa, kwa ajili ya mshahara wake, wamwoneao mjane na yatima, na kumpotosha mgeni asipate haki yake, wala hawaniogopi mimi, asema Bwana wa majeshi. Malaki 3:1-5.

Watu wa Mungu waliposoma unabii wa Bibilia kwa makini, waligundua kwamba wale ambao watavumilia siku ya kuja kwake watapitia moto wa asafishaye na kusafishwa kama dhahabu na fedha. Waligundua kwamba Mungu atawakaribia katika hukumu ambayo watasimama mbele za Mungu bila mpatanishi wa dhambi. (Isaya 59:16).

Uzoefu wa Patakatifu pa Patakatifu utaleta watu wa Mungu katika uhusiano wa karibu kama huo na Mkombozi wao kwamba kweli itasemwa kwao:

> Wapenzi, sasa tu watoto wa Mungu, lakini bado haijadhihirika tutakavyokuwa, lakini twajua ya kwamba, Yeye atakapodhihirishwa, tutafanana naye, kwa maana tutamwona kama alivyo. 1 Yohana 3:2.

Katika wakati huo ambao Yesu aliletwa mbele za Baba, wengi wa Wakristo ulimwenguni walikataa kukubali kwamba Kristo kwanza alikuwa akija, na pili alikuwa akija kwa Mzee wa Siku kupokea ufalme kupitia kwa mchakato wa Hukumu.

Hukumu humruhusu Bwana harusi kuuchunguza moyo wa Bibi harusi ili kuona kama kweli anampenda na kumuamini. Anamwamini kwa kweli ili kumpitisha katika hukumu? Anaamini kwamba anaweza mbeba hadi

katika pahali ambapo anaweza ishi bila upatanisho kwa dhambi? Ahadi zake zinaweza pewa kipao mbele kwake na kumfikisha katika bandari ya pumziko?

Uzoefu wa Patkatifu pa Patakatifu unahitaji bibi harusi anayetazamiwa kumtahini kwa karibu Mume wake anayetazamiwa sawasawa na anavyomtahini kwa karibu. Mwana wa Adamu ni nani? Alitoka wapi? Hati ya utambulisho wake ni ipi? Ana uhusiano upi na Mzee wa Siku, Baba? Mbona anahitaji mchakato halisi kama huo wa kusafisha? Inawezekana mtu awe na uhusiano wa karibu na mtu mwingine ambaye machache karibu na kukosekana yanajulikana kuhusiana na asili yake? Mtu kama huyu anaweza aminiwa kubeba mwingine kupitia uzoefu wa Patakatifu pa Patakatifu?

Hili linatuleta kwenye mada ya kitabu hiki, kujifunza yote ambayo tunaweza kumhusu Mwana wa Adamu katika muktadha wa uzoefu wa Patakatifu pa Patakatifu. Wakati inaweza wezekana kuorodhesha tu ukweli wote wa Andiko kuhusu Mfalme huyu mkuu wa uzima, uzoefu wa Patakatifu pa Patakatifu unatwalika katika harusi na kwa hivyo kuanda jukwaa la kuelezea kisa cha upendo. Nafikiria wengi wetu wanapendelea visa kuliko kweli mbichi iwapo watapewa uteuzi.

Katika sura zifuatazo nitashiriki nanyi uzoefu wangu katika kumjua Bwana harusi na mbona nampenda. Nitawaonyesha jinsi alivyouteka moyo wangu na mbona alistahili niache vyote ili kumpata.

Yesu ni njia ya uzima, na tunaambia katika Zaburi kwamba:

> Ee Mungu, njia yako i katika utakatifu; Ni nani aliye mungu mkuu kama Mungu? Zaburi 77:13.

Kisa hiki cha upendo kitajengwa juu ya njia ya Patakatifu, kuanzia kwa lango na kuelekea katika Patakatifu pa Patakatifu. Yakiongengezwa kwa mada hii kuu yatakuwa mambo ya kisa kutoka kwa "Pilgrim's Progress" yakiandamana na mada inayopatikana katika Wimbo wa Sulemani.

## 2. Kishawishi

Nilisimama nikitazama nyota za mbinguni. Chini ya anga lisilo kuwa na mawingu nilitafiti ukuu na ukubwa wa mkusanyiko wa (Milky-Way Galaxy). Ni moja ya kumbukumbu zangu za awali za kukutana na muumbaji wangu. Nilikuwa na umri wa miaka minne na udhahiri wa kumbukumbu hiyo unasalia nami. Ni uzuri wa namna gani, ni ukuu namna gani macho yangu yalitazama. Nilifunzwa kama mtoto kwamba:

> Mbingu zauhubiri utukufu wa Mungu, Na anga laitangaza kazi ya mikono yake. Zaburi 19:1.
>
> Kwa neno la Bwana mbingu zilifanyika, Na jeshi lake lote kwa pumzi ya kinywa chake. Zaburi 33:6.

Mama yangu angechukua kila fursa kuniambia kwamba Mungu aliumba ulimwengu huu na kila kitu ndani yake. Mawazo haya yalizikwa chini ya shughuli nyingi za kufurahisha ambazo zilimudu bila mawazo mtoto anayekua katika miaka ya 1970's. Sehemu kubwa ya utoto wangu ilizingatiwa kwa kucheza na marafiki, kwenda shuleni na kujiburudisha. Nilitafiti kumbukumbu yangu nikitafuta wakati ambao makini yangu ilitekwa kuisikiza sauti ya Mpendwa wangu.

Kuna vitu vingi ambavyo naweza sadiki vilitendeka, lakini kile kinachobubujika kutoka kwenye kumbukumbu ndicho kinacho unganisha dukuduku za kisa cha upendo. Kuna baadhi ya vitu ambavyo nakumbuka kupitia kwa uzoefu hasi. Nakumbuka usiku mmoja wazazi wangu walikuwa wamehudhuria tamasha na mmoja wa rafiki zao alikuwa anamtunza dada yangu pamoja nami. Nakumbuka dhahiri wasiwasi niliohisi nikiwa nimelala bila usingizi kitandani mwangu, nikikaza masikio yangu kusikiza mlio wa injini ikija kwa njia ya gari letu.

Ingawa sikutambua wakati huo, naona wazazi wangu walidhihirisha ulinzi wa Mpendwa wangu. Niko na kumbukumbu wazi ya kuhisi salama katika ufahamu wa uwezo wa baba yangu, hasa wakati ambao alinikumbatia na kunishika kwa ukaribu. Kwangu, baba yangu angekimbia kama upepo, kubeba vitu vizito, aniginize shoka kwa neema na nguvu, na ajenge chochote. Uzoefu wangu unathibitisha ukweli kwamba:

> Wana wa wana ndio taji ya wazee, Na utukufu wa watoto ni baba zao. Methali 17:6.

Mpendwa wangu alimweka baba yangu maishani mwangu kama dhihirisho la nguvu zake, neema na uwezo wa kufanya chochote kwa pendo na ulinzi wa wanawe. Kitu kingine ambacho nakumbuka ni himizo, huruma na malezi ya mama yangu. Kuna vibanzi vya kipekee ambavyo angeoka, kukata na kuponda angeuguza, sauti yake changamfu wakati nilikuwa nimeongeza kikwazo au sauti yake tulivu akinukuu kutoka kwa Zaburi tufani kali ilipopitia juu ya makao yetu. Mara nyingine ningesikia sauti ya Mpendwa wangu kupitia kwa ulinzi wa malezi ya mama yangu.

Kwa kukabiliana na nyoka aina ya tiger mwenye hasira na kuepuka mara zisizohesabika kutoka kwa madhara fulani ya ajali ya gari, nilitambua ulinzi wa Mpendwa Wangu. Fungu la Bibilia ambalo mama yangu alilipenda zaidi lilileta hisia ndani yangu:

> Malaika wa Bwana hufanya kituo, Akiwazungukia wamchao na kuwaokoa. Zaburi 34:7.

Kwa uwazi nakumbuka picha kutoka kwa visa vya Bibilia ambavyo mama yangu angenisomea. Ilionyesha mvulana mdogo akiwa na Kigali kidogo chekundu na gari likimjia na malaika mwenye mabawa makubwa akimkinga kutoka kwa lile gari. Huu ulikuwa ujumbe wa kufariji uliotumwa kutoka kwa Mpendwa wangu, ukidhihirisha jinsi huwatuma malaika wake kutulinda.

Imani ya baba yangu kwa Mungu imekuwa rahisi na ya vitendo. Nakumbuka mada mbili kutoka kinywani mwake: tunza amri za Mungu na umpende mwenzako. Mafungu mawili ambayo alisisitiza yalikuwa:

> Hii ndiyo jumla ya maneno; yote yamekwisha sikiwa; Mche Mungu, nawe uzishike amri zake, Maana kwa jumla ndiyo impasayo mtu. Mhubiri 12:13.

> Kwa hiyo cho chote ambacho mngetaka mtendewe na watu, ninyi nanyi watendeeni vivyo hivyo. Kwa kuwa hii ndiyo Torati na Manabii. Mathayo 7:12.

Msisitizo wake wa kutenda haki na kuwa mkweli ulinisababisha kuwa na dhamiri nyeti. Nakumbuka matukio kadhaa nilipoivunja sheria na dhamiri yangu iligongwa na hisia za hatia. Nakumbuka ombi la machozi kwa Mungu anisamehe nikiwa miaka sita. Leo hii, hisia ya hatia inachukuliwa kama mateso ya kutisha. Ila kwangu, namshukuru Mungu kwa dhamiri nyeti kama hiyo. Kupitia kwayo, nilisikia sauti ya upendo, kuongoza na kuonya ya Mpendwa wangu.

Wazazi wangu walinunua mfululizo wa matukio kumi uitwao "Hadithi za Bibilia." Baadhi ya hadithi hizi tulikuwa nazo kwenye kanda za sauti. Nakumbuka nikisikiliza kisa cha Musa na Bahari ya Shamu, Yoshua na Yeriko, Daudi na Goliatho, Eliya na Elisha. Bado tuko na mfululizo huu nyumbani mwetu na picha nyingi ambazo hurejesha kumbukumbu za utoto wangu. Visa hivi vikiwekwa juu ya ulinzi na malezi ya wazazi wangu viliniruhusu kumtazama Mpendwa wangu. Kupitia visa hivi alinifunza kisa cha ulimwengu, jinsi ulianza, kilichoenda mlama, mgogoro kati ya wema na uovu, suluhisho la dhambi, jinsi ulimwengu huu utaisha, na kile ambacho kitakuwa malipo kwa wale ambao wanampenda Mungu na kutunza amri zake ikiwemo Sabbato.

Nakumbuka nikihudhuria kanisa na shule ya Sabato na vile vile kuhudhuria shule ya msingi ya kanisa. Miaka kumi na miwili ya kwanza ya maisha yangu, nakumbuka matukio machache kama kunayo yaliyoteka makini yangu kuhusu masuala ya kiroho. Nakumbuka nikipaka picha rangi, kuimba nyimbo, kucheza ala ya muziki, lakini hakuna kumbukumbu ya athari yoyote ya kiroho. Kilicho nishangaza zaidi ni kwamba ingawa nilikuwa nimesikiza visa vingi kumhusu Yesu katika miaka yangu kumi na miwili ya kwanza, sikuwa na kumbukumbu nyingi kuvihusu. Ninakumbukumbu mara moja au mbili za wito wa madhabahu na kuhisi shinikizo macho mengi yakinitazama na ufahamu kwamba waliosimama walionekana wema na wale ambao hawakusimama walionekana wabaya.

Kanisa letu lina shirika la vijana liitwalo watafuta njia (Pathfinders) ambalo mtu mchanga huendelea katika viwango mbalimbali kwa kozi fulani na shughuli zinazoafikiwa. Katika miaka kumi na miwili nilihitajika kusoma Bibilia kama sehemu ya kazi ya kozi yangu. Hii ilikuwa mara yangu ya

kwanza kuhusiana na Bibilia kwa kweli. Ninakumbukumbuka mambo kadhaa kutoka kwa visa vya Mwanzo na Hesabu. Ninakiri kwamba nilisoma Walawi pamoja na vitabu vingine vya Bibilia kwa kupitia tu! Nakubumbuka baadhi ya hadithi zingine katika Agano la Kale na injili. Ingawa motisha yangu kimsingi ilikuwa kukamilisha kazi, bado kulikuwa na mvuto ulioinuka moyoni mwangu ambao ulileta maswali kuhusu visa fulani vilivyoamsha hamu ya kudadisi. Hii ilikuwa ladha yangu ya kwanza ya Neno la Mungu. Sehemu ya kazi ya kozi ilinihitaji kukariri Zaburi ishirini na tatu na Heri nane za Mathayo 5. Maneno hayo yaliniathiri:

> Bwana ndiye mchungaji wangu, Sitapungukiwa na kitu. (2) Katika malisho ya majani mabichi hunilaza, Kando ya maji ya utulivu huniongoza. (3) Hunihuisha nafsi yangu; na kuniongoza Katika njia za haki kwa ajili ya jina lake. (4) Naam, nijapopita kati ya bonde la uvuli wa mauti, Sitaogopa mabaya; Kwa maana Wewe upo pamoja nami, Gongo lako na fimbo yako vyanifariji. (5) Waandaa meza mbele yangu, Machoni pa watesi wangu. Umenipaka mafuta kichwani pangu, Na kikombe changu kinafurika. (6) Hakika wema na fadhili zitanifuata Siku zote za maisha yangu; Nami nitakaa nyumbani mwa Bwana milele. Zaburi 23:1-6.

Ni kutoka kwa kifungu hiki Mpendwa wangu alinishawishi kwa mara ya kwanza kwaza kumhusu. Nilipokuwa nikisoma maneno "Bwana ndiye mchungaji wangu," nilifikiria kuhusu mtu ambaye kwa upole anajali kondoo, akichunguza zaidi ya upeo wa macho kuona kama kuna hatari yoyote. Nilijenga uhusiano kati ya mchungaji na Yesu. Kisha swali lilijitokeza polepole akilini mwangu, *"*Sitapungukiwa na kitu*" inamaana gani?* Nakumbuka nikibaini kwamba sitakosa chochote kwa sababu Mchungaji atanipa vyote vilivyohitajika. Mpendwa wangu alikuwa akinizungumzia kwa Neno lake. Sauti ilikuwa laini na ya kusikika, bado nilihisi utulivu wa maji niliyokuwa nikisoma kuyahusu. Ni jinsi gani natamani ningeisikiza sauti hiyo salama, lakini kulikuwa na sauti nyingine ambayo tutaizungumzia katika sura ijayo, ilinipotosha, kunidanganya, ilinisifu mno, iliniogofya na kunitamausha.

Wakati huu nilifanya uchambuzi wa Bibilia na mhubiri wa kanisa letu kwa maandalizi ya ubatizo. Sikumbuki mengi ya vipindi hivyo, lakini nilikuwa na

hisia kwamba Mungu, wazazi wangu na kanisa langu walipendezwa na uamuzi wangu. Sikuwa na dhana tofauti ya Mungu ambaye nilikuwa nikiapa kumtumikia. Nilijua kwamba kulikuwa na Mungu na Yesu Mwanawe. Nilikuwa nimefunzwa kumhusu Roho mtakatifu lakini sikuwa na wazo kweli kuhusu kazi yake. Niliamini kwamba Mungu alimtuma Mwanawe ulimwenguni na kwamba kama nilimwamini Yesu nitakuwa na uzima wa milele. Ilikuwa mapatano rahisi yaliyofanywa kwa imani rahisi.

Ninapotafakari miaka yangu ya msingi, ninauona mkono wa Mpendwa wangu mahali kwingi sana. Mawe ya msingi yaliwekwa ambayo yalinipelekea kumfahamu Bwana wangu. Ingawa licha ya faida hizi zote, urithi wangu kutoka kwa Adamu na mazingira niliyokulia yalifanya ubatizo wa utotoni mwangu kuwa na maana ndogo kuliko ilivyotarajiwa. Katika miaka yangu yote ya masomo niliyokuwa nimepokea, bado kwa kweli sikujua mambo yakutosha kumhusu Mpendwa wangu ili kufanya ubatizo wangu kuwa na maana kamili. Pia kulikuwa mikondo kadhaa iliyopita ikibeba kanisa langu na ambayo ilikuwa ikimpeleka Mpendwa wangu mbali zaidi na mbali na ufahamu wangu.

Ninaamini kwamba Mungu alipendezwa na kiapo changu kwake na Mwanawe, ingawa kiapo rahisi cha utoto wangu karibuni kilikuwa kimedhoofishwa kabisa na mavuno ya magugu ambayo yule muovu alikuwa amefanikiwa kupanda maishani mwangu.

## 3. Mkanganyiko

Sauti ya Mpendwa wangu iliteua utoto wangu kupitia kwa ulinzi wa upendo tefu wa wazazi wangu, mkutano wangu na maumbile na visa vya Bibilia. Ushawishi ulikuwa laini na wenye hila, ingawa sasa natabasamu ninapoangazia juu ya amani, utulivu na baraka amabayo ningehisi katika makabiliano hayo. Ni jinsi gani natamani hii ingekuwa sauti tu ambayo masikio yangu yangesikia milele.

Ilikuwa vigumu kwangu kusikia sauti ya Mpendwa wangu kwa kuwa ingawa alikuwa karibu nami zaidi, alisikika kuwa mbali. Sauti nyingine ilionekana kuwa karibu zaidi. Ilikuwa juu zaidi, ilikuwa ya kusisitiza zaidi na hata ya kulazimisha wakati mwingine. Sauti hii inaweza jumuishwa vyema katika mafungu haya:

> Nawe ulisema moyoni mwako, Nitapanda mpaka mbinguni, Nitakiinua kiti changu juu kuliko nyota za Mungu; Nami nitaketi juu ya mlima wa mkutano, Katika pande za mwisho za kaskazini. (14) Nitapaa kupita vimo vya mawingu, Nitafanana na yeye Aliye juu. Isaya 14:13-14.

Sauti hii ilikuwa na mwangui asilia kwangu. Ilipendekeza kwamba furaha ilipatikana katika burudani na pumbao, katika pipi (lollies katika Australia!) na vinyago, katika kuteka makini na pongezi. Awali katika uzoefu wangu nilibaini kwamba kushikilia hadhira, kuwafanya wacheke au kuwafanya wakutukuze kulileta kiwango cha juu cha kuridhishwa. Hisia ambazo ziliosha roho yangu zilihisi sawa na zile ambazo zilinijia kutoka kwa kutazama mbingu au kwa kukumbatiwa na wazazi wangu. Zote zilihisika kuwa nzuri; singeweza kubaini tofauti kati ya sauti.

Sauti hii ilinishawishi kutafuta furaha katika keki, pipi, malai ya barafu na vinywaji. Malezi ya kujizuia yalinisababisha kulalamika kwa nguvu na kwa muda mrefu hadi fimbo ya marekebisho iliponiangukia. Televisheni ilikuwa mwelimishaji muhimu. Nilitazama wahusika wenye nguvu kubwa wakiwashinda adui hatari zaidi. Niliona familia zilizokuwa sawa na yangu zikikabiliana na changamoto kwa werevu wao wenyewe bila haja ya

maombi. Niliwatazama watoto wa senema wenye kuonyesha mwisho mzuri bila hisia za haja ya Mungu, Bibilia au ombi.

Sehemu ambayo haijazungumziwa ya mafunzo yangu ya kielimu shuleni ilikuwa kwamba furaha ilipatikana kwa kupata utambuzi na makini ya walionizunguka. Sheria hii ambayo haijaandikwa ilinipendekezea kwamba kama nilihitaji uthibitisho, ninahitaji kusoma kwa nguvu. Kama mtoto mchanga, kusoma kwa bidii hakukuwa kunapendeza kabisa; kwa hivyo niligundua njia zingine za kuteka makini! Kucheza chale kuliteka makini ya wanafunzi wote na kumfanya mwalimu kutamatisha darasa kwa sababu yangu tu! Ilipendeza ilipodumu. Ingawa fimbo ya marekebisho ilinijuza kwamba kulikuwa na gharama ya kutafuta aina hii ya makini.

Kwa kuakisi, sauti ya mshawishi ingenisukuma kwa njia panda. Pengine ningeshawishiwa kuteka makini kwa kucheza chale na kuwatia katika watawala maishani mwangu au kutafuta kuteka makini ya watawala na kutamaniwa na marafiki kupitia kwa kusoma kwa bidii, kufanikiwa na kuwa mtoto wa kutolewa mfano. Njia yoyote ile, sauti hii ilipendekeza kwamba furaha huja kutoka kwa kuteka makini ya hadhira kwa kiwango fulani.

Kadri nilivyohisi kukubalika kidogo na wazazi wangu, ndivyo sauti ya mshawishi ingenisukuma zaidi kuwatia watawala katika changamoto na kucheza chale. Kadri nilivyohisi kukubaliwa na wazazi wangu, ndivyo ningijitahidi zaidi kujitofautisha kwa alama nzuri shuleni. Ila haya hayakuwa yote. Pia ningetafuta kuonyesha familia yangu na rafiki zangu kwamba nilikuwa mkristo mzuri. Katika muktadha huu sauti ya Mpendwa wangu na sauti ya mshawishi zilisikika karibu kufanana.

Mpendwa wangu alitaka niwaheshimu wazazi wangu, nisome Bibilia, niombe na nifanye vyema katika masomo yangu. Ingawa mshawishi alipoona kwamba nilitamani thibitisho ya walio katika utawala juu yangu, angenitia moyo kufanya vitu sawa kabisa, ila kwa kusudi tofauti kabisa. Kama mtoto sikuwa na uwezo wowote wa kufahamu na kutambua tofauti ya kusudi. Mtoto hufahamu tu kwamba hupokea amri na kuchagua kutii au kutotii. Hakuna ufahamu wa mbona akachagua kutii au kutotii.

> Lile nisemalo ni kwamba wakati wote mrithi akiwa bado ni mtoto, hana tofauti na mtumwa, ingawa ndiye mmiliki wa mali yote. (2) Yeye huwa yuko chini ya uangalizi wa walezi na wadhamini mpaka ufike wakati uliowekwa na baba yake. (3) Vivyo hivyo na sisi, tulipokuwa bado watoto wadogo, tulikuwa utumwani chini ya taratibu za kawaida za ulimwengu: Wagalatia 4:1-3.

Ushawishi wa Mpendwa wangu kupitia kwa wazazi wangu na visa vya Bibilia ulinithibitishia kwamba kutafuta kujulikana vibaya kwa kupinga utawala kulikuwa kosa na pia kuchungu. Hitimisho hizi kweli hazikuwa na fahamu; zilikuwa tu mtazamo usiokuwa na fahamu. Hivyo nilipendelea njia ya makini kupitia kwa kufanya bidii, jitihada na mafanikio yanayokubalika. Hili halikumaanisha kwamba sikuangukia njia nyingine watawala walipoonekana kukosa haki, kupendelea au wasioendana. Nilijifunza kwamba hata baada ya bidii, lengo la heshima bado lingeniepuka kwa hila.

Karibu sehemu zote za uzoefu wangu zilinifahamisha kwamba lengo la maisha ni kutafuta makini kupitia kwa mafanikio. Kulikuwa na moja peke, sauti ambayo bado ilijaribu kuniambia jambo tofauti. Nilipojisomea Bibilia katika wakati wa miaka kumi na miwili, nilivutiwa na kisa cha Yesu kufa msalabani kwa wenye dhambi. Nilikuwa nimepokea nidhamu ya kutosha maishani mwangu kujua kwamba nilikuwa mwenye dhambi, ingawa nilihisi kwamba sikuwa mbaya kama wengine!

Kisa cha msalaba kilinipendekezea kwamba Mungu aliwapokea watu jinsi walivyo bila kuzingatia mafanikio yao. Najua kwamba mpendwa wangu alikuwa akiniita, lakini sauti ilikuwa laini sana ikilinganishwa na sauti hiyo nyingine ambayo ilinipendekezea kwamba mbingu iligharamika sana kukabiliana na tatizo langu la dhambi na kwamba kama vile Mungu aliingia katika shida hii yote ya kumtuma Mwanawe kufa kwa ajili yangu basi hakika nilihitaji kumuonyesha kwamba ninashukuru. Nilihitaji kuonyesha kwamba nilifaa juhudi na jitihada hii yote.

Hili lilileta maana kubwa ndani yangu. Nilipambanua kutoka kwa makabiliano yangu mengi na watawala binadamu kwamba wakati uliotumika kunirekebisha ulisababisha muwasho na ulitumia mali ya

thamani ambayo vinginevyo yaliwekwa kwa sababu inayostahili. Kama sauti ya mshawishi iliavyo wakati wote:

> Kwa nini ubadhirifu huu wote? Mathayo 26:8

Hivyo tunaona kwamba kupitia kwa pambio inayotawala ya kutafuta makini, ishara ya kudumu milele ya upendo wa Baba kwa watoto wake ya kumtoa Mwanawe kufa iligeuzwa kuwa sababu kuu ya kupata idhini kwa kuonyesha shukurani zangu kupitia kuzingatia kwa imani nidhamu ya maisha ya Mkristo. Uchochezi huu nafsini mwangu wote ulikuwa kiinitete kwa miaka kumi na miwili, ila mbegu zilipandwa na wakati wa mavuno ulikuwa unakuja.

Baada ya ubatizo wangu sauti ya mshawishi ilinikumbusha kwamba nilikuwa nimefungwa katika kuwa mvulana mzuri na kwa wakati huo ilinihimiza kuteka makini kwa njia kongwe na mbinu zinazojulikana. Kama Mkombozi wangu mbele yangu, alikuwa ananijaribu nijithibitishe kwa *kugeuza mawe kuwa mkate au kuruka kutoka juu ya hekalu* kupata makini. Sabato ilikuwa uzoefu mgumu zaidi katika sura ya akili. Ilikuwa kama kupanda Mlima Zayuni kila siku ya saba. Katika kipindi cha muda mfupi wa ubatizo wangu, nilianza kukata tamaa kuweza kumpendeza Mungu. Kidogo sana cha hili kilikuwa dhahiri akilini mwangu; ilijiweka wazi tu katika kushuka taratibu kwa hisia za kiroho, nafsi yake ikichukuliwa na shughuli za kunisaidia kusahau nilichokuwa nimeapa kwa Mungu.

Nikitazama nyuma sasa, ninaona hila za ujanja wa mshawishi zikinivuta katika hamu ya kumradhi Mungu ikiongozwa na hamu ya msingi ya kupata makini na idhini. Nilianguka katika matokeo ya kutabirika ya kutafuta kujitumbukiza katika burudani ya muachano. Hapo katika miaka muhimu ya ujana, nikawa chombo cha kuendesha tamaa za sasa zilizozaliwa katika upepo wa kujiinua. Katika nafasi ya miaka mitano nilikuwa nikitafuna maganda katika mabwawa ya nguruwe.

Mafunzo yangu ya utotoni yalinizuia kutumbukia kwa kina katika kujiumiza na unyanyasaji ambao vijana wengi hujipata, ingawa hisia


zilikuwa za mavuno sawa. Namshukuru Mpendwa wangu sana kwamba sikukumbana na vidonda halisi ambavyo vijana wengi wanashuhudia.

Naweza tu fikiria jinsi ilivyokuwa vigumu kwa Mpendwa wangu kunitazama nikipokea kwa urahisi sauti ya mshawishi na kufuata mapendekezo yake. Ni jinsi gani ilikuwa vigumu kunitazama ni kivuna mazao niliyokuwa nimepanda. Mara nyingi nilifikiria kwamba sauti iliyokuwa ikiniongoza hakika ilikuwa sauti ya Mpendwa wangu wakati ambao kwa huzuni ilikuwa sauti ya adui yangu.

Natetemeka kwa kufikiria kwamba nilijua machache sana kumhusu Mpendwa wangu kwamba singepambanua sauti yake kutoka kwa ile ya mshawishi. Mwanga wenye joto uliokuja kuto kwa kupokea zawadi shuleni mbele ya mariika yangu ulihisika sawa na kumbatio laini la baba yangu. Kicheko kilichopasuka kutoka kwa uigizaji wangu kilihisika sawa na wakati nilipotazama kwa hofu juu ya nyota za mbinguni. Vitendo vya kusoma Bibilia, kuomba na kuhudhuria kanisa vilitamaniwa na Mpendwa wangu na pia vilevile na mshawishi wangu, ingawa kwa sababu tofauti kabisa ambazo zilikuwa zaidi ya ufahamu wa akili yangu iliyokuwa ikikua.

Vita vya kuelezea sauti hizi mbili tofauti vitafunguliwa katika sura zijazo. Ninaomba kwamba unapotafakari mambo haya utaweza kupambanua hali ya vita hivi na uwembamba wa njia ya uzima. Wazo kwamba ningepokea kwa urahisi mshawishi na kumuumiza Mpendwa wangu ni chanzo cha aibu na udhalilishaji kwangu, lakini ninaamini katika msamaha wake wa rehema na utulivu tefu.

## 4. Lango




Kurudi nyuma katika kiapo nilichokula kwa Mungu kwa njia ya burundani ya muachano kulianza kuvuna mazao ya kizunguzungu chenye uwiano. Uzoefu wangu wa mchezo wa mzunguko ulionekana kwenda upesi kwa kila mzunguko wa kukaza. Hitaji la kupewa kipaumbele na kukubalika liliweka madai yaliyoongezeka zaidi juu yangu, wakati ambao fursa za kufanikiwa zilionekana kudidimia.

Watu wengi wachanga wanaong'ang'ania nafasi ya kati ya kupewa kipaumbele katika mbinu kadhaa za utamaduni wangu wanaweza kutazamwa na watu wachache kwa wakati mmoja. Ndoto na matarajio yaliyopendekezwa na mshawishi na kukuzwa ndani ya moyo wangu zilizanza kuvuna mazao yanayoweza kutabiriwa ya kupuuza. Mara nyingi ningejifikiria ni kifanya mafanikio makuu ambayo riika yangu yote, jamii yangu na taifa wangepongeza wanamichezo wa kishujaa kutoka Australia wakipokea nishani ya dhahabu katika nyanja waliojichagulia na mshawishi angeninong'onezea kwamba hii ndio ilikuwa njia ya wokovu.

Kuhalalisha uwepo wangu kwa mafanikio tofauti ya akili na mwili ilionekana kuwa suluhisho kamili la kukabiliana na hasira ya kufikiria niliyokuwa nimemsababishia Mungu, wazazi wangu, na kanisa langu kwa kushindwa kwangu. Hamu hii ya kuhalalisha uwepo wangu ilikuwa asili na asilika kama kupumua. Sikuwa na ufahamu kwamba nilikuwa navikwa ibada ya Kaini, akitafuta kutoa kile ambacho alikuwa nimevuna kama kafara ya kumwabudu Mungu. Kwa kuisikiliza sauti ya mshawishi, pasipo kujua nilijiweka katika mgongano huu na sheria ya uzima. Uhalalishaji wa uwepo wangu kupitia mafanikio kwa kulinganisha na wengine ni kinyume cha uhusiano wa kupenda na kujali na watu wao hao. Urafiki wa kweli ulinyiririka kutoka ndani yangu bila kufahamu kwa sababu kila mmoja aliyenizunguka alikuwa na uwezo wa kuwa tisho kwa malengo yangu au

kinyume mshiriki wa kutumika kuafikia malengo hayo. Ila wakati wote nilitamani kupendwa na kuwa na marafiki wa karibu.

Nguvu hizi pinzani zingeibuka nafsini mwangu kutoka wakati hadi wakati kama ishara ya onyo kwa njia ambayo nilikuwa nikifuata. Ninakumbuka kwa usahihi mchezo wa mpira wa vikapu uliosababisha kuibuka kwa wote kuona. Nilikuwa nimefanikiwa kuondoa mpira kutoka kwa mpinzani katika nafasi muhimu ya mchezo, lakini mwalimu mwamuzi alifanya uongo dhidi yangu. Roho wa mafanikio alilenga kuhusu kujihalalisha kwa muda alifunga aina zote za heshima kwa mwalimu wangu kwa kutoa mito ya maneno ya hasira kwa uamuzi wake usiosahihi. Nilipoteza kabisa hisia zote za wajibu wangu wa kuheshimu watawala. Hasira zilinianza na kupendekeza majibu mbalimbali yasiyokuwa na maadili.

Nilisikia sauti ya Mpendwa wangu ikininenea. Kimya kimya kwa maswali, "Uko sawa Adrian? Kweli hivi ndivyo unataka kuwa?" katika nafasi muhimu ambapo mshawishi alikuwa akivuna mazao ya uasi kutoka kwangu, Mpendwa wangu aliweza kuniuliza kama nilipenda ladha ama nilihitaji kitu bora. Katika vina vya giza niliwezeshwa kutofautisha tofauti katika sauti. Giza, zimbaa, roho wa kulipiza kizazi ambaye alikuwa amechukuwa utawala ndani yangu sasa alikuwa tofauti na sauti tefu, tamu na tulivu ya Mpendwa wangu.

Mwamuzi alinipiga marufuku kutoka kwenye mashindano. Mshawishi alipendekeza kulipiza kisasi; Mpendwa wangu alipendekeza nifikirie kwa makini njia zangu. Sauti zilikuwa zikipanuka, na pambano kuu nafsini mwangu lilikuwa kubwa. Hii ilikuwa fursa muhimu maishani mwangu—fursa ya milele ambapo uamuzi uliofanywa ungeweka mwendo wa njia yangu. Mpendwa wangu aliniita kwa namna ya kurudisha ndani yangu hamu ya ndani ya kubadilika. Sikutaka kuwa mbaya, mwenye fujo au mwenye vurugu; nilitaka amani, furaha na upendo. Mlango ulianza kuchukua sura akilini mwangu; uamuzi ulikuwa ukianza kuchukua lengo. Hamu hii ilikuwa itiwe nguvu kwa marobota zaidi kutoka kwa mapendekezo ya mshawishi.

Mzee wa siku mwenye hekima yote hakukejeliwa na ujinga wangu. Riziki iliruhusu kwamba mfuatano wa matukio yakiwekwa pamoja kwa mfululizo wa haraka yalinifanya nitake kuacha chumba cha nguruwe na kurejea kwa nyumba ya baba. Nguvu za tectoniki za hamu yangu zilipogongana, nilipewa picha fupi ya tabia yangu ya dhambi ambayo singeficha. Kwa kila zao ambalo mshawishi alikuwa anafaidi kutoka kwangu, ndivyo ulivyo kuwa wito mkuu kutoka kwa Mpendwa wangu kuigeuza miguu yangu kuelekea barabara ya wokovu na kupata uhuru kutoka kwa dhuluma zangu mwenyewe.

Hamu inayooneka kutokuwa na hatia ya kukubaliwa kwa ujuzi na juhudi ziliniacha na ukweli kwamba:

> Tangu wayo wa mguu hata kichwani hamna uzima ndani yake; bali jeraha na machubuko na vidonda vitokavyo usaha; havikufungwa, havikuzongwa-zongwa, wala havikulainishwa kwa mafuta. Isaya 1:6.
>
> Kama ilivyoandikwa: Hakuna mwenye haki, hakuna hata mmoja. (11) Hakuna hata mmoja mwenye ufahamu, hakuna hata mmoja amtafutaye Mungu. (12)Wote wamegeukia mbali, wote kwa pamoja hawafai, hakuna atendaye mema, naam, hata mmoja. Warumi 3:10-12.

Mpendwa wangu alionyesha ujuzi huo na hekima katika kukabiliana nami. Alijua uchungu ambao ningepitia, ila akanirusu kuchagua njia ambaya nilitamani. Hakuweka vizuizi vyovyote juu yangu na alitembea nami katika mazao ya uchungu ambayo nilikuwa nimekusanya kutoka kwa mshawishi. Kila nilipoanguka, hakunizomea, hakunilaumu, na hakuonyesha roho wa kukasirishwa. Aliniuliza tu kama nilihitaji kitu bora; aliniacha nionje upendo wake kidogo kwa kuchumbia moyo wangu. Mlango sasa ulikuwa wazi mbele yangu. Nilitambua minyororo iliyokuwa mikononi, miguuni na shingoni mwangu. Sasa ningeona kwamba nilikuwa nimefungwa kwa uharibifu fulani, bado tumaini kutoka kwa Mpendwa wangu iliangaza kwa kina ndani ya nafsi yangu.

Kisha akasema Mwinjilisti, “Mbona hauko tayari kufa, kwa vile maishaa haya yamejawa na maovu mengi?” mtu huyu akajibu, “kwa sababu, ninahofu kwamba mzigo huu ambao uko mgongoni mwangu utanizamisha ndani zaidi kuliko kaburi, na nitaanguka katika Tofethi. Isa. 30:33. Na bwana, kama siko sawa kwenda gerezani, siko sawa kwenda hukumuni, na kutoka kwa hilo kuuawa; na mawazo ya mambo haya hunifanya kulia.”

Kisha akasema Mwinjilisti, “kama hii ndio hali yako, mbona umesimama wima?” alijibu, “kwa sababu sijui kwa kuenda.” Kisha akampa vile vya ngozi, na kulikuwa kumeandikwa ndani yake, “kuikimbia ghadhabu inayokuja.” Matt. 3:7.

Mtu huyu kwa hivyo alilisoma, na kwa kumwangalia Mwingilisti kwa makini, alisema, “nikimbilie wapi?” Kisha akasema Mwinjilisti, (akionyesha kwa kidole uwanja mkubwa sana,) “unaona lango ndogo kule?” Matt. 7:13,14. Mtu huyu akasema, “Hapana.” Kisha akasema mwingine, “unaona nuru ikiangaza kule?” Zaburi 119:105; 2 Pet. 1:19. Akasema, “nadhani naona.” Kisha akasema Mwinjilisti, “dumisha nuru hiyo machoni mwako, na uende moja kwa moja hadi hapo, hivyo utaona lango; ambalo, ukilibisha, utaambiwa kile ambacho utafanya. *Pilgrim’s Progress* Stage One.

## 5. Madhabahu ya Shaba



Sasa nilijua kwamba nilihitaji Mkombozi. Msukosuko uliochochea nafsini mwangu ulinifanya kutamani mbingu ya pumziko. Kupitia kwa usimamizi makini, Mpendwa wangu alinisaidia kuelewa kwa uwazi kabisa sauti ya mshawishi. Nilikuwa sasa nikiukimbia mji wa uharibifu, ingawa sikuwa na uhakika nifuate njia ipi. Moyo wangu ulivutwa kumfikiria Yesu. Kwa mara ya kwanza maishani mwangu nilihisi hamu ya kutaka kumjua. Nilikuwa nimefunzwa kwamba Yesu alikuwa Mkombozi apendaye katika miaka yote sabini ya maisha yangu, ila hata sasa, sikuwa nimetambua hasa ni kutoka kwa nini nilihitaji kuokoka.

> Yesu akawaambia, Mimi ndimi njia na kweli na uzima. Mtu hawezi kuja kwa Baba isipokuwa kwa kupitia Kwangu. Yohana 14:6.

Njia ya kuwa huru ilikuwa kupitia kwa Kristo, ila vipi? Katika umri wa miaka kumi na miwili, nilikuwa nimemkubali Yesu kama Mkombozi wangu, nilikuwa nimeungama dhambi ambazo nilifahamu na niliamini kwamba angekuja tena kwa ajili yangu. Ingawa, kuna kitu ambacho kilikosekana. Kwa vile sikuwa nafahamu kina cha utumwa wangu, sikuthamini karama ya Mkombozi wangu.

> …Lakini yule aliyesamehewa kidogo, hupenda kidogo. Luka 7:47.

Kitabu "*Steps to Christ*" kilinijia akilini na nikawaza "Hiki ndicho kitabu hasa ambacho nilihitaji." Pasi tena kusoma kwa lengo la kuonyesha juhudi za kidini na pasi tena kutafuta kumwonyesha Mungu nilikuwa na shukurani, maneno ambayo nilisoma yalianza kupenya nafsini mwangu.

Maumbile na ufunuo kwa usawa yanashuhudia upendo wa Mungu. Baba yetu aliye mbinguni ni chanzo cha uzima, hekima na furaha. *Steps to Christ*, page 9.

Mungu ameifunga mioyo yetu kwake kwa ishara zisizohesabiki mbinguni na duniani. Kupitia kwa vitu vya maumbile, na kwa mahusiano kamili na tefu ya ulimwengu ambayo moyo wa mwanadamu unaweza jua, ametaka kujidhihirisha kwetu. Ibid, page 10.

Mwana wa Mungu alikuja kutoka mbinguni ili kumdhihirisha Baba. "Hakuna mtu ye yote aliyemwona Mungu wakati wowote, ila ni Mungu Mwana pekee, aliye kifuani mwa Baba ndiye ambaye amemdhihirisha." Yohana 1:18. "Wala hakuna amjuaye Baba, ila Mwana, na yeyote ambaye Mwana apenda kumfunulia." Ibid, page 11.

Maneno haya yalipata gumzo moyoni mwangu. Vifungo vya furaha vilinijia nilipowaza Yesu akija kudhihirisha upendo wa Baba kwetu. Kisha ulianza kumueleza.

Alizunguka akitenda mema na kuwaponya wote walioteswa na Shetani. Kulikuwa na vijiji vizima ambavyo hapakuwa na mguno wowote wa ugonjwa katika nyumba yoyote, kwa kuwa alikuwa amewapitia na kuwaponya wagonjwa wao wote. Kazi yake ilitoa ushahidi wa kuteuliwa kwake kutakatifu. Upendo, rehema, na huruma zilidhihirishwa katika kila tendo la maisha yake; moyo wake ulikuwa wa huruma tefu kwa wana wa Adamu. Alichukua hali ya mwanadamu, ili aweze kufikia mahitaji ya mwanadamu. Masikini na wanyenyekevu hawakuhofu kumkaribia. Hata watoto wachanga walivutiwa naye. Walipenda kupanda juu ya goti lake na kutazama uso wake wa kupendeza, wa upole na upendo.

Yesu hakuhusuru neno moja la kweli, ila alilitamka daima kwa upendo. Alionyesha umahiri mkuu na uzingativu, ukarimu katika mwingiliano wake na watu. Kamwe hakuwa mjeuri, hakunena neno kali bila sababu, kamwe hakuipa nafsi nyeti uchungu bila sababu. Hakulaumu udhaifu wa mwanadamu. Alizungumza

> ukweli, lakini kwa ukweli daima. Alishtumu unafiki, kutokuamini, na uovu, lakini machozi yalikuwa kwenye sauti yake alipotamka kemeo hili kali. Alilia juu ya Yerusalemu, mji alioupenda, ambao ulikataa kupokea, njia, ukweli, na uzima. Ibid, page 11, 12

Nilihisi moyo wangu umefunguka kwa Mpendwa wangu. Alikuwa mtu ambaye hakulaumu udhaifu wa mwanadamu, alijawa na huruma, na alionyesha adabu. Watoto wachanga walipenda kupanda juu ya goti lake! Nilipowaza kumhusu nikimlinganisha nami, nilihisi giza la aibu likitafuta kuziba njia za nuru iliyokuwa ikiingia nafsini mwangu. Ni mtakatifu zaidi, msafi na mwenye haki na mimi sio mwenye haki, mchafu na mbinafsi. "Haina haja," ananogoneza mshawishi. "Endelea kusoma, Adrian," anajibu Mpendwa wangu.

> Kila nafsi ilikuwa ya thamani machoni pake. Wakati alichoshwa na heshima yake takatifu, alinyenyekea kwa zabuni ya kujali kila mshiriki wa familia ya Mungu. Ndani ya watu wote aliona mioyo iliyoanguka, ambayo ilikuwa kazi yake kuiokoa. Hiyo ndio tabia ya Kristo kama inavyodhihirishwa katika maisha yake. Hii ndio tabia ya Mungu. Ni kutoka kwa moyo wa Baba ndio kijito cha huruma takatifu, inayodhihirishwa katika Kristo, kinatiririka kwa wana wa Adamu. Yesu, mkombozi tefu, wakuhurumia, alikuwa Mungu. "Alidhihirishwa katika mwili wa kibinadamu." 1 Timotheo 3:16. Ibid, page 12.

Kweli nilikuwa wa thamani machoni pake? Inaweza kuwa kwamba ni kweli?

> Msinichunguze kwa kuwa ni mweusi-mweusi, Kwa sababu jua limeniunguza. Wana wa mamangu walinikasirikia, Waliniweka niwe mlinzi wa mashamba ya mizabibu; Bali shamba langu mwenyewe sikulilinda. Wimbo Ulio Bora 1:6.

Mshawishi lazima alikuwa amehisi kwamba tumaini lilikuwa likipanda moyoni mwangu. Kama ningejaribu kuamini kwamba Mungu alinipenda na akamtuma mwanawe kunikomboa, basi kazi yake ya uharibifu katika

maisha yangu ingefanywa ngumu zaidi. “Waza kuhusu dhambi zako, Adrian!”

> Hivyo Mkristo aliachwa kutumbukia katika kukomaa kwa kujipapatua peke yake, lakini bado alijitahidi kung’ang’ana kwa upande huo wa kujipapatua ambao ulikuwa mbali na chumba chake, na karibu na lango ndogo; ambalo alikuwa nalo, lakini hangetoka nje kwa sababu ya mzigo uliokuwa mgongoni mwake: lakini niliona katika ndoto yangu, mtu alimjia, ambaye jina lake lilikuwa Saidia. *Pilgrim’s Progress* Stage One

“Endelea kusoma Adrian.” Mpendwa wangu aliashiria.

“Ndio, nataka kuendelea kusoma.”

> Ilikuwa kutukomboa ndio Yesu aliishi na kuteseka na kufa. Akawa “Mtu wa huzuni,” ili kwamba tuweze kuwa washirika wa furaha ya milele. Mungu alimruhusu Mwanawe mpendwa, aliyejaa neema na ukweli, aje kutoka kwa ulimwengu wa utukufu usioweza kuelezewa, hadi kwa ulimwengu uliogubikwa na kukumbwa na dhambi, kutiwa giza na kivuli cha mauti na laana. Alimruhusu kuacha kifua cha upendo wake, ibada ya malaika, kuteseka aibu, matusi, udhalilishaji, kuchukiwa, na kifo. “Adhabu ya amani yetu ilikuwa juu yake, Na kwa kupigwa kwake sisi tumepona.” Isaya 53:5. Mtazame jangwani, Gethsemane, msalabani! Mwana wa Mungu asiye kuwa na doa alibeba juu yake mzigo wa dhambi. Yeye aliyekuwa na Mungu, alihisi moyoni mwake utengano mkubwa ambao dhambi huleta kati ya Mungu na Mwanadamu. Hili lilitoa midomoni mwake kilio cha dhiki, “Mungu wangu, Mungu wangu, mbona umeniacha?” Mathayo 27:46. Ulikuwa mzigo wa dhambi, hisia ya ubaya wake wa kutisha, wa utenganisho wake wa nafsi kutoka kwa Mungu—hili ndilo lililovunja moyo wa Mwana wa Mungu. Ibid, page 13.

Niliketi kwa kuduwaa. Kwa maneno “Mtazame msalabani,” mawazo yangu yalichora taswira ya eneo hili. Hapa msalabani alisulubiwa Mwana wa Mungu, alipigwa, akachapwa na kupondwa na kwa nini, kwa ajili yangu? Pambano kuu lilikuwa likiendelea akilini mwangu.

"si stahili upendo wa namna hii…"

"Kristo amekufa kwa ajili ya dhambi zako, amini tu…"

Kisha nilisoma maneno:

> Mwana wa Mungu asiye kuwa na doa alibeba juu yake mzigo wa dhambi. Yeye aliyekuwa na Mungu, alihisi moyoni mwake utengano mkubwa ambao dhambi huleta kati ya Mungu na Mwanadamu. Hili lilitoa midomoni mwake kilio cha dhiki, "Mungu wangu, Mungu wangu, mbona umeniacha?" Mathayo 27:46. Ibid, 13.

Siwezi elezea jinsi ilinijia, lakini nilihisi kwamba Yesu alikuwa amekufa msalabani kwa sababu ya dhambi zangu na kwamba zilikuwa dhambi zangu pamoja na ulimwengu wote zilizomfanya Yesu kulia, "Mungu wangu, Mungu wangu, mbona umeniacha?'' nilipochora taswira ya tukio, niliutazama uso wa Yesu na akageuka na kunitazama bila hata onyesho moja la hasira, masikitiko na kukatishwa tamaa. Niliona tu upendo na kukubalika.

"Ninaamini, Bwana naomba uje moyoni mwangu na uyatawale maisha yangu. Nakushukuru kwa kunipenda na kunikomboa…"

Nilikuwa nimeridhishwa kikamilifu kwamba kifo cha Kristo kilitosheleza hitaji la sheria. Rehema ya Mungu ilifikia mtazamo wangu wa haki ya dhambi. Katika aloi hii ya Shaba[1] msamaha wangu ulipatikana.

Wakati huo mlipuko wa amani uliingia nafsini mwangu. Nilihisi minyororo shingoni mwangu, miguuni na mikononi imeanguka. Kisha mto wa machozi ulifuriko kutoka moyoni mwangu. Nilipiga magoti nikalia na kulia. Hisia yangu yote ya hatia, unafiki, uasi, maneno yangu makali na ya kukata, mawazo yangu maovu yote yalikuwa yamesamehewa. Nilionja upendo wa Yesu.

---

[1] Madhabahu ya kafara yalikuwa madhabahu ya shaba. Kafara ya mwanakondoo ilitosheleza mahitaji ya haki iliyojulikana ila Bibilia inatwambia kwamba Mungu kamwe hakutaka kafara. Zaburi 40:6. Ila katika huruma yake kuu Mungu alishuka kukutana nasi tulipokuwa ili tuwezi kuwa na uhakika kwamba tumesamehewa

Hata sasa ninapoandika na kukumbuka tukio hili, moyo wangu unapata joto na macho yangu yanakuwa na unyevu. Siwezi kuweka katika maandishi kwako jinsi nilihisi kumhusu Mkombozi wangu wakati huo. Utengo, oh, utengo! Alikuwa tayari kuvumilia utengo kutoka kwa Baba kwa ajili yangu. Hilo liligonga kwa kina moyoni mwangu. Kama alikuwa tayari kufanya hili kwa ajili yangu, lazima ninastahili kitu, na kama Mungu alikuwa tayari kumtoa Mwanawe—nilipoa na kuruhusu mawimbi yaliyovimba kuosha nafsi yangu. Kama kweli Mungu alikuwa tayari kumtoa Mwanawe kwa ajili yangu, basi naamini kwamba Mungu alinipenda.

> Sasa niliona katika ndoto yangu, kwamba barabara kuu ya kwenda juu ambayo Mkristo angepitia, ilikuwa imewekwa ua pande zote kwa ukuta, na ua huo uliitwa Wokovu. Isaiah 26:1. Kupanda njia hii, kwa hivyo, Mkristo aliyelemewa alikimbia, lakini sio bila ugumu mkubwa, kwa sababu ya mzigo mgongoni mwake. Alikimbia na kwa hivyo akafika mahali kiasi fulani pa kupanda; na mahali pale kulisimama msalaba, na chini kidogo, upande wa chini, kaburi. Hivyo niliona katika ndoto yangu, kwamba kama tu Mkristo alivyopanda na msalaba, mzigo wake ulifunguliwa kutoka mabegani mwake, na ukaanguka kutoka kwa mgongo wake, na ukaanza kutumbukia hadi ulipofika kwenye kinywa cha kaburi, ambapo ulianguka ndani, na sikuuona tena. *Pilgrim's Progress* Stage Three.

## Kingilio I


Ninapotazama machoni mwa Mpendwa wangu, nimepotea kwa mazingira yangu yote. Nahisi kukubaliwa naye; najua kwamba napendwa. Oh mwana wa Adamu, ni kwa jinsi gani namiliki fadhila hii? Nilijaribu kuyageuza macho yangu kutoka kwa mtazamo wake, lakini tazamo lake la upendo linanihakikishia tena. Hili ni kweli! Kweli linatendeka na ni kwangu! Ananipenda kweli, na inampendeza Baba kwamba tutakuwa pamoja. Moyo wangu unajawa na furaha, mwanga wa jua unacheza nafsini mwangu harufu nzuri ya Ukombozi inapojaza kila pembe ya uwepo wangu.

Mpendwa wangu ni mkuu, ni shupavu. Alizichukua dhambi zangu kaburini. Alivumilia kutengwa kutoka kwa kumbatio la Baba yake. Haya yote kwa ajili yangu! Oh mfalme mkuu zaidi, umeuteka moyo wangu. Siwezi kataa ushawishi wako. Nimesamehewa? Ndio, nimesamehewa, na dhambi zangu zote zikaondolewa. Na vazi nyeupe na safi nimepewa, lililoshonwa kwa mfumo wa mbinguni bila hata uzi mmoja wa fikira za mwanadamu.

Baba mpendwa, Mwanao ni karama isiyoweza kuelezewa, ingawa, uliitoa kwa hiari. Naelewa mbona Mwanao anapendeza; vyote alivyonavyo vinatoka kwako. Sielewi mbona ufanye hili, lakini kama mtoto mchanga nalia kwa furaha “Abba, Abba.” Sijaachwa, ninaye Baba na Mwanawe ni Mpendwa wangu.

Oh Mwana wa Adamu, moyo wangu unaenda mbio kwa furaha. Nani angejua kwamba wokovu ungekuja nyumbani mwangu kupitia kwa kumtazama Mwana aliyeinuliwa? Naamini. Ndio, naamini. Mpendwa wangu ni wangu nami ni wake.

## 6. Birika ya Shaba



Ninyi waume, wapendeni wake zenu, kama vile Kristo alivyolipenda Kanisa akajitoa kwa ajili yake, (26) kusudi alifanye takatifu, akilitakasa kwa kuliosha kwa maji katika Neno lake. Waefeso 5:25-26.

Hapo mwanzo, alikuwako Neno. Huyo Neno alikuwa pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. (2) Tangu mwanzo huyo Neno alikuwa pamoja na Mungu. Yohana 1:1-2.

Athari ya kile ambacho Yesu alikuwa amenitendea msalabani ilibadilisha kila suala la maisha yangu. Nilitaka kuwa naye kila wakati. Nilipenda kuwaza kumhusu, kumuiga, na kuleta kila kitu maishani mwangu chini ya utawala wake. Niliporuhusu akili zangu kutekwa na mambo mengine kwa saa kadha, ningeanza kuhisi kutoweka kwa uwepo wake na mawazo yangu yalirejea kwa Yesu. Furaha ya kujua dhambi zangu zimesamehewa ilinifanya kuelea kwa majuma kadha. Hivyo ndivyo ilivyo furaha ya upendo wa kwanza.

Furaha hii iligeuza Bibilia kikamilifu. Singeiweka chini. Ghafla nilikuwa na kiu ya ajabu ya kumfahamu Yesu katika Bibilia. Kulikuwa na mambo mengi ya kujifunza na pia ya kusahau. Roho wa Kristo alianza kunitia hatiani kupitia kile nilichosoma. Niliona kwamba vitu kadha vilihitaji kubadilishwa. Neno la Mungu lilianza kusafisha na kufanya upya mawazo yangu. Sasa Neno lilikuwa mtu, sio tu mkusanyiko wa maandishi. Sasa ilikuwa Yesu akinizungumzia moja kwa moja, kwa upendo na binafsi.

Nilipotazama kwenye kioo cha sheria niliona hatia kwa tabia kadha ambazo nilihitaji kubadilisha. Kamwe singevumilia tena kutazama senema zenye kuapisha, vurugu na uasherati. Roho alinisukuma kuwakaribia watu kadha na kuwaomba msamaha kwa tabia zangu mbaya. Baadhi ya watu walijitahidi kuelewa mbona nilihitaji msamaha, nikinukuu kwamba sisi sote ni binadamu. Ingawa kwa kutazama kwa makini katika macho ya Mpendwa wangu kupitia kwa Neno, mambo haya yalionekana ya kawaida

tu. Haki na dhambi zikawa kama usiku na mchana na dhamiri yangu ikawa tefu, yenye lengo, na tahadhari.

Baadhi ya masuala ya mchakato huu wa kuosha yalikuwa ya furaha na ya kuweka huru ingawa kwa matukio mengine kukata kwa Neno moyoni mwangu kulikuwa uchungu, kwa kukabili na kufedhehesha. Ninapotazama nyuma, naona rehema ya Mpendwa wangu haiwasilishi sifa nyingi za dosari na tabia za dhambi hata mara moja. Kama uwezo wote wa kutakasa ungekuwa umeonyeshwa, ningechoka kwa kukatishwa tamaa. Ila kwa kila kiunzi, upendo wa Yesu ulinibeba.

Ni jinsi gani natamani naweza ripoti "na waliishi kwa furaha baadaye na milele," lakini ukweli wa ulimwengu, mwili na ibilisi unafanya tokeo hilo ngumu sana. Miaka yote ya kusikiza mapendekezo ya mshawishi na kukuza tamaa ya kutambuliwa kupitia mafanikio, mawazo yangu yaliwekwa katika mpangilio wa mawazo ambao ni kinyume kabisa cha ufalme wa Mungu. Kwa miezi michache ya kwanza ya kuamini kwangu, sauti ya mshawishi ilikimya ikilinganishwa na ya Mpendwa wangu, ingawa bado alikuwepo. Akikasirishwa na pato jipya la upendo wangu kwa Kristo, alitumia wakati wake, akitafuta sehemu ya kuingilia kurejesha mamlaka na utawala moyoni wangu tena.

Mabadiliko ya kushangaza katika maisha yangu na tabia yalivutia maoni ya dharau kutoka kwa baadhi ya washirika wangu wa zamani. Mshawishi angenisukuma kwa maoni yao. Nikawa mfungwa katika hisia za kutengwa na kukatishwa tamaa. Sikumtambua mshawishi kwa vitu hivi. Nilijua machache kuhusu mbinu zake hivyo basi nikampa faida. Kupitia kwa kujihurumia, adui yangu alipata lango la kuingia moyoni mwangu. Kwa wakati uo huo, baadhi ya mabadiliko ya maisha yangu yakawa vigumu kuyadumisha. Wakati mwingine ningesahau na kuanguka kwa tabia za kale. Na wakati mwingine, kwa kukata tamaa kwa kujua ningetereza kwazo na kuwacha weusi unifunge.

Nilikuwa nimefika kwenye kilima cha ugumu. Hamu ya urahisi, kukosa uvumilivu, na nia ya furaha ilikaa katika utengo kadri ilivyohitajika ilimpa mshawishi fursa ya kufikia aliyokuwa akisubiri. Zaidi ya hili, nilikosa ujuzi

katika Neno na jinsi ya kukabiliana na majaribu ambayo yalijiinua dhidi ya maarifa ya Mungu. Roho wa Kristo alinifunza kukariri Neno.

> Moyoni mwangu nimeliweka neno lako, Nisije nikakutenda dhambi. Zaburi 119:11.

Nilijifunza kwamba niliporudia Neno la Mungu kwa imani kwamba lingekatiza hoja, mawazo na hisia ambazo mshawishi angesukuma nafsini mwangu.

> Kwa maana Neno la Mungu li hai tena lina nguvu tena lina makali kuliko upanga uwao wote wenye makali kuwili, tena linachoma hata kuzigawanya nafsi na roho, viungo na mafuta yaliyo ndani yake, tena li jepesi kuyatambua mawazo na makusudi ya moyo. Waebrania 4:12.

Kama mpendwa angekuwa amenikinga tu kutoka kwa mapendekezo yote ya mshawishi singekua katika tabia. Pia ningejifunza asili ya kweli na ukali wa hali yangu ya anguko. Kupitia kwa migogoro hii ya awali na mwili wangu, nilianza kupambanua uovu wa moyo wangu.

> Moyo huwa mdanganyifu kuliko vitu vyote, una ugonjwa wa kufisha; nani awezaye kuujua? Yeremia 17:9.

Nuru ya ulimwengu iliniangazia njia yangu na kuniruhusu kuanza kuona ambapo nimekuwa na mbona uharibifu fulani ungekuwa kura yangu kama singetii wito wa Mpendwa wangu.

Nilifunzwa kupigana kwa maombi. Wakati mwingine nilipokuwa nikiomba, moyo wangu ulihisi kama jiwe na mbingu zilikuwa juu ya kichwa changu. Kadri nilivyojaribu kuomba zaidi ndivyo nilivyoogopa zaidi. “Dai Neno, Adrian,” sauti ilinijia. “Amini kile ambacho Neno linasema. Usiwe bila imani bali kuamini.”

Mpendwa wangu alinifunza sayansi ya kusubiri katika ufa kati ya kudai na uzoefu wa ahadi. Wakati mwingine nilivuna aibu na kukata tamaa, na hili liliruhusu Mpendwa wangu kunionyesha ubadilishaji, udhaifu na pupa ya moyo wangu. Wakati mwingine nililalamika na kusinasina kwa Mungu kuhusu matatizo yangu, na niliondoka kama nimekatishwa tamaa zaidi

kuliko awali. Huu ulikuwa wakati mgumu, ingawa kupitia kwa wakati huu wote Mpendwa wangu alinihimiza, akanikumbusha kifo chake kwa niaba yangu, na ahadi ya ushirika wa milele naye na Baba yake. Polepole lakini kwa hakika, Neno la Mungu likawa upanga wangu, imani yangu na ngao yangu.

Nakumbuka kwa upendo furaha ya huo upendo miaka miwili ya kwanza ya kutembea na Mpendwa—Mkombozi mwaminifu, Mwalimu na Rafiki. Tamaa yangu moja ilikuwa niwe kama Yesu.

Baada ya miaka kama miwili hivi, maneno ya Maandiko yalijiweka juu yangu.

> Petro akawajibu, Tubuni, mkabatizwe kila mmoja wenu abatizwe kwa jina la Yesu Kristo, ili mpate kusamehewa dhambi zenu. Nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu. Matendo 2:38.

Ingawa kama mtoto nilifunzwa mengi kumhusu Yesu, sikumjua na wakati wa ubatizo wangu nilipomkubali, alimaanisha kidogo sana kwangu binafsi, kwa sababu nilijua machache kujihusu na karibu bure kuhusu Mpendwa wangu. Ubatizo ni kutia muhuri uhusiano kati ya watu wawili ambao wamekuja kupendana. Yesu alikuwa amenipenda wakati wote, lakini sasa nilimpenda na urafiki huu ulihitaji kutiwa muhuri kwa ubatizo.

Nilipoteremka kwa maji ya ubatizo, moyo wangu ulilenga kwa Yesu. Alikuwa furaha na wimbo wangu, na nilifurahia kuweza kumwahidi maisha yangu na kumwita Bwana wangu. Maji yaliyoizika nafsi yangu yaliashiria kuoshwa kwa Neno ambalo lilikuwa likitendeka maishani mwangu. Kazi ambayo ilikuwa imeanza iliweka mbele ahadi kwamba itakamilishwa.

# 7. Mkanganyiko Zaidi

> Mtu wa nia mbili husitasita katika njia zake zote. Yakobo 1:8.

Baada ya zaidi ya muongo mmoja tangu uzoefu wa upendo wangu wa kwanza na Yesu, nilichanganyikiwa. Maisha yangu ya Ukristo yaliviringika; nakuhisi kama wana wa Israeli wakizurura katika jangwa. Kama mtu angependekeza kwamba nilikuwa na mawazo yaliyogawanyika mara mbili, nilitishika na kukasirika. Nilimpenda yesu kwa kina kwa kunifia msalabani, nilitamani kuzitunza amri za Baba kwa uaminifu na niliomba neema na uwezo wa kushinda. Nilikuwa na ushindi, ingawa uthabiti uliniondoka.

Nilikua katika ujuzi wangu wa Maandiko na kufurahia Sabbato nyingi nzuri nikishiriki na familia na marafiki. Ingawa kuna kitu kilichopungua. Jambo lilikosekana na singeweza kulipata. Kwa muda mwingi wa kipindi hiki, sikutambua kikamilifu chochote kilikosekana.

> Nasi sote, tukiwa na nyuso zisizotiwa utaji tunaakisi utukufu wa Bwana, kama kwenye kioo. Nasi tunabadilishwa ili tufanane naye, toka utukufu hadi utukufu mkuu zaidi, utokao kwa Bwana, ambaye ndiye Roho. 2 Wakorintho 3:18.

Bila kujulikana kwangu, Yesu niliyemtazama katika miaka hii alikuwa muunganiko wa ulimwengu mbili tofauti kabisa. Kwa upande mmoja, nilijifunza Yesu mwenye upendo, wa kujali, mwenye huruma ambaye alidhihirisha upendo wa ajabu kwa Baba yake. Nilitafakari pambano ambalo Baba alivumilia kumtoa Mwanawe kwa ajili yetu. Niliwaza kuhusu maisha ya Yesu ya maombi na kuomba kwake kwa ajili yangu na vitu hivi ziliguza nafsi yangu, vikayeyusha moyo wangu na kunipa msukumo wa kuishi maisha ya Ukristo. Ingawa kulikuwa na jambo katika utu wa Yesu, nilijifanya kwamba lilikuwa katika Bibilia na hili lilijenga msingi wa jitihada zangu zote katika maisha ya Ukristo. Nahitaji muda mchache kuelezea kwa kina kilichokuwa kikitendeka akilini mwangu. Kuna sababu kadha zilizonifanya nilie:

> Usiku kitandani nalimtafuta mpendwa wa nafsi yangu, Nalimtafuta, nisimpate. Wimbo Ulio Bora 3:1.

Katika maisha yangu yote ya utotoni na ujana, sauti ya mshawishi ilipendekeza sera ya kujitegemea na kufanya bidii ili kupata heshima. Dhana yangu ya mtu mzuri ilijengeka kupitia kwa hali yangu iliyoanguka ikiunganishwa na pendekezo la Shetani kwamba heshima ingepatikana kupitia kwa ukweli, unyofu na uaminifu. Utakumbuka kwamba nilitaja kwamba mshawishi angenipendekezea kufanya vitu ambavyo Mpendwa wangu alipenda hasa lakini kwa lengo tofauti.

Kwa vile sauti ya mshawishi ilikuwa kubwa kuliko ile ya Mpendwa wangu katika miaka hii ya ukuaji, wazo langu la mtu wa kuigiwa mfano lilikuwa yule ambaye alifanya haki na kuonyesha tabia nzuri kwa wengine. Onyesho hili la kuishi vizuri basi lingeteka upongezwaji kutoka kwa wengine na kunipa kukubalika katika kikundi changu cha jamii.

Sikufahamu hata kidogo kwamba mtu huyu wa kuigiwa mfano ambaye nilikuwa nimeingiza akilini, ambaye alikuwa katika uhalisia ni sanamu, bila kujua nilikuwa nimemuunganisha na mtu aitwaye Yesu. Niliona katika Yesu ambaye alionyesha tabia zote za mtu wa kuigiwa mfano, ambaye katika matendo ya ukarimu na matendo ya haki alijishindia pongezi na kuabudiwa na mamilioni. Kweli Yesu alikuwa mtu ambaye naweza iga, nakili na kutaka kuwa kama yeye. Tena, mshawishi alinishawishi kufanya vitu vyote vizuri kwa sababu zote mbaya.

Sehemu ngumu kabisa ilikuwa kwamba Yesu halisi wa Bibilia aliunganishwa pamoja na Yesu huyu wa uongo akilini mwangu, kiasi kwamba singewatenganisha.

> Hivyo tangu sasa hatumwangalii mtu ye yote kwa mtazamo wa kibinadamu, ingawa wakati fulani tulimwangalia Kristo kwa namna ya kibinadamu, hatumwangalii tena kwa jinsi hiyo. 2 Wakorintho 5:16.

Haikuniingia kwamba ningemfikiria Yesu kwa mtazamo wa ulimwengu. Kilichofanya uzoefu huu kuwa mgumu zaidi ni ukweli kwamba Ukristo ulikuwa katika miaka michache mia moja ya kuanza kwake umekamilisha

mtazamo wa Yesu kama ambaye alikuwa aheshimiwe kwa nguvu asili, uwezo na talanta.[2] Kwa namna sawa na ile nilikuwa nimejaribiwa kupokea mtu wa kuiga mfano kama yule ambaye anapata sifa kupitia kwa matendo mazuri, viongozi wa Kikristo pia walikuwa wamenyenyekeshwa kwa mchakato huu. Yesu huyu mpya alikuwa sehemu ya watu watatu, Mungu mmoja, Utatu. Utata wa watu watatu kuwepo ndani ya Mungu mmoja ulinisababisha kuacha juhudi za kuelewa hasa jinsi walivyo husiana. Nilihimizwa kukubali hili kama siri.

Ukisoma kwa makini maelezo ya Mungu kutoka kwa makanisa mengi ya Kikristo, utaona kwamba sababu ambayo Mungu anastahili kuabudiwa, kutukuzwa na huduma ni kuwa ana uwezo na anajua yote. Huyu alikuwa mungu wa utoto wangu! Nilipowaza kuhusu mungu huyu, kiasilika ilionekana sawa. Kile ambacho mtazamo huu uliniruhusu kufanya kilikuwa kuchukua mtu wangu wa kuigia mfano niliyemjua kama mtoto na kumuadhimisha kama Mungu wangu.

Kamwe haikutendeka kwangu kwamba mungu huyu ambaye niliahidi kutumikia hakika alikuwa onyesho lililofungwa la tamaa ya utoto wangu ya kuwa mtu mzuri, anaye stahili sifa, na heshima.

Kama nilivyotaja awali, kilichomfanya mungu huyu kuwa mgumu sana kumpambanua kuwa wa uongo ni kwamba nilikuwa nimeunganisha vipengele vya Yesu wa kweli wa Bibilia na mungu huyu. Ubatizo wangu miaka miwili baada ya kuamini kwangu ulionyesha kikamilifu unganiko hili la mawazo mawili kumhusu Mungu.

Kiapo changu cha ubatizo kiliuliza:

> Je, unaamini katika Baba, katika Mwanawe Yesu Kristo, na katika Roho Mtakatifu?

Lakini kauli ya Kanisa ilionyesha:

---

[2] Tazama "Athanasian creed" kwa mfano wa hili.

> Kuna Mungu mmoja: Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu, muungano wa watu watatu wa milele, wenye uwezo wote, wajuae yote, juu ya vyote, na waliopo daima. Asiye elezeka na aliye zaidi ya ufahamu wa mwanadamu….

Watu wengi watasoma kauli hizi mbili na wasione tofauti yoyote kabisa. Kama mtu mchanga, hakika sikuona tofauti yoyote. Ningeona istilahi Baba, Mwana na Roho Mtakatifu. Istilahi hizi zilijitokeza katika Bibilia na niliona ushahidi wa viumbe hawa watatu wakitenda kazi, hivyo basi nilichukulia kauli hii kuwa sahihi.

Kiapo cha ubatizo wangu kilionyesha tu imani katika viumbe watatu ambapo uhusiano kati ya Baba na Mwana ulionyeshwa tu kama *Wake*. Neno hili ndogo *wake* lilikuwa na tofauti chungu nzima. Neno *wake*, lilitoa maana halisi ya maneno Baba na Mwana. Yesu alikuwa Mwana *Wake*; mwana wa Baba. Jambo muhimu la kuangazia hapa lilikuwa kwamba kuvunjika kwa uhusiano kati ya Baba na Mwana *wake* ni kwamba kulivunja moyo wangu. Haya ndio maneno yaliyonigonga.

> Mwana wa Mungu asiyekuwa na doa alichukua juu yake mzigo wa dhambi. Yeye aliyekuwa na Mungu, alihisi moyoni mwake utengano wa kutisha ambao dhambi hufanya kati ya Mungu na mwanadamu. Hili lilitoa midomoni mwake kilio cha uchungu, "Mungu wangu, Mungu wangu, mbona umeniacha?" Mathayo 27:46 *Steps to Christ*, page 13.

Katika maneno haya nilipambanua kweli:

> Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu hata **akamtoa Mwanawe wa pekee**, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele. Yohana 3:16.
>
> Hivi ndivyo Mungu alivyoonyesha upendo Wake kwetu, kwa sababu Mungu alimtuma Mwanawe wa pekee ulimwenguni, ili tupate uzima kwa Yeye. (10) Huu ndio upendo, si kwamba tulimpenda Mungu, bali Yeye alitupenda, akamtuma Mwanawe, ili Yeye awe dhabihu ya kipatanisho kwa ajili ya dhambi zetu. 1 Yohana 4:9-10.

Katika miaka kumi na miwili iliyofuatia Ubatizo wangu, hakika sikuelewa kwamba asili ya uhusiano kati ya watu wawili waitwao Baba na Mwana walishikilia ufunguo wa kile kilibadilisha maisha yangu kikamilifu. Upendo wa Mungu ulidhihirishwa kwa kumtoa Mwanawe. Lilikuwa tendo la Mungu kumtoa Mwanawe, sio tu Mwana kujitoa, sio tu Mwana kuthibitisha uwezo wake, tabia ya kujikana nafsi, sio tu Yesu kutuonyesha matendo na kazi yake kuu. Baba alimtuma Mwanawe kudhihirisha tabia yake ya upendo kwetu, na kutupa Mwanawe tunaona onyesho la kuvutia zaidi, nzuri, tefu na ujasiri la moyo wa Mungu.

Kama nilivyoanza awali, sikutambua kwamba katika kukubali watu watatu ndani ya utatu wa Mungu mmoja, niliingizwa katika mkanganyiko kuhusu asili ya uhusiano kati ya Baba na Mwana. Tatizo hili lilifungamanishwa na pendekezo lingine kwamba kama nilimpenda Yesu kweli ningemuinua sawa kabisa kama Baba. Namna nilikuwa nimejifunza usawa kama mtoto ilikuwa kulinganisha kiasi. Ningehakikisha kwamba kiwango cha maji ya limau katika kikombe cha dada yangu sio zaidi ya kile kilichokuwa kwenye kikombe changu. Nililalamika kwa sauti na kwa muda mrefu kama dada yangu alipoke pipi au peremende tano nami nikapokea nne. Hivyo ndivyo nilivyojua vitu vilikuwa sawa. Hivyo ilipokuja kwa kuonyesha jinsi Baba na Mwana walikuwa sawa, mmoja angehakikisha kwamba wote walikuwa na sifa sawa hasa, uwezo sawa wa ndani, maarifa sawa, uwepo sawa wa milele. Kama mmoja alikuwa amepokea chochote kutoka kwa mwingine, ubora ungekuwa tofauti; ingekuwa kama mmoja kuwa na maji ya limau 100% na mwingine kuwa na maji ya limau 50% na 50% maji.

Aina hii ya kufikiria ilikuwa ikichukua pahali pa kina na pa siri katika akili zangu; ilikuwa asili, asilika, na kwa hivyo inavyooneka yenye mantiki. Sikuwa na wazo lolote kwamba kumfikiria Mungu kwa namna hii hakika kuliiba maana ya maneno *Baba* na *Mwana* na uhusiano wao kwa kila mmoja.

Nilipotazama Uwana wa Yesu kutoka kwenye Bibilia, nilimwona mtu aliyemwamini Baba yake kikamilifu na alidumu kikamilifu katika mapenzi yake. Niliona jinsi angelala kwenye chombo katikati ya mawimbi; angekabiliana kwa utulivu na umati wenye hasira uliotaka kifo chake;

angesubiri kwa siku 40 bila chakula akiamini Babake atampa mahitaji yake katika utimilifu wa wakati. Matendo haya ya uaminifu na utiifu yalipowekwa juu ya mtazamo wa Yesu kama Mtu wa Pili wa Uungu, akiwa na uwezo sawa kwa njia sawa na Baba, akili zangu zilikanganyika. Mtu huyu hakuwa na shukurani yoyote kwa Baba kwa uwezo aliokuwa nao, badala yake alisimama bega kwa bega na mtu anayeitwa "Baba,"nguvu kwa nguvu, maarifa kwa maarifa, miaka kwa miaka, walikuwa sawa. Kupendeza sawa, bila shaka, ila walikuwa sawa. Janga kuu kwangu ni kwamba katika kujua usawa huo kulikuwa na kipengele cha babuzi kilichofuta maana ya maneno *Baba* na *Mwana* ambayo kwa upande wake uliotesha kutu maana yangu binafsi ya uwana. Kama Yesu hakuwa Mwana wa kweli wa Mungu katika Nyanja yake basi wala mimi sikuwa katika yangu. Namna gani hivyo? Kwa kutazama tunabadilishwa. Kama nilikuwa na tashwishi ya Yesu kuwa Mwana wa Mungu kweli na kwamba alikubalika kwa nafasi yake badala ya Uwana wake msafi, basi nilikuwa wazi kwa kushuku uwana wangu na kuanza kutafuta kukubalika kwa nafasi yangu na juhudi zangu kwa kanisa langu.

Hivyo nilimwabudu Yesu wa dunia ambaye alikuwa mtiifu, mwaminifu na kuheshimu na nilimuunganisha huyu na mtazamo wa Yesu aliye mbinguni ambaye alijitegemea, mwenye uwezo wake mwenyewe bila urithi wowote kutoka kwa Baba. "Yesu huyu wa mbinguni" alinifanya nitafute kuiga matendo ya Yesu wa duniani kwa kunakili na kuiga utegemezi wake wa kimbingu. Bila kutambua, hali yangu ya kidunia kimfano nilimuinua Yesu sanamu katika Patakatifu pa mbinguni, nikisukumwa na tamaa sawa ya kidunia iliyomsukuma Pembe Ndogo dhidi ya Kristo wa kweli mbinguni.

Wacha nikupe baadhi ya mifano ya jinsi hili lilitenda kazi katika maisha halisi. Mara nyingi wakati ningeketi na kusikiliza mahubiri, Mpendwa wangu angenifanya kupokea maneno haya kwa moyo. Kwa wakati uo huo mshawishi alikuwa anajaribu kumlenga mhubiri vile alikuwa akihubiri vizuri. Kama mhubiri yaliwasilishwa vizuri, nilianza kuota kuhusu kuwasilisha mada hii mbele ya hadhira na kufikiria mwitikio wao. Kama mhubiri aliwasilisha vibaya, mshawishi anginipendekezea kwamba ningefanya kazi bora. Wakati ningehubiri na watu kuguzwa na kweli,

Mpendwa wangu alinihimiza kufurahia, lakini mshawishi alinihimiza kuvuta sifa kutoka kwa watu mlangoni walipotoka hekaluni.

Nilipoketi katika mafundisho ya Bibilia, Mpendwa wangu angetafuta kuathiri maneno ya Maandiko juu ya moyo wangu ila mshawishi aliniathiri kuhakikisha kwamba nilijua kunukuu mafungu vizuri na kunukuu mafungu kadha kuonyesha uwezo wangu juu ya mada. Nilipokuwa katika mviringo wa maombi, mpendwa wangu alinihimiza kufurahia kwa fadhila ya fursa ya kumfikia Baba kupitia kwake, mshawishi alinisukuma na mawazo kwamba mtu huyu aliye kando yangu huomba kwa muda mrefu zaidi na hakika hana kitu cha maana cha kusema. Dhamiri zangu basi zingepigwa wakati huo na ningekuwa na vita hivi vidogo akilini mwangu kati ya pande hizi mbili na kupoteza mwelekeo kikamilifu wa kile kilichoombwa na walionizunguka.

Nilisoma kumhusu Yesu na kuomba usiku mzima na badala ya kulenga jinsi lazima alikuwa amempenda Baba yake, niliwaza zaidi kuhusu ukweli kwamba hakika alitumia usiku wote katika maombi, na nilikaribisha wazo la kushiriki biashara hii, lakini wakati huu Mpendwa wangu angeniambia kuwa hili ni kosa. Kama nilivyosema, mgogoro huu wa mawazo uliendelea kwa zaaidi ya muongo mmoja. Mkombozi wangu aliponidhihirishia umuhimu wa lishe na masuala ya mtindo wa maisha, mshawishi alinivuta katika kuzingatia mtindo mzuri wa lishe, mavazi, na burudani. Ishara ya kuelezea hadithi ya kwamba nilikuwa naitikia sauti ambayo sio sahihi ilinijia nilipokosoa wengine kwa tabia zisizofaa. Tabia sahihi za Mkristo zikawa mzizi badala ya tunda la uzoefu wangu. Ilikuja kwa sababu mungu wa utoto wangu aliadhimishwa moyoni mwangu kama Mungu wa ulimwengu.

Mgogoro wa kila siku ndani yangu ulileta huzuni nyingi moyoni mwangu. Yesu huyu aliyefanya matendo haya yote mazuri alianza kuenda mbali na mbali zaidi kutoka kwa ufahamu wangu. Furaha ya upendo wangu wa kwanza ilikuwa imechukuliwa. Nilimtafuta Mpendwa wangu bure, lakini sikufanikiwa kumpata. Moyo wangu ulijawa na shughuli za kanisa, na masomo kwa kiasi kwamba nilikuwa na muda mchache wa kuakisi na kushiriki na Mkombozi wangu. Hata nilipokuwa na wakati, nilihisi

msukumo huu wa kuingia katika siku na kufanya matendo ambayo Yesu alitenda na kuwa mtu wa msaada na kujali aliye kuwa. Hakuna aliyejali sana kama nilitumia saa nyingi kuzungumza na kushiriki na Yesu pekee, isipokuwa, bila shaka nipate hadhira ambayo itatamani utengo kama huo.

Kulikuwa na mgogoro wa mara kwa mara katika kutaka kwangu kuwa Mkristo mzuri ambaye anampenda Mungu, Neno lake na walionizunguka ikipingana na kutaka kwangu sifa kwa kufanya mambo hayo. Nilijua kwamba kutaka sifa binafsi si sawa, lakini nilifikiria kwamba hii ilikuwa sehemu ya uzoefu wa Mkristo ukipigana dhidi ya mwili. Nilijaribu kufuta maoni ya kusifiwa baada ya kuhubiri, lakini nilihisi ni jambo la kawaida kwamba nilikuwa nikijilenga niliposema "Usinishukuru mimi, mshukuru Bwana." Sikufaa kufanya "mimi" kuwa lengo. Ningesema tu, "Mshukuru Bwana," lakini "usinishukuru mimi ilitoka kwa tamaa ya siri ya kutaka kushukuriwa na kuthaminiwa kwa kufanya kazi nzuri.

Mara nilipokuwa mhudumu wa Kiadventista, nilikuwa nimewekwa katika nafasi ya manufaa ambayo sikuwa nimeiona awali. Nilianza kuwaangalia wahudumu, nilikuwa nikitaka nafasi hiyo; niliona ushindani mwingi wa ndani na binafsi niliokuwa nao ulionyeshwa wazi katika baadhi ya wahudumu walionizunguka. Kwa vile ushindani wangu ulionekana ndani kwangu ningeonyesha kushangazwa na tabia za wahudumu hawa waliokuwa wakipotosha kundi.


Baada ya kipindi cha wakati katika huduma, nikiona michezo ya nguvu na mikakati iliyowekwa katika siasa za kanisa. Nadhani nilikuwa kinyume kidogo, huu ndio wakati mshawishi alinihimiza kuchukua njia nyingine wakati kupendeza watawala kulipoteza mvuto. Nilianza kujiingiza katika filamu za uwezekano (documentary films), michezo na burudani ya muachano tena. Nilijiambia kwamba sikutaka kuwa Mfarisayo, nilihitaji kupumzika na kujiburudisha. Hakika nilihitaji kupumzika na kujiburudisha lakini sio kupitia kwa michezo. Walithibitisha zaidi tu imani kwamba kufanya matendo na mafanikio ni njia ya kukubalika, sifa njema na heshima.

Ni katika hali hii ya mawazo ndio nilisita katika Njia ya Maisha. Singesonga mbele kwa sababu dhana yangu ya Mungu ilikuwa imekanganyika na ibada ya sanamu ya utoto wangu. Ibada hii ya sanamu ilimruhusu mshawishi kupendekeza vitu kwangu, mara nyingi bila mimi kutambua mahali vilikuwa vikitoka na mbona vilikuwa vikitendeka. Matokeo ya kukata tamaa kwangu yalinifanya kulala katika mlima uitwao *ugumu*, na kulegeza kitabu ambacho niliagizwa kuweka karibu na kifua changu kama inavyoelezewa na John Bunyan katika Mchakato wa Safari (*Pilgrim's Progress)*.

> Nikasema, Haya, niondoke nizunguke mjini, Katika njia zake na viwanjani, Nimtafute mpendwa wa nafsi yangu. Nikamtafuta, nisimpate. (3) Walinzi wazungukao mjini waliniona; Je! Mmemwona mpendwa wa nafsi yangu? Wimbo Ulio Bora Song of Solomon 3:2-3.

# Sehemu 2. Uchumba

## 8. Pazia ya Kwanza



Mshawishi alikuwa amenidanganya kupitia kwa sura iliyokanganywa ya Mpendwa wangu. Muungano wa Kristo unaodhihirishwa kwa watu kwa mwili wake uliunganishwa pamoja[3] na “mtu wa pili wa Uungu” aliyekuwa na nguvu, uwezo na heshima kutoka kwa chanzo chake mwenyewe. Mtu huyu aliwasilishwa kwangu akiwa sawa kwa sababu ya uwezo wake badala ya urithi wake kama Mwana. Hakuna katika haya lililokuwa dhahiri kwangu; nilihishi tu matokeo ya utabiri wa imani kama hiyo.

Nilitaja, nilitamaushwa zaidi na matukio kadha yaliyohusisha wahubiri wenzangu. Niliona mapendeleo, mambo yakifanyiwa kichini chini na ujanja wa kisiasa katika mikutano ya kanisa.

Kwa kupoteza ukaribu na Mpendwa wangu, dhambi haikuonekana kuwa kubwa sana, dhamiri yangu haikuwa tefu, na kujihurumia kulimruhusu mshawishi kushikilia kwa uthabiti moyo wangu. Kujiingiza kwa mambo madogo kukakua mambo makubwa. Kama kiongozi wa dini, mambo ya nje yalikuwa yamedumishwa kwa makini, lakini katika wakati wangu binafsi, sikujali juu ya lugha na vurugu ya senema nilizotazama. Nilivutiwa zaidi na michezo ambapo heshima kwa mafanikio ilionyeshwa mara kwa mara mbele yangu.

[3] Hii ilikuwa kuandika kwangu upya bila kujua kile ambacho Roma ilikuwa imefanya zamani za kale katika mafundisho ya hypostatic union yaliyofanywa rasmi katika baraza la Chalcedon la 451 A.D. ni kuchomelea pamoja lahaja za vinyume viwili. Roma ilihitaji mafundisho haya ili kukabiliana na ukweli kwamba Mungu mwenye uwezo wa kuwepo hawezi kufa. Nilitamani umbo ghafi la fundisho hili kuchomelea pamoja Yesu wa duniani wa kutii kwa uaminifu na Yesu wa mbinguni wa kujitegemea na mwenye uhakika.

Katika hali hii ya mawazo, nilivuka mstari binafsi ambao nilifikiria haukubaliki. Hakikuwa kitu chochote kutoka nje na kilikuwa tu moyoni mwangu, lakini kulingana na sheria ya Mungu, nilihisi kuhukumiwa. Hili lilinileta katika hatua muhimu katika maisha yangu. Kwa msingi wa kanuni ya sifa njema na heshima kwa bidii, uadilifu na nidhamu, nilihisi kwamba nilikuwa nimeshindwa. Chaguo tu ambalo awali niliona lilikuwa kuyaacha yote nyuma na kusahau kuhusu kudai kuwa mkristo kwa kiwango cha juu kama hicho. Kama kile ambacho nilikuwa nikihubiri hakikuwa halisi katika maisha yangu basi nafaa kuacha kuhubiri. Bibilia inaahidi ushindi juu ya dhambi kwa wale ambao wanamfuata Kristo kwa imani katika Patakatifu pa Patakatifu. Sikuwa nashuhudia ushindi huu. Nilijua kwamba Mungu husamehe wenye dhambi, lakini pia huahidi ushindi katika maisha.

Uwezekano wowote wa kuwa na uzoefu wa Patakatifu pa Patakatifu ulifanywa kutowezekana kwa sababu ya mawazo yaliyogawanyika kuwili kuhusu Yesu kweli alikuwa nani. Sikuwa hata nimepata uzoefu wa Patakatifu kwa sababu ya dhana zangu zilizokanganyika. Tutashughulikia hili kwa undani kabisa baadaye, lakini inatosha kusema kwamba niliibiwa uwezo wa kuwa na uthabiti, ibada tamu na Yesu kwa sababu bila kujua nilikumbatia mawazo ya kutatanisha kuhusu Uwana wake. Sikujua hata kwamba mawazo yalikuwa tatanishi. Nilipata tu uzoefu wa utata akilini mwangu kwa kukabiliana na maisha yangu siku baada ya siku.

Nilipohisi uzito wa sheria juu yangu na nilipotafakari matarajio yangu, nilitambua kwamba kupitia kwa kuabudu miungu ya mawazo yangu na mawazo yangu ya sasa ya roho za baba wa kale ambayo:

> ...ile amri iliyokusudiwa kuleta uzima, ilileta mauti. (11) Kwa maana dhambi kwa kupata nafasi katika amri, ilinidanganya na kwa kupitia hiyo amri, ikaniua. Warumi 7:10-11.

Amri iliyoteuliwa kwa uzima, niliipata kuwa kwa mauti kwa sababu ya tamaa yangu ya dhambi ya kutambuliwa kwa mafanikio yangu na kuadhimisha mungu kama huyo moyoni mwangu. Nilihisi kuwa na hatia mbele za Mungu. Nilipofikiria kuhusu hatia, kiasilia niliwaza kuhusu Baba, kwa sababu baba yangu wa duniani alikuwa wakala wa Mungu wa kunifunza nidhamu. Hivyo wakati nilikabiliana na dhambi zangu, ni Baba

wa mbinguni ningekabiliana naye. Angenisamehe aje? Kulingana na sheria ya watu wa kuheshimiwa, nilihisi nisiyestahili msamaha. Pia nilihisi kutostahili kwa sababu sehemu yangu ilikuwa imekatishwa tamaa kiasi kwamba singeendelea na safari ya kujishindia kukuzwa na sifa kwa huduma yangu kwa Mungu.

Nilipokuwa nikipigana na kuomba, Mpendwa wangu alinijia na kunikumbusha kwamba Baba ananipenda. Kama nikichagua kushikilia kafara yake ya dhambi zangu, basi kwa kweli nilikuwa nimesemehewa kweli.

Nilipochungua kupitia kwa ukungu wa mchanganyiko, nilikua nikitafuta uhakika wa upendo wa Baba. Neno la Mungu lilisema, “Amini!” ingawa kulikuwa na jiwe lililokuwa kikwazo katika njia yangu. Baba wa Bibilia wa Yesu alikuwa na uhusiano wa karibu na maisha yangu, ila Baba wa utatu alikuwa mbali kiasi kwa sababu Yesu alifanya kazi yote halisi. Baba kweli aliketi tu kwenye kiti cha enzi na kuidhinisha na kutabasamu kwa kazi ya Mwanawe. Sikujua vitu hivi kimantiki wakati huo, lakini akilini mwangu hicho ndicho kiliweka mwanya kati yangu na Baba. Anaweza nisamehe kweli?

Neno liliniambia, “Mbona usishikilie kwa nguvu, Adrian?” bado nilijitahidi. Na kisha Neno likanijia:

> Kwa hiyo tunamsifu Mungu kwa huruma zake kuu alizotumiminia kwa sababu sisi ni wa Mwanae Mpendwa. Waefeso 1:6.
>
> Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu hata akamtoa Mwanawe wa pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele. Yohana 3:16.
>
> Kwa sababu ninyi ni watoto wa Mungu, Mungu amemtuma Roho wa Mwanawe mioyoni mwenu, anayelia, Abbaa! Yaani, Baba. Wagalatia 4:6.

Tena nilikumbushwa kwamba kutengwa kwa Baba kutoka kwa Mwanawe ndicho kile kilidhihirisha hisia ya Baba kwetu. Kwa kuona tu kuwa Mungu alikuwa Baba ya Yesu ningeweza anza kuthamini upendo wake kwangu. Kama Yesu kwa kweli hakuwa Mwana wa Mungu basi Mungu hakuwa

akipeana kitu kilichokuwa chake; alikuwa akimtazama "Mwana" akifuata imani yake. Tunaweza sema kwamba Baba alikuwa akipeana uhusiano wake na Mwana, lakini haukuwa uhusiano aliokuwa nao, hivyo hili halikutafsiri niliposoma "kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu." Ninaposoma *Mungu* katika sentensi, kwa kiasi niliwaza kuhusu wahusika watatu wa Uungu wakiamua kwamba Yesu lazima aje na kwa wakati uo huo Mungu alimtuma. Mkanganyiko huu uliweka neema ya Mungu na msamaha katika urefu wa mikono. Nilisimama kama msafiri aliyechoka katika *mwendo wa safari (pilgrim's Progress)* baada tu ya simba wawili njiani mwake. Ningeona usalama wa makao zaidi, lakini kwanza jaribio la imani.

Katika wakati wa mgogoro, nilimfikia Baba yangu wa kweli na kuchagua kuamini alinisamehe. Furaha ilijaa nafsini mwangu niliposhikila uhakika kwamba nilikuwa nimekubalika katika Mpendwa. Kwa kweli alikuwa Mpendwa wangu.

> Kitambo kidogo tu nikiisha kuwaondokea, Nikamwona mpendwa wa nafsi yangu; Nikamshika, nisimwache tena, Hata nilipomleta nyumbani mwa mamangu, Chumbani mwake aliyenizaa. (5) Nawasihi, enyi binti za Yerusalemu, Kwa paa na kwa ayala wa porini, Msiyachochee mapenzi, wala kuyaamsha, Hata yatakapoona vema yenyewe. (6) Ni nani huyu apandaye kutoka nyikani, Mfano wake ni nguzo za moshi; Afukizwa manemane na ubani, Na mavumbi ya manukato yote ya mchuuzi? Wimbo Ulio Bora 3:4-6.

Furaha yote ya upendo wangu wa kwanza ilirejea. Tena upendo wa Kristo ulitia manukato kila pumziko la nafsi yangu. Nilikuwa nimesamehewa, nimesamehewa mara mbili; kwanza kwa dhambi za utotoni mwangu na ujana wangu na sasa tena kwa ibada ya sanamu katika mwanzo wa maisha ya utu uzima.

Muda mfupi baada ya matukio haya, Baba yetu alihakikisha kwamba nimepata wakati wa kusoma kwa kina kumhusu Mwanawe na kuanza kufahamu mbona nilikuwa nimepotea kwa miaka mingi katika hali ya mkanganyiko. Niligonjeka sana na nikakomesha kazi yangu kama

mhudumu. Tulihamia mahali ambapo ningekuwa na wakati wa kupona, kusoma na kuomba.

Katika wakati wangu wa kupata ahueni, nilikumbuka mazungumzo marefu niliyokuwa nayo miaka saba iliyopita. Mmoja wa rafiki zangu alijaribu kunielezea kwamba kulikuwa na matatizo katika Utatu na kwamba fundisho hili kamwe halijakuwa sehemu ya kanisa. Nilishangazwa. Sikujua chochote kuhusiana na hili. Maana ambayo hili lilikuwa nayo kwa kanisa ilikuwa kubwa sana kwa akili yangu kukubali. La kuhuzunisha, niligeuka kutoka kwa suala hilo na kuchagua kauli kadha teule ambazo zilionekana kuunga mkono imani yangu. Hakuna chochote ambacho kingemfanya Mpendwa wangu kuonekana mdogo kwa vyovyote vile kuliko anavyostahili. Singeruhusu mtu yeyote apunguze uungu wa Yesu. Mimi, pamoja na marafiki wengine, tulimwona mtu huyu kama aliyegeuzwa na kupotoka kutoka kwa kazi ya kweli ya kuokoa mioyo. Hili lilisikika kama hoja kamili kwangu kuweza kuonyesha uaminifu wangu kwa Mungu.

Sasa baada ya miaka saba, nilienda kwa rafiki yangu na kuomba msamaha kwa kutokuwa mwanafunzi wa Bibilia wa Berea na kuthibitisha mambo yote. Alinisamehe kwa ukarimu, na kisha nikaagiza vifaa kadha vya kusoma kuhusu suala hili. Niliposoma, nilijihisi nikivutwa kwa tamka wazi la Maandiko.

> Kama vile Baba alivyo na uzima ndani Yake, vivyo hivyo amempa Mwana kuwa na uzima ndani Yake. Yohana 5:26.
>
> Nao uzima wa milele ndio huu, wakujue Wewe uliye Mungu wa pekee, wa kweli na Yesu Kristo uliyemtuma. Yohana 17:3.
>
> Mwanzo wa Injili ya Yesu Kristo, Mwana wa Mungu; Marko 1:1.
>
> Simoni Petro akamjibu, “Wewe ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai.’’ Mathayo 16:16.
>
> Zamani Mungu alisema na baba zetu kwa njia ya manabii mara nyingi na kwa njia mbalimbali, (2) lakini katika siku hizi za mwisho amesema nasi kwa njia ya Mwanawe, ambaye amemweka kuwa mrithi wa vitu vyote, ambaye kwa Yeye aliuumba ulimwengu. (3) Mwana ni mng’ao wa utukufu wa Mungu na mfano halisi wa nafsi

> Yake, akivihifadhi vitu vyote kwa neno Lake lenye uweza. Akiisha kufanya utakaso kwa ajili ya dhambi aliketi mkono wa kuume wa Ukuu huko mbinguni. (4) Kwa hiyo alifanyika bora kuliko malaika kama Jina alilorithi lilivyo bora kuliko lao. Waebrania 1:1-4.

Mpendwa wangu alininenea kupitia kwa maneno haya. Niliposoma Bibilia tu, ilionekana kuashiria kwamba kweli Yesu alikuwa Mwana wa Mungu. Nilianza kujivuna katika furaha ya mawazo haya mshawishi aliposema kimya kimya, "Yesu anawezaje kuwa sawa na Baba na bado azaliwe katika mahali fulani? Adrian, hili linapunguza uungu wa Kristo. Uko na uhakika kwamba unataka kunyoosha kila kitu kwa kitu ambacho hauna hakika kabisa kukihusu?"

Nilimtumia barua pepe msomi wa kuheshimiwa kuhusiana na masuala haya na alinipa hoja zilizooneka kuwezekana. Hili likiunganika na hamu yangu ya kumuona Yesu akiwa na uungu kamili na kuwa sawa na Baba lilinifanya kurudi nyuma kutoka kwa kukumbatia kikamilifu ukweli kwamba Yesu alikuwa Mwana wa Mungu. Ingawa nilikuwa nimesoma Maandiko ya kutosha kujua kwamba kulikuwa na pande mbili za kisa. Niliamua kuwa wazi kwa suala hili, lakini la kuhuzunisha nilijishikilia kwa Utatu.

Ningependa kukwambia kwamba hofu ya kuwapoteza rafiki wengi na msimamo wangu kanisani haikuathiri uamuzi wangu, lakini siwezi sema hilo. Baadhi ya rafiki zangu walikuwa wameondolewa kanisani kwa kukataa Utatu, na kwa kweli sikutaka kujiingiza katika hali za namna hiyo. Nilikubali majadiliano dhidi ya Uwana halisi kutokana na usomi niliokuwa nimezua bila kuupa maanani barabara. Msomi rafiki yagu alikuwa amependekeza kwamba kama kazi ya usoni ya Kristo ajae ingetumiwa katika kutarajia, kichwa *Mwana* pia kinaweza tumika kwa njia hii. Ndio, Istilahi K*risto* ilikuwa kichwa au ofisi ya kazi ya Kristo kwa sababu kweli alikuwa mwana-kondoo aliyechinjwa kutoka kuwekwa msingi wa ulimwengu na hiyo ilikuwa ahadi ya kile ambacho angekuja kufanya. Istilahi *Kristo* ilikuwa ofisi ya Mwana wa Mungu na kwa hivyo ingetumika kwa matarajio. Hata hivyo, istilahi *Mwana* haikuwa ofisi bali yule aliye kuwa kwa uhusiano na Baba. Hoja ya rafiki yangu ilikuwa imegeuza neno

*Mwana* kutoka kwa *kiumbe* hadi kwa *ofisi*. Tofauti ni gani? Ni tofauti ya yule uliye na kile ambacho unafanya. Ni kujulikana katika muktadha wa mahusiano badala ya muktadha wa kazi. Tofauti ni muhimu? Nilipogundua baadaye, ilikuwa tofauti kati ya kumwabudu Mungu badala ya Shetani.

Moyo wangu sasa ulikuwa wazi zaidi kwa masuala mengi kuhusiana na Mpendwa wangu. Ingawa bado nilikuwa nikisita kati ya maoni mawili. Moyo wangu sasa uliegemea upande wa ukweli kwamba kweli Yesu alikuwa Mwana wa Mungu, lakini kuna mambo ambayo singetatua.

> Yesu akawaambia, "Ninyi ni wajinga kiasi gani, nanyi ni wazito mioyoni mwenu kuamini mambo yote yaliyonenwa na manabii! Luka 24:25.

Baba yangu mwenye upendo alinihurumia. Alijua nilihitaji nguvu zaidi, dawa ya macho na kuombewa kutoka kwa Mpendwa wangu ili kuandaliwa kukabiliana na kweli yote. Vitu hivi vyote vingepatikana Patakatifu. Mkate wa mbinguni, nuru ya ulimwengu na ukuhani wa Kristo katika madhabahu kwa ajili yangu, kungezaa majibu niliyohitaji ili kuweza kufikiria kumkumbatia kikamilifu mpendwa wangu.

# 9. Nuru ya Ulimwengu



Neno lako ni taa ya miguu yangu, Na mwanga wa njia yangu. Zaburi 119:105.

Ndani Yake ndimo ulimokuwa uzima na huo uzima ulikuwa nuru ya watu. Yohana 1:4.

Kisha Yesu akasema nao tena akawaambia, Mimi ni nuru ya ulimwengu. Mtu ye yote akinifuata hatatembea gizani kamwe, bali atakuwa na nuru ya uzima. Yohana 8:12.

Akili zangu zilipofunguka kwa uhalisia kwamba Yesu kweli ni Mwana, mafungu kadha ya Maandiko gafla yalifurika kwa nuru. Kwa vile Kristo ni jiwe la pembeni, mitazamo yetu yote ya kweli inaunganishwa na jinsi tunamjua. Kama "Mtu wa pili wa Utatu," mtazamo wangu wa "Mwana" ulikuwa wa yule ambaye alifanya mambo makuu kutoka kwa mali yake mwenyewe. Kama Mwana wa Baba, nilianza kumuona Mwana kama ambaye hupokea vitu vyote, ambaye hupokea mibaraka na anapendwa kwa vile alivyo wala sio kwa kile anachokitenda. Mtazamo huu haukuwa dhahiri kwangu lakini ulidhihirishwa kwa njia ambayo nilisoma Andiko na kuhusiano na waliokuwa karibu nami.

Hata ingawa sikuwa na majibu yote kuhusu Utatu, ukweli kuhusu Uwana ulibadilisha jiwe la pembeni la imani yangu, na jiwe hili la pembeni jipya na lenye thamani lilianza kuleta kuamini kwangu katika laini moja nalo. Mambo ya Shaba katika kufikiria kwangu sasa yalikuwa yanaanza kuondolewa nilipotoka kwenye ua na kuingia Patakatifu pa Patakatifu.

Ndipo nikapewa mwanzi wa kupimia ulio kama fimbo, nikaambiwa, "Nenda ukapime Hekalu la Mungu pamoja na madhabahu, nawe uwahesabu wale waabuduo humo. (2) **Lakini usiupime ua wa nje wa Hekalu, uache, kwa sababu ua huo wamepewa watu Mataifa**…. Ufunuo 11:1-2

Maneno ya Bwana ni maneno safi, Ni fedha iliyojaribiwa kalibuni juu ya nchi; Iliyosafishwa mara saba. Zaburi 12:6

> Neno linenwalo wakati wa kufaa, Ni kama machungwa katika vyano vya fedha. Methali 25:11

Mungu ambaye nilikuwa nimeadhimisha tangu utotoni mwangu alikuwa anakumbwa na changamoto kuu. Ingawa bado nilikuwa nikimjua Yesu kama mwenye uwezo wote kutoka kwenye rasilimali yake mwenyewe, dhana ya kuwa Mwana wa kweli iliniruhusu kunakili kanuni hii katika maisha yangu. Nilianza kuiga yule ambaye hupokea, yule ambaye amebarikiwa na Baba yake na nikaanza kubadilisha kila kitu.

Sabbato moja nilipokuwa nikitembea katika mazingira ya kijijini karibu na nyumbani mwangu, niliwaza kuhusu kuzaliwa kwa mwanangu. Niliporejelea kipindi cha kuzaliwa kwake, nilikumbuka fikira zilizokuwa moyoni mwangu. Nilipo mtazama mwanangu, nilikuwa nimeomba "Bwana, usiruhusu chochote kije kati yangu na mwanangu, na ninaomba kwamba aje kunijua jinsi nilivyo." Sasa kwa vile nilikuwa nimefunguka kumuona Yesu kama Mwana kweli, nilikuwa tayari kusikia jibu hili wazi ambalo lilinijia kutoka kwa Baba yangu wa mbinguni nilipokuwa nikitembea siku hiyo ya Sabbato tulivu.

"Hivyo ndivyo ninavyohisi kukuhusu"

Niliduwaa. Badiliko langu katika ufahamu wa Yesu alikuwa nani, uliniruhusu kujua nguvu za kweli za kauli hii. Mungu alikuwa akisema kwangu kwamba hakutaka chochote kije kati yangu naye, na alitaka tu nimjue jinsi alivyo. Sasa kwa vile nilijua Yesu alikuwa Mwana, ningemuiga kweli na kuamini kwamba pia mimi nilikuwa mwana katika nyanja yangu. Uwana wa Yesu kwa Baba ulifanya hakika uwana wangu kwa Baba. Ni kupitia tu kwa Mwana wa Mungu ningeweza kuelewa hili.

> …Ninapaa kwenda kwa Baba yangu ambaye ni Baba yenu, kwa Mungu wangu ambaye ni Mungu wenu. Yohana 20:17

> Kwa hiyo tunamsifu Mungu kwa huruma zake kuu alizotumiminia kwa sababu sisi ni wa Mwanae Mpendwa. Waefeso 1:6

Licha ya ufahamu huu mpya, nilipojua kile ambacho Baba yetu wa mbinguni alikuwa akisema kwangu, nilihisi wimbi la upinzani likiiosha nafsi

yangu. Mshawishi alinikumbusha kushindwa kwangu na sababu ambazo sikufaa uwana. Vita hivi vilijirudia katika akili zangu kama nilidai cheo cha uana na kwamba Mwenyezi Mungu wa mbingu na dunia alitaka tuwe karibu bila chochote kati yetu. Ilionekana kama ndoto ngumu zaidi kuiamini. Baba yangu wa Mbinguni kwa upole alininenea, "Kweli utakataa pendekezo langu?"

"Nini ambacho nakifanya?" nilijiambia. "Hapana Bwana, nachagua kuamini kwamba unanipenda kama mwana. Hakika silielewi hilo, lakini ninaamini."

Uwana wa Yesu ukawa jiwe la msingi wa uwana wangu. Kwa kutazama Uwana wake naweza dai wangu. Nuru iliyokuwa katika Mwana wa pekee ikafurika nafsini mwangu. Yote haya yalikuwa yakitendeka ndani yangu bila mimi kuelewa jinsi haya yalihusiana na Utatu. Ulikuwa mchakato taratibu wa kujenga juu ya jiwe jipya la pembeni.

Maana yangu mpya ya uana ilinisababishia kuwa na utambuzi mkuu wa utegemezi wangu kwa Baba Yangu. Siku moja nilipokuwa nikisoma:

> Nyoka akamwambia mwanamke, Hakika hamtakufa, (5) kwa maana Mungu anajua ya kwamba siku mtakayokula matunda ya mti huo, mtafumbuliwa macho, nanyi mtakuwa kama Mungu, mkijua mema na mabaya. Mwanzo 3:4-5.

Ghafla lilinigonga kilichokuwa katika uongo huu kilikuwa kanuni ya kujitegemea na uhuru. Mfululizo wa haraka wa nuru iliangaza katika mawazo yangu kwamba uhuru humaanisha kupoteza baraka ambayo humaanisha kupoteza thamani na karama. Mawazo haya ndiyo yalikuwa mwanzo wa mfululizo wa *Vita vya Utambulisho* ambao niliwasilisha muda mfupi baadaye. Kisha hili lilifuatwa na kitabu *Vita vya Utambulisho*.[4] Ingawa sikutambua jinsi mabadiliko haya katika kuwaza yalikuwa yakitendeka, hata hivyo mabadiliko katika kumuelewa Yesu kama Mwana wa kweli yalipelekea kwa msingi wa urithi, ambao ulielekeza kwa kanuni

[4]. Tazama www.identitywars.org

ya kubarikiwa, ambayo ilipelekea ufahamu wa *thamani kwa mahusiano kinyume na thamani kwa mafanikio*.

Nakumbuka mara ya kwanza iliponigonga kwamba Shetani kwa kweli alihisi kutofaa kwa sababu ya uongo huu wa kijitegemea. Kama kila kitu tulichonacho hutoka kwa Mungu basi tutashuhudia furaha tu, fahari na amani tunapotambua yule ambaye alitupa. Mwana wa Mungu anaishi na kupumua hili kikamilifu. Hafanyi lolote lake Mwenyewe, lakini anamtambua Baba kama chanzo kikuu cha vyote. Ila shetani alikataa kutambua kwamba vyote alivyonavyo vilitoka kwa Mungu kupitia Kristo. Hili lilimvua baraka za Baba na hatimaye likamfanya mwanzilishi wa kukosa thamani. Kisha ningeona kwamba mbegu hii ya kukosa thamani ilikuwa imeshikamanishwa katika uongo uliopatiwa Adamu na Hawa katika bustani. Kukosa thamani kulikuwa kumefichwa katika uongo wa kujitegemea.

> Enyi wanadamu, hata lini utukufu wangu utafedheheka? Je! Mtapenda ubatili na kutafuta uongo? Zaburi 4:2

Kuunganisha uongo wa Shetani wa kupata thamani kwa mafanikio kulirarua pande za udanganyifu ambazo mshawishi alikuwa ameweka vitendoni juu yangu. Hitaji la kuthaminiwa kwa juhudi zangu kanisani, hitaji la kuwa na kazi kila wakati, kuhakiki wengine kwa kutofanikiwa kwao vyote vilianza kuwekwa wazi kwa nuru kwamba thamani haiji kutoka kwa kile tunachofanikisha bali kwa yule tuliyewake.

Kutoka kwa uongo uo huo wa nyoka, nilianza kuona kwa uwazi zaidi kwamba uzima hupokelewa kutoka juu. Awali nilikuwa nimeamini kwamba hii ni nadharia, lakini vile jiwe la pembeni la imani yangu lilikuwa limefahamika kama mtu wa kujitegemea kikamilifu, mwazo yangu yalikuwa yamekanganyika. Kisha nilipigwa na mafungu haya ya Bibilia:

> Mungu aliyeumba dunia na vyote vilivyomo ndani yake, Yeye ndiye Bwana wa mbingu na nchi, hakai katika mahekalu yaliyojengwa kwa mikono ya wanadamu. (25) Wala hatumikiwi na mikono ya wanadamu kana kwamba anahitaji cho chote, kwa sababu Yeye

> mwenyewe ndiye awapaye watu wote uhai na pumzi na vitu vyote. Matendo 17:24-25.
>
> Yeye ni mfano wa Mungu asiyeonekana, mzaliwa wa kwanza wa viumbe vyote. (16) Kwa Yeye vitu vyote vilivyoko mbinguni na juu ya nchi viliumbwa, vile vitu vinavyoonekana na vile visivyoonekana, kama ni viti vya enzi au falme, au wenye mamlaka au watawala, vitu vyote viliumbwa na Yeye na kwa ajili Yake. (17) Yeye alikuwapo kabla ya vitu vyote na katika Yeye vitu vyote vinashikamana pamoja. Wakolosai 1:15-17.

Huwapa watu wote uhai na pumzi. Kupitia kwa Kristo vitu vyote vinashikamana pamoja. Mawazo haya yalipasuka na nuru mpya katika uso wa Uwana wa kweli wa Yesu. Sikuelewe jinsi vitu hivi vyote vilikuwa vimeunganishwa, lakini ujenzi mpya wa mafundisho ya Bibilia ulikuwa ukichukua sura yote kwa mkataba na jiwe la pembeni la Uwana.

Mpendwa wangu akawa wa kuvutia zaidi nuru ya Uwana wake ilipofurika Katika Maandiko. Katika miaka michache, ufahamu wangu wote wa pambano kuu kati ya Kristo na Shetani na mpango wa ukombozi ulibadilika kwa kiasi kikubwa. Jinsi Nuru ya Ulimwengu ilifungua akili zangu, sasa nilikuwa tayari kwa Karamu ya kweli ya Neno.

## 10. Mkate wa Uzima



Dhana kuwa huzuni na kukosa maana iliunganishwa kwa uongo wa kujitegemea ilianza kuongeza maana ya ndani kwa anguko la mwanadamu, vita kati ya wema na uovu na mchakato mzima wa ukombozi. Macho yangu yalifungukia ukweli kwamba anguko la mwanadamu dhambini lilikuwa kuanguka katika kukosa thamani na aibu. Ni hali ya kuishi na uhalisia kwamba tunafanya vitu ambavyo Mungu haidhinishi. Katika moyo wa hali hii ya unyonge ni hamu ya kutaka kujitegemea badala ya kutegemea yule ambaye anakupa vitu vyote.

Ninapotafakari mambo haya, uzoefu wote wa Yesu akisikia sauti ya Baba yake ikimwambia kwamba alimpenda na alimkubali kama Mwanawe, sasa ilizungumza moja kwa moja kwangu.

> Nayo sauti kutoka mbinguni ikasema, Huyu ni Mwanangu mpendwa, ambaye ninapendezwa sana naye. Mathayo 3:17.

Katika ibada yangu ya awali ya Yesu wa kujitegemea, singesikia wazi Baba yangu akinena kwangu katika kifungu hiki. Ila sasa kwa kuwa nilimjua Yesu kama Mwana wa kweli wa Mungu, maneno haya yaliugonga moyo wangu kama zeri nafsini mwangu. Moyoni mwa Mwana wa pekee, akinitazma; nikimpenda na kubadilishwa naye, sasa naweza simama mahali ambapo Yesu alisimama katika nyanja yangu na kwa kweli kusikia sauti ya Baba yangu wa mbinguni ikiniambia kwamba nilikuwa mwanawe aliyempendeza. Ila kupitia kwa Kristo tu, Mwana wa Mungu, ningesikia sauti hii. Nilipotafakari mambo haya nilielekezwa kwa kauli hii ambayo ilithibitisha furaha niliyokuwa nikishuhudia.

> **Sauti ambayo ilinena kwa Yesu inasema kwa kila nafsi iaminio, Huyu ni mtoto wangu mpendwa, ambaye napendezwa naye.** "Wapenzi, sasa tu watoto wa Mungu, lakini

> bado haijadhihirika tutakavyokuwa, lakini twajua ya kwamba, Yeye atakapodhihirishwa, tutafanana naye, kwa maana tutamwona kama alivyo." 1 Yohana 3:2. Mkombozi wetu amefungua njia ili muovu zaidi, mwenye hitaji kuu, wenye kudhulumiwa zaidi na kudharauliwa, wanaweza pata fursa ya kumfikia Baba. *Desire of Ages*, page 113.

Hapa, hapa hasa katika Mathayo 3:17 palikuwa na siri ya tamaa ya moyo wangu, hamu yangu ya kujua kwamba napendwa na Muumbaji mkuu wa ulimwengu na kwamba nampendeza. Kwa kumtazama Mwana wa Mungu katika kukubaliana na Baba yake, niliweza kujiona kwa imani katika ukubaliano sawa na kuyasikia maneno hayo hayo yakienezwa kwangu. Kwa kumtazama Mwana ambaye alirithi vyote bila kuthibitisha kwa Baba kwamba alistahili, niliwezeshwa kukubali urithi wote wa upendo ambao Baba alitamani kuhifadhi juu yangu.

Ni jinsi gani natamani kwamba katika hatua hii ya maisha yangu ningekuwa nimeelewa kikamilifu Uwana wa Yesu. Baba yetu alikuwa akiniruhusu kuonja mkate wa uzima na jinsi ulivyokuwa mtamu, ingawa mtego wa minyiri ya Utatu ungenifanya kuenda mbele na nyuma wakati mwingine. Nitaelezea hili kwa maelezo zaidi katika sehemu ifuatayo, lakini ni muhimu kutaja kwamba ingawa nilionja upendo mtamu wa Mwana wa pekee, singeona kwamba bado nilikuwa nimekanganyika na kwamba nilikuwa nimejenga juu ya jukwaa la kuwaza kuwili.

Ila licha ya haya, sasa ningekuwa na vipindi vya mara kwa mara vya furaha halisi. Nilijishikilia kwa ukweli wa kudumu kwamba Baba alipendezwa nami. Sasa ningeona hilo; ningelidai hilo sasa. Nilipotereza na kuanguka, ningeangalia katika Neno la Mungu. Bado Baba alipendezwa na Mwanawe? Ndio! Basi nimekubalika katika Mpendwa. Hakika lazima anapendezwa nami. Ahadi ya uzima wa milele haikutegemea chochote nilichokitenda mwenyewe kwa sababu mara nyingi zaidi nilikuwa nikimtazama kupitia kwa Bibilia Yesu ambaye hakujitegemea mwenyewe, ila alidumu katika ahadi za Baba yake.

Nikiwa na mambo haya yote akilini, nilisoma kisa cha mgogoro jangwani na ubatizo kama vita juu ya uwana na jinsi unavyopokelewa. Shetani aliendelea kumsukuma Yesu kuonyesha Uwana wake kwa kufanya miujiza au kuuonyesha ulimwengu uwezo wake. Niliona mgogoro wa Yesu na Shetani kama pambano la jinsi uwana unaelezewa. Ni rahisi amini katika Neno linalonenwa na Baba au lazima lithibitishwe na kile ambacho mwana anatenda?

Mara nyingine tena, vita ambavyo nilisoma kuvihusu na Kristo jangwani vilikuwa jiwe la pembeni la pambano langu mwenyewe la ndani. Ni mfano upi ninaiga kushikilia uwana? Ninajaribu kufanya mambo makuu au ninaamini Neno la Baba yangu? Mara nyingine uthibitisho ulinijia.

> "Wengi huutazama mgogoro huu kati ya Kristo na Shetani [jangwani] kama ambao hauna mwelekeo muhimu juu ya maisha yao wenyewe; na kwao unamvuto mdogo. Lakini katika uwanja wa moyo wa kila mwanadamu pambano hili linarudiwa." *Desire of Ages*, page 116.

Sehemu bora kuhusu mchakato huu wote ni kwamba badala ya kutazama tu Yesu na kujaribu kuiga alichokitenda, sheria ya urithi humaanisha kwamba alichokitenda kilitolewa bure kwangu.

> Wacha yule ambaye anang'ang'ana dhidi ya uwezo wa kuwa na hamu amtazame Mkombozi katika jangwa la majaribu. Muone katika uchungu juu ya msalaba, alipolia, "Naona kiu." Amevumilia hayo yote inawezekana nasi tuyashinde. Ushindi wake ni wetu. *Desire of Ages,* page 123.

Kusherekea katika Neno la Mungu karibu kunifanye kupasuka. Ufunuo wa thamani kama huo! Ushindi wake ni wangu, kwa imani. Nilikuwa nimejaribu mara nyingi hapo awali kushikilia ukweli huu, lakini Yesu wa kujitegemea ambaye nilikuwa nikiabudu alizidi kuniondoa kwenye mwamba wa kweli pasipo kutambua kwambo yote huja kwa kurithi!

Kuona kukosa maana kutoka kwa kupoteza uwana kama sehemu kubwa ya anguko la mwanadamu, sasa niliona mgogoro wa Yesu jangwani baada

ya ubatizo wake kama jiwe la pembeni la ushindi wa Uwana uliodaiwa. Alikataa kuegemeza Uwana wake juu ya kitu chochote ila maneno ya Baba yake. "Imeandikwa" ilikuwa majibu pekee ambayo alitoa, kamwe hakujibu shuku kuhusu kama kweli alikuwa Mwana wa Mungu au alihitaji kuthibitisha alikuwa nani kwa miujiza na uwezo.

Kwa ufahamu huu mpya wa jinsi Yesu alirejesha utambulisho wetu kama wana na binti za Mungu, sasa naweza anza kuona hili katika ujumbe wa Eliya.

> Angalieni, nitawapelekea Eliya nabii, kabla haijaja siku ile ya Bwana, iliyo kuu na kuogofya. (6) Naye ataigeuza mioyo ya baba iwaelekee watoto wao, na mioyo ya watoto iwaelekee baba zao, ili nisije nikaipiga dunia kwa laana. Malaki 4:5,6.

Katika moyo wa Eliya, ujumbe ni kuigeuza mioyo ya watoto kwa baba na baba kwa watoto. Hili lilinielekeza kwa kifungu hiki

> Wana wa wana ndio taji ya wazee, Na utukufu wa watoto ni baba zao. Methali 17:6.

Na utukufu huu wote ulitambuliwa kwa mfumo wa thamani unaosema:

> Bwana asema hivi, Mwenye hekima asijisifu kwa sababu ya hekima yake, wala mwenye nguvu asijisifu kwa sababu ya nguvu zake, wala tajiri asijisifu kwa sababu ya utajiri wake; (24) bali ajisifuye na ajisifu kwa sababu hii, ya kwamba ananifahamu mimi, na kunijua, ya kuwa mimi ni Bwana, nitendaye wema, na hukumu, na haki, katika nchi; maana mimi napendezwa na mambo hayo, asema Bwana. Yeremia 9:23-24.

Kama mwana wa kweli wa Mungu sikuhitaji kujisifu kwa sababu ya hehima, nguvu au utajiri; nilihitaji tu kujisifu kwa kumjua Baba yangu kupitia kwa Kristo. Nakumbuka nikiwasilisha kanuni hii kwa hadhira yangu kule Sydney, na kuona furaha iliyoangaza nyuso za watu wengine walipoanza kushika mtazamo wa ufalme wa Baba.

Asubuhi na mapema asubuhi iliyofuata, niliamshwa na sauti ya kuimba. Nilisikia katika mawazo yangu wimbo maarufu wa Charles Wesley.

Niwezeje nipate uzima
katika damu ya Mwokozi Yesu;
Alinifilia pendoni,
mimi niliye msulubisha,
upendo mkuu wa kushangaza sana,
wewe Mungu wangu ulinifilia pendoni
upendo mkuu washangaza
Mungu wangu kunifilia

Nilipotafakari kuhusu maneno haya na uhakika wa uwana wangu kwa Baba kupitia kwa Kristo na kwamba Baba yangu wa mbinguni kweli alikuwa sababu ya kujisifu, nilihisi kuzidiwa na hisia ya upendo, furaha na amani zikinibeba. Hisia ya upendo niliyokuwa nayo ilikuwa kuu kiasi kwamba singeweza kuzungumza kwa vile machozi ya furaha yalinidondoka. Kwa kweli siwezi elezea hisia hiyo kikamilifu.

Nilifikia katika imani ya ndani kwamba nilihitaji kushiriki hili na wengine. Niliomba nguvu za kushiriki ujumbe huu wa thamani wa kile ina maanisha kuwa mwana wa Mungu kupitia kwa Kristo. Nilipoketi pale na kukumbuka masuala yote ya ujumbe ambao nilikuwa nimejifunza katika nafasi ndogo kama hiyo na mibaraka ambayo yalikuwa yameleta maishani mwangu, nilimwabudu Baba yetu tu na Bwana wetu Yesu kwa mambo mazuri kama hayo. Yote ya ufahamu huu wa kupendeza yalikuwa yanapata nuru kupitia utu wa Mwana wa mungu.

Kutoka kwa hatua hii ni na hamu ya kusonga mbele na kushiriki furaha niyokuwa nimepata. Lakini hata katika kusonga mbele huku kuna baadhi ya mambo ambayo nilihitaji kujifunza, mambo ambayo yangeniwezesha kwa kweli kuingia katika uzoefu wa Patakatifu pa Patakatifu.

## Kiingilio II

Katika utulivu wa pambazuko, namngojea. Mpendwa wangu anasongelea kwa upesi milimani, njia potovu anainyoosha. Ushirika wetu ni mzuri. Ananinogonezea kutoka kwa hazina yake aliyorithi; maneno yake yalianguka kama asali kwenye midomo yangu. Ni jinsi gani maneno yake yalivyo matamu kwa ladha yangu.

Kama chemchemi yenye kina, Mpendwa wangu anatiririsha mto wa kioo wa maji ya uzima kwa nafsi yangu. Nafurahia kuonja maji haya ya uzima ingawa kuna vitu ambavyo huniacha kama nimeduwa. Mpendwa wangu mpenzi, samehe upole wangu wa moyo katika kushika kila tone la ufahamu unaotia kwangu. Tafadhali niruhusu nishike pumzi yangu na kuchukua muda wa kuafikiana na furaha hii.

Kama tu wangemjua Mpendwa, kama wananchi wangu kweli wangekujua! Basi wangejua mbona nakupenda, mbona ushirika wako ni mzuri. Naufungua moyo wangu kwa wingi wa shukurani kwa kunionyesha njia ya kwenda kwa Baba kupitia kwa Uwana. Nilihisi upendo wa Baba kwako moyoni, ninaushahidi wa kuwa mrithi mwenza nawe, Mpendwa wangu. Unapendeza kwa vyote.

Utanipeleka, Mpendwa wangu, Patakatifu pa Patakatifu? Nimetamani kwa muda kupata njia, ila nimekuwa nikiteleza na kuanguka kwa machozi ya aibu. Kama mwana wa Adamu wa kwanza, ninapofushwa na jinsi ya kupata mlango. Utanipeleka, Mpendwa wangu? Utanipeleka kwa pahali pa siri pa Patakatifu pa Patakatifu? Najua kwamba sisitahili, lakini naweka imani yangu kwako, kwa maana wewe ni Njia ya Uzima.

> Nikaondoka nimfungulie mpendwa wangu; Mikono yangu ilidondoza manemane, Na vidole vyangu matone ya manemane, Penye vipini vya komeo. (6) Nalimfungulia mpendwa wangu, Lakini mpendwa wangu amegeuka amepita; (Nimezimia nafsi yangu aliponena), Nikamtafuta, nisimpate, Nikamwita, asiniitikie. Wimbo Ulio Bora 5:5-6.

# Sehemu 3. Kusita Kati ya Mawazo Mawili

## 11. Vita Baina ya Mwili na Roho

Lilikuwa jambo la kukatisha tamaa sana! Maarifa haya yote ya kupendeza kuhusu Mpendwa wangu, na bado jinsi mshawishi angenipotosha virahisi kupitia kwa njia mbalimbali. Shetani alikuwa ametumia fursa ya utoto wangu na ujana wangu na kutia nafsini mwangu pendo la raha, burudani na hamu. Alinifunza katika moyo wa kujitegemea, elimu na kupenda michezo yenye ushindani.

Mpendwa wangu alipoanza kujionyesha zaidi kwangu na nikahisi kuwa na upendo naye zaidi, mpenzi wangu wa awali alianza kushikilia msingi ambao alikuwa nao kwangu na kujaribu kuniondoa kwa Mpendwa wangu kile ambacho alikuwa amepoteza. Hata ingawa nilimpenda Yesu kweli, sikujua kwamba hali yangu ya kidunia bado ilidai ukuu. Sehemu mbaya zaidi ya hali ya anguko ni tabia iliyopangwa vizuri kwa kutumia mantiki yakiunganishwa na uongo kuficha nia na hamu ya kweli.

> Ni nani awezaye kuyatambua makosa yake? Unitakase na mambo ya siri. Zaburi 19:12.

> Moyo huwa mdanganyifu kuliko vitu vyote, una ugonjwa wa kufisha; nani awezaye kuujua? (10) Mimi, Bwana, nauchunguza moyo, navijaribu viuno, hata kumpa kila mtu kiasi cha njia zake, kiasi cha matunda ya matendo yake. Yeremia 17:9-10.

Katika wakati wangu wa kusherehekea Neno katika Patakatifu pa Patakatifu, nilikutana ana kwa ana na majaribu kadha kutoka kwa maisha yangu ya awali. Wakati mwingine nilihisi kuvutiwa sana kwa kutazama aina mbalimbali ya burudani kwenye televisheni. Mara nyingi nilitekwa na kutazama, lakini katika kipindi kifupi singepata kuridhishwa kabisa. Nilihisi kutegwa nasikufahamu mbona. Nilikuwa nimeomba ushindi, lakini hamu ingerejea. Katika miaka yangu ya uchanga nilikuwa nimetiwa moyo kuonekana mwenye haki kama walivyokuwa wengi katika rika yangu. Hili

lilinifanya kuonekana kuwa na ushindi juu ya majaribu kadha, lakini ilikuwa udanganyifu na mshawishi alijua hilo.

Ushindi mwingi katika maisha yangu ulikuwa vigumu kuupata. Nilisimama karibu na Patakatifu pa Patakatifu nikitamani kuingia, lakini kitu kilikuwa kinazuia njia yangu na sikuelewa kilikuwa nini. Kusoma kwangu Danieli na Ufunuo kulinisadikisha kwamba kazi ya upatanisho ingeisha karibuni, na wale tu ambao walikuwa wamesafisha mavazi yao katika haki ya Yesu ndio wangeingia kwenye mji. Niliona baadhi katika rika yangu wakivuna bidii yao ya kuingia Patakatifu pa Patakatifu, na walifunza kwamba kwa sababu ya upendo mkuu wa Yesu kwa wenye dhambi, atawasamehe na kufunika dhambi zao na haki hadi marejeo yake ya pili. Mafundisho kuhusu ushindi juu ya dhambi yakawa moja ya ukomavu wa Mkristo, kwa vile sheria ya Mungu haikuonekana tena kuweza kutunzwa kikamilifu.

Kile ambacho nilisoma ndani ya Maandiko kilipingana na kile ambacho wengi wa rika yangu walikuwa wakisema, ila uzoefu wangu ulionekana kuashiria kwamba walikuwa sawa. Ningewezaje kukiri kuamini katika ushindi juu ya dhambi wakati ambao nilikuwa na uzoefu wa kuyumba kama huo? Ni haki gani niliyokuwa nayo kutoa tumaini la ushindi katika maisha wakati ambao mimi mwenyewe sikuwa nina ushuhudia?

Wakati ambao ningeanguka katika majaribu, nilijua kwamba Baba yetu alinipenda na kwamba kupitia Kristo nilipokea msamaha, lakini nilitaka kutembea na mkombozi wangu wakati wote na kutomtonesha kidonda kwa maneno yangu ya kutojali na matendo bila kufikiria ambayo mara nyingi yalikuwa binafsi. Ndio, Mungu hutusamehe, lakini bado dhambi husababisha uchungu katika mahusiano yetu. Bibilia iliniahidi kwamba ningewacha kuwaumiza waliokuwa karibu nami, ila ni mara ngapi nilianguka.

> Kwake Yeye awezaye kuwalinda msianguke na kuwaleta ninyi mbele za utukufu Wake mkuu bila dosari kwa furaha ipitayo kiasi, Yuda 24.
>
> Kwa hiyo, kwa kuwa Kristo aliteswa katika mwili Wake, ninyi nanyi jivikeni nia iyo hiyo kwa maana mtu aliyekwisha kuteswa katiaka mwili ameachana na dhambi; 1 Petro 4:1.

> Kila mtu akaaye ndani yake hatendi dhambi. Kila mtu atendaye dhambi hakumwona Yeye wala hakumtambua. (7) Watoto wadogo, mtu ye yote na asiwadanganye. Kila mtu atendaye haki ana haki, kama Yeye alivyo na haki. 1 Yohana 3:6-7.

> Kwa njia hii, upendo hukamilishwa miongoni mwetu ili tupate kuwa na ujasiri katika siku ya hukumu, kwa sababu kama alivyo ndivyo tulivyo sisi katika ulimwengu huu. 1 Yohana 4:17.

> Hapa ndipo penye subira na uvumilivu wa watakatifu, yaani, wale wanaozishika amri za Mungu na kudumu kuwa waaminifu kwa Yesu. Ufunuo 14:12.

Mkombozi wangu mwenye hekima na upendo aliniacha kuhisi athari asili ya ufahamu wa uongo kumhusu ambao bado nilishikilia. Vipindi hivi vya mgogoro, majaribu na ibada ya sanamu viliongeza utafutaji wangu wa sehemu zilizokosekana. Kila wakati nilipopiga magoti mbele ya Baba na kumsihi anipe hekima na maarifa kupitia kwa Yesu, ndivyo nilivyo karibia nuru.

Mmoja anaweza fikiria kuwa ufahamu wangu wa Yesu kama Mkombozi wa dhambi za ulimwengu ungetosha na kwamba singesumbukia vitu vingine. Hoja ni kwamba majaribu yalikuja kila siku, dhihirisho la hali ya kidunia lilikuwa likiniandama bado. Sauti ya Mpendwa wangu na sauti ya mshawishi bado zilikuwa zikiungana akilini mwangu mahali fulani.

Katika juhudi zangu za kumwabudu na kumwinua Mkombozi wangu, pasipo kujua nilihusika katika ibada ya masuala haya ambayo hayakuwa yamedhihirishwa katika Maandiko. Pasipo kujua nilimjua Kristo katika muktadha mkuu wa kujitegemea. Mambo haya zaidi yalitoka kwa baba zangu wa kale wa kiroho na yakawa na hisia asili nami. Ladha ya kujitegemea ambayo nilikuwa nimependa kama mtoto na ilikuwa imekuzwa na mshawishi ilikuwa imeingia moyoni katika utu wa Yesu ambaye nilidai kumwabudu.

Ufahamu wangu tu wa Yesu ulikuwa umenijia kupitia kile ambacho nilikuwa nimefunzwa kama mtoto na familia yangu na kanisa langu. Nilikuwa nimefunzwa kwamba Yesu ni Mungu, na Baba ni Mungu, na Roho ni Mungu. Nilifunzwa kwamba wote walikuwa mungu na kwa hivyo

walikuwa sawa. Muktadha wangu wa usawa huu kwa uasilia ulionekana kuwa ule wa kujitegemea kutoka kwa nguvu, uwezo, na maarifa asili. Kwa hivyo kamwe sikuuliza jinsi Baba, Mwana na Roho walikuwa sawa. Nilidhani hili lilimaanisha kwamba wote walikuwa na uwezo na nafasi sawa. Hii ndio maana ya usawa katika ulimwengu, na kwa hivyo nikadhani hivi ndivyo ilivyo kwa Mungu pia. Haikuwa imeniangazia kwamba kama Mungu alikuwa watu watatu ambao walikuwa sawa katika uwezo basi maana ya maneno yenyewe ingebadilika. Maneno *Baba* na *Mwana* hasa yangekoma kumaanisha kile ambacho yalisema. Kama Baba na Mwana walikuwa sawa katika uwezo, miaka na cheo basi haingewezekana kwa mtu wa pili kutoka kwa mtu wa kwanza kwa sababu hilo lingemfanya mtu wa pili kumtegemea au chini ya mtu wa kwanza.

Uongo wa Shetani kwa Hawa ulieleza kwamba sisi ni viumbe wa kujitegemea; umetiwa mhuri katika hali yetu haswa na unapitishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Sauti ya mshawishi ili saisi roho hii ya kujitegemea ndani yangu kupitia kwa familia yangu, elimu na uzoefu wa jamii. Wakati utu wa Yesu uliwasilishwa kwangu kama ambaye anajitegemea na ila inaonyesha utiifu na unyenyekevu kwa manufaa yetu binafsi tu, nahisi kwa hilo. Mtazamo wangu wa Mungu kama mwenye nguvu zaidi, mwenye enzi yote, na wa kujitegemea kabisa akifungwa kikamilifu na mafundisho ya Utatu ambao uliwasilisha viumbe watatu wenye uwezo kama muungano wa mmoja wa ushirika wa familia takatifu.

Singeona kwamba kupitia kwa mtego uliowekwa kwa ujanja, Mungu wa ukweli na Mwanawe walikuwa wameunganishwa na mungu wa uongo ambaye alikata rufaa kwa hali yangu ya kidunia. Wakati mwingine ningelenga kwa uhusiani wa Baba na Mwana na kuvutwa kwao. Kisha ningeteleza katika masuala ya uwezo na kujitegemea, na hili lingenipelekea kuwa vile hasa.

Roho wa kujitemea ulipiga gumzo na michezo na senema nyingi. Wakati ningetaza washindi wa Olympiki wakionyesha uwezo wao, ujuzi na uhodari wa kushinda medali ya dhahabu, nilivutiwa na hili kwa sababu sehemu ya mungu niliyemwabudu ilidhihirisha nguvu, uwezo na uhodari katika onyesho la kujitegemea. Nilipotazama timu ya watu ikilazimisha

kupita ukuta wa watu wengine kutia mpira kwenye mstari, nilihisi uwezo na kupongeza onyesho. Iliguza kikamilifu mshipa katika mwili wangu. Ila roho huyu alikuwa vitani na Yesu mnyenyekevu na mpole ambaye daima alifanya mambo ambayo yalimpendeza Baba yake. Hakufanya chochote chake yeye mwenyewe lakini aliamini vitu vyote mikononi mwa Baba yake. Roho huyu hakuwa wangu asilia, lakini kupitia kwa kukutana na Mpendwa wangu, nilianza kuonja Roho huyu na kwa hivyo nikaitamani. Hili lilisababisha mgogoro mkubwa ndani yangu.

> Kwa maana mwili hutamani yale yaliyo kinyume na Roho, nayo Roho hutamani yale yaliyo kinyume na mwili. Roho na mwili hupingana na kwa sababu hiyo hamwezi kufanya mnayotaka. Wagalatia 5:17.

> Ole wangu, mimi maskini! Ni nani atakayeniokoa na mwili huu wa mauti? (25) Ashukuriwe Mungu kwa njia ya Yesu Kristo Bwana wetu! Hivyo basi, mimi mwenyewe kwa akili zangu ni mtumwa wa sheria ya Mungu, lakini katika asili ya dhambi ni mtumwa wa sheria ya dhambi. Warumi 7:24-25.

Vita moyoni mwangu vilikuwa kati ya maarifa mawili tofauti ya Kristo ambaye nilimpenda. Upendo wangu wa utotoni kimsingi ulikuwa onyesho langu binafsi kama kujitegemea, mtu mwenye uwezo ambaye alishinda pongezi na heshima ya wale walionizunguka. Mtu wa pili alikuwa Yesu mpole na mnyenyekevu ambaye alimpenda na kumwamini Baba yake ambaye vyote alivyokuwa navyo vilitoka kwake. Bila kuzingatia chochote cha ujuzi wake, talanta au uwezo, Mkombozi huyu alikuwa amebarikiwa na kupendwa na Baba yake kwa sababu tu alikuwa ametoka kwake.

Nilikuwa nimefungwa katika pambano hili katika mitazamo hii miwili ya Kristo kwa sababu fomyula ya Utatu iliyoonyeshwa kwa makini ilikuwa imefanya vigumu kwangu kuvitenganisha. Kulikuwa na mambo ya utamaduni ambayo yaliongezeka kwa ugumu wangu wa kutambua tofauti. Ni kwa suala hili tunageukia aidha.

## 12. Drama ya Utambulisho Uliobadilishwa



Wakati wa kristmasi ulikuwa wakati wakuvutia kwangu kama mtoto. Nakumbuka mtu akivalia kama Santa Claus na kuwapa watoto zawadi katika vituo vya ununuzi tulipokuwa tukifanya ununuzi. Pia nakumbuka kisa cha mtoto Yesu horini akichezewa kwa uaminifu katika rangi za kudumu na Darasa la Shule ya Sabato.

Nilipokua, niliona nyota wa senema wakivaa na kuchukua jukumu la shujaa wa magharabi au mjini kuokoa siku. Utoto na ujana wangu ulikuwa umejawa na drama. Wazo nzima la mtu mmoja kuchukua utambulisho wa mtu mwingine kwa lengo la kufanya hoja ya maadili kuwa sehemu ya kitambaa cha maisha yangu. Baada ya mamia ya saa za kutazama watu wanachukua utambulisho wa watu wengine ili kuelezea kisa chenye maana, nilikuwa nimekengeushwa na dhana kwamba hivi ndivyo ulimwengu hufanya kazi. Sikuwa nimefunzwa hili, lakini badala yake nililishika kupitia kwa utamaduni wangu.

Tabia hii ya kuwatazama watu wakichukua utambulisho wa wengine pia ikawa dirisha ya kukimbilia ambayo ningeweza kujifikiria katika uwepo wenye uwezo kuliko kile nilichokaa sasa. Kutazama senema ikawa kama tabia ambayo kwayo ningechukua utambulisho wa mwingine kwa lengo la kujifikiria kupata heshima na makini niliyotamani.

Utoto wangu ulipogeuka ujana na tamaa za utoto wangu zikawa ngumu kuzitambua, dirisha la utambulisho niliochukua likawa hoja muhimu katika kudumisha uongo wa kujitegemea na uhuru. Siri ilikuwa kuunganisha utambulisho wangu na mtu ambaye nilitamani kuiga. Kupitia kwa kuvaa upendo wangu wa kwanza wa utotoni, dirisha la kuingia kwa uwezo lilikuja kupitia kwa kusalimisha utambulisho wangu. Sikutambua kwamba mchakato huu ungegharimu utambulisho wangu, kwa sababu kitu tu ambacho kilijalisha kilikuwa uwezo. Matumizi ya drama na senema

kulijenga sehemu ya msingi ya mbinu ya mshawishi ya kunidumisha kama nimefungwa katika uongo wa kujitegemea. Pia ilinipofusha kikamilifu kwa ibada ya sanamu ya Utatu.

Utatu ulikuwa onyesho kamili la utambulisho uliochukuliwa kwa lengo la maadili; watu watatu wakichukua majukumu ya Baba, Mwana na Roho kwa lengo la kutoa kauli yenye maadili ya juu kuhusu ukombozi. Hili liliingia kikamilifu na kujificha kwangu kupitia drama. Tena, kisa kilisambazwa nami, kwa sababu kilikuwa asili kama kupumua.

Kama vile tu kamwe sikuona utambulisho uliochukuliwa husababisha hasara au kukanganyika kwa yule mtu aliye, ndivyo kamwe sikuona kwamba katika kuamini kwamba watu watatu watakatifu kuchukua utambulisho wa wengine kwa kweli kulisababisha hasara na mkanganyiko wa wale waliokuwa. Hili likawa siri ya Mungu! Wakati wote lilileta maana kamili kwa mawazo yangu asili.

Haipaswi kudunishwa kwamba uongo wa msingi ulionenewa Hawa uliwasilishwa kupitia kwa kiumbe ambaye alikuwa amejibadilisha kwa utambulisho tofauti kabisa. Wacha kamwe tusisahau kwamba hali yetu ya ubinadamu kutoka kwa Adamu imetiwa mhuri kwa ujumbe wa kijitegemea unaopitishwa kupitia kwa njia ya utambulisho uliobadilishwa.

Ujumbe huu ulitiwa mhuri zaidi katika mawazo yangu kwa kutazama mashujaa wakubwa wa kubadilishwa kama vile Superman, Spiderman na wengine. Wahusika hawa walikuwa na uwezo wa ndani ambao wangeutumia wakati wamebadilishwa. Uwezo huu kwa kawaida ulitumika kwa lengo la maadili na kwa ubora wa jamii. Kanuni ya msingi iliyokuzwa ilikuwa *kufikia uwezo wa ndani kupitia utambulisho uliobadilishwa*. Mara kwa mara somo hili lilirudiwa kwangu. Badala ya kupiga goti na kuomba kwa Baba yangu wa mbinguni, nilionyeshwa kwamba mashujaa wa kweli waliitisha uwezo wao wa ndani kwa kujibadilisha. Tena, nilikuwa nikinywa roho wa kujitegemea kwa kujibadilisha.

Katika miaka yangu ya awali ya ujana wangu niliwekwa wazi kwa mtindo mwingine wa kujitegemea kwa kujibadilisha. Mfululizo wa “Star Wars”

ulioandikwa na George Lucas uliwasilisha mashujaa wake wazuri kama wakuu wa upatanisho. Kupitia kwa sanaa ya mkusanyiko na kufuata hisia za ndani, mtu anaweza tenda matendo makubwa katika vita na kushinda sifa za kila mmoja ambaye alishuhudia. Hii ilikuwa hila yangu ya kuanzishwa kwa upagani wa mashariki.

Hivyo kwa sababu hizi zote mara nyingi nilijipata nikivutwa kwa televisheni kushiriki katika mazoea ya mungu wa utoto wangu na hilo lilikuwa kukuza uongo wa kujitegemea kupitia kwa utambulisho uliobadilishwa. Ningejifikiria kama mhusika mkuu wa senema na ningehisi uwezo aliouonyesha. Kadri nilivyoendelea kumwabudu mungu aliyeshiriki katika kujitegemea kwa kujibadilisha. Kwa kweli singepoteza upendo wangu wa senema, michezo na visa vya fantasia.

Mwelekeo mwingine wa mafundisho yangu kutoka kwa televisheni ulikuwa falsafa ambayo huvutia vinyume. Hadithi yote wazi ya yin/yang ilichezea tu kwa kisa cha upendo, mara nyingi ikitoa mada za vinyume vikiunganishwa pamoja kwa uwezo mkubwa, riziki na kuridhishwa. Mafundisho haya yaliweka anguko kamili la kuunganisha Yesu wa mbinguni mwenye uwezo, wakujitegemea na Yesu wa duniani mtiifu, mnyenyekevu na mwenye kuheshimu kuwa kitu kimoja.

Ninapotazama nyuma sasa ninaona mengi katika kuingiliana na jamii kupitia utoto wangu ulijenga msingi wa kuniandaa kukubali mungu wa utatu kama kitu ambacho kilikuwa asili, kawaida na bila shaka. Msisitizo wa kutazama ndani na roho wa kujitegemea uliendana kikamilifu na sura ya viumbe hawa watatu waliojibadilisha katika tabia ya Baba, Mwana na Roho.

Tabia ya Mpendwa wangu ambaye alimwamini Baba yake na daima alitii, kuamini na kumtazama iliunganishwa na kumezwa na sura zangu nyingi za kujitegemea, kutafuta nafsini na kubadilishwa katika uwezo wa Uungu.

Ni jinsi gani mambo yangekuwa rahisi kama ningekuwa nimefahamu maneno haya:

Yesu Kristo ni Yeye yule jana, leo na hata milele. Waebrania 13:8.

Kisha tupate kwamba mambo mengi yangekuwa rahisi zaidi kama ningeendelea kusoma Bibilia kwa uwazi. Ila mara nyingine tena, ulezi wangu na elimu viliweka kipimo machoni mwangu kunizuia kutenda hilo tu.

## 13. Michezo ya Akili



Siku moja nilipokuwa nikicheza na rafiki zangu shuleni, mtu aliniita kwa bidii, “Adrian! Unamgawanyiko kwenye suruali yako.” Moyo wangu ulianza kupiga kwa kasi nilipogeuka upesi kutafuta mgawanyiko ulikua wapi. Kisha nikasikia kicheko kikubwa pamoja na maneno “Gotcha!” karibu katika ulimwengu wa masihara. Mara moja maisha yangu yakawa mchezo wa maisha yangu ya kuchenga na kurusha mishale hii ya udanganyifu.

> Kama mtu mwenye wazimu atupaye mienge, Na mishale, na mauti; (19) Ndivyo alivyo amdanganyaye mwenzake, Na kusema, Je! Sikufanya mzaha tu? Methali 26:18-19.

Lilikuwa jambo la kuhuzunisha kushikwa na darasa zima la watoto kukucheka. Uzoefu wa riika ulinifunza kamwe nisiwe kwenye hatari, kamwe nisimwamini yeyote na la muhimu zaidi, kujizuia kutochukulia kila kitu ambacho watu wanasema kuwa makini.

Vipengele tawala na muhimu zaidi vya masihara ni kuainisha kinyume cha kile ambacho ni kweli na kuvuta watu wenye akili halisi za kudanganywa katika hali ya kukanganywa ili kuchekesha. Katika miaka yangu ya ujana, nilikuwa nimefungwa katika roho huyu wa udanganyifu, kukanganya na burudani kwa kufurukuta maneno kumaanisha jambo lingine tofauti na maana halisi. Hata hivyo, jambo la kwanza ambalo Mpendwa wangu alinifanya kuamini baada ya kubadilika lilikuwa kanuni ya kusema nilichomaanisha.

> ‘Ndiyo,’ yenu iwe ‘Ndiyo’ na ‘Hapana’, yenu iwe ‘Hapana.’ Lo lote zaidi ya hili latoka kwa yule mwovu.’’ Mathayo 5:37.

Mishale ya udanganyifu ilichukua nafasi katika kujaribu kunizuia kuingia kupitia kwa mlango mwembamba[5] ndani ya ua la Patakatifu. Niliaminishwa kabisa kuhusu suala hili nilipojifunza kwamba masihara yalikuwa aina ya kushuhudia uongo na kwa hivyo kukiuka amri ya tisa.

> Usimshuhudie jirani yako uongo. Kutoka 20:16.

Pia nilijifunza kuwa moja wapo wa vitu ambavyo wafuasi wa Yesu wangeacha kufanya ni kuhusika katika hila.

> Kwa kuwa ninyi mliitwa kwa ajili ya hayo, kwa sababu Kristo naye aliteswa kwa ajili yenu, akiwaachia kielelezo, ili mzifuate nyayo zake. (22) Yeye hakutenda dhambi, wala udanganyifu haukuonekana kinywani mwake. 1 Petro 2:21-22.

> Hawa ndio wale ambao hawakujitia unajisi kwa wanawake, kwa kuwa wao ni mabikira. Wao humfuata Mwana -Kondoo kila aendako. Hawa wamekombolewa kutoka miongoni mwa wanadamu wakawa malimbuko kwa Mungu na kwa Mwana-Kondoo. (5) Vinywani mwao hapakuonekana uongo, wala hawakuwa na hatia yo yote. Ufunuo 14:4-5.

Hila (Guile) inaelezewa:

> to decoy; compare G1185); a trick (bait), that is, (figuratively) wile: - craft, deceit, guile, subtilty.

Kinachovutia mno kwangu ni kwamba mahali ambapo nilihisi roho huyu zaidi ni katika fundisho langu la seminari kwa huduma. Niliipata kuwa vita vya mara kwa mara kutovutwa katika roho wa kicheko kupitia kwa ufundi wa masihara. Niliomba bila kukoma kwa msaada nisiingie katika suala hili. Wakati wowote ningeonyesha mwelekeo wakusoma kifungu cha Bibilia

---

[5]. "Hatua chache kutoka kwenye lango hili kumesimamishwa ngome yenye nguvu, ambayo Beelzebub ndiye nahodha: kutoka pale yeye pamoja na walionaye, hulenga mishale kwa wale ambao wanakaribia lango hili, wakitaraji wanaweza kufa kabla ya kuingia ndani. Kisha akasema Kristo, nilifurahi na kutetemeka." *Mwendo wa safari hatua ya pili (Pilgrim's Progress* Second Stage).

katika maana yake wazi, kicheko na dharau mara nyingi zingejaza masikio yangu.

Mafundisho ya masihara (indoctrination of jest) ya mshawishi yalinifundisha nisiyachukulie maneno kwa umakini na kutafuta maana fiche. Masihara (Jest) yaliwezesha uthamini wangu wa mtindo wa allegorical wa Alexandrian katika kujifunza Bibilia. Maana ya maneno haipo katika usomaji halisi. Masihara yalikuwa mchezo wa wazo moja tu ambalo liliathiri usomaji wangu wa Bibilia na utambulisho wa kweli wa Mpendwa wangu.

Mtindo rahisi wa kuelezea kisa wa televisheni ulinifunza dhana ya usawa sambamba. Katika wakati tofauti wa maisha yangu niliwekwa wazi kwa vipindi vya televisheni ambavyo vilionyesha familia zikifanya kiungwana vitu vya kawaida. Vipindi hivi vilikuwa Vipindi viliyoratibiwa (serial programs), kumaanisha vingekuwa na sehemu kila siku au kila siku ya juma. Katika kipindi cha wakati, nilipata ujuzi wa wahusika na kuanza kujitambulisha nao. Wahusika hawa wakawa sehemu ya maisha yangu zaidi kiasi kwamba mara nyingi ningejifikiria kuwa kati yao, ni kawa na wasiwasi kuhusu vitu walivyokuwa wakikabiliana navyo na wakati mwingine hata ningeota kuwahusu kama sehemu ya ulimwengu wangu.

Vipindi hivi vilivyoratibiwa (serial programs) viliniruhusu kimawazo kuingia katika uhalisia mwingine tofauti na wangu binafsi. Kwa mfano, unapotazama kitu ambacho kinatisha, ningejiambia, “ilikuwa senema tu.” Tabia hii iliniruhusu kushuhudia hisia zote za uhalisia sambamba, na ingawa ningetoka kwayo wakati haikunifaa. Na wakati mchakato huu ulikuwa na nguvu zaidi katika vipindi hivi viliyoratibiwa, ilikuwa sawa kwa senema yoyote. Matumizi ya picha na sauti za watu wanaohusika katika shughuli za maisha halisi yalijenga ulimwengu wa muigo ambao ulinivuta kutoka kwa wangu.

Bila kujali yaliyomo, mchakato wa kuishi katika usambamba au uhalisia ulioigwa uriathiri jinsi nilisoma Bibilia. Kuliweka msingi kamili wa kuruhusu Yesu kuingia katika uhalisia sambamba kama mtu wa duniani. Alichotenda duniani hakikuwa alivyokuwa kweli. Hakuwa wa kutegemea, Mwana

mwaminifu katika uhalisia, alikuwa tu amekanyaga ndani ya uhalisia huu mbadala kwa lengo la kutoa kauli yenye maadili. Hili lilikuwa sawa na senema nilizozitazama. Nyingi yazo zilijaribu kutoa kauli yenye maadili ya namna fulani kupitia kwa uhalisia sambamba na wangu binafsi.

Moja ya usemi huu wa uhalisia sambamba ambao ni wa kawaida umekuwa "hili lilikuwa tu wakati wa kiwiwili (This was only during the incarnation)." Unganiko ovu la uhalisia sambamba na mabadiliko ya utambulisho lilifanya kuwaza kwa namna hii kuwa rahisi zaidi. Ningesoma semi za Bibilia kama zifuatazo na kuziweka katika uhalisia sambamba ambao kimsingi ulikuwa fantasia.

> Yesu akawaambia, Amin, amin nawaambia, Mwana hawezi kufanya jambo lo lote peke yake, Yeye aweza tu kufanya lile analomwona Baba yake akifanya, kwa maana lo lote afanyalo Baba, Mwana pia hufanya hivyo hivyo. Yohana 5:19.
>
> Kama vile Baba alivyo na uzima ndani Yake, vivyo hivyo amempa Mwana kuwa na uzima ndani Yake; Yohana 5:26.
>
> Nao uzima wa milele ndio huu, wakujue Wewe uliye Mungu wa pekee, wa kweli na Yesu Kristo uliyemtuma. Yohana 17:3.
>
> Zamani Mungu alisema na baba zetu kwa njia ya manabii mara nyingi na kwa njia mbalimbali, (2) lakini katika siku hizi za mwisho amesema nasi kwa njia ya Mwanawe, ambaye amemweka kuwa mrithi wa vitu vyote, ambaye kwa Yeye aliuumba ulimwengu. (3) Mwana ni mng'ao wa utukufu wa Mungu na mfano halisi wa nafsi Yake, akivihifadhi vitu vyote kwa neno Lake lenye uweza. Akiisha kufanya utakaso kwa ajili ya dhambi aliketi mkono wa kuume wa Ukuu huko mbinguni. (4) Kwa hiyo alifanyika bora kuliko malaika kama Jina alilorithi lilivyo bora kuliko lao. Waebrania 1:1-4.

Wakati wowote mawazo yangu yangeamini kwamba mafungu haya yanafaa kusomwa kihalisia, ufahamu wangu kwamba Yesu alikuwa sawa na Baba kwa uwezo wake wa kujitegemea ungeweka mafungu haya katika uhalisia sambamba wa fantasia kwa lengo la kutoa kauli yenye maadili. Nilifanya hivyo moja kwa moja bila hata kutambua. Akili yangu ilikuwa imeratibiwa namna hii kwa miaka mingi, na mafundisho haya yalifanya

kazi kikamilifu kuzuia kutoroka kwangu kutoka kwa viumbe watatu ndani ya mungu mmoja kuitwao Utatu.

Kila wakati tunapotazama senema au mfululizo wa kisa cha aina yoyote, pasipokuzingatia yaliyomo, tunaratibiwa kwa uhalisia sambamba ambao unaweza fikiwa au kukataliwa wakati wowote. Hata visa vya kweli vikiwakilishwa kwa muundo huu wa senema zinaweza leta athari hii, kwa sababu harakati za watendaji na mwingiliano unaotazamwa moja kwa moja hujenga uhalisia huu sambamba na hutufanya kuingia ndani yake.

Hili ni tofauti kabisa na kusoma visa vya Bibilia na kuruhusu Roho wa Mungu kutuvutia kwa kile ambacho vinamaanisha. Tunapofundishwa kusoma Bibilia kihalisia na sio kuenda zaidi ya mipaka ya Maandiko, tunawezapata funzo kutoka kwa visa, lakini hatuingii katika uhalisia sambamba ambao hutufanya kuacha wetu binafsi. Wakati mwingi baada ya kutazama senema, ishara za kuelezea hadithi kwamba nilikuwa nimeingia katika uhalisia tofauti ni kwamba mara nyingi ningekuwa na kipindi cha kuchanganyikiwa kuhusu nilipokuwa, wakati gani, na kile ninachopaswa kuwa nikikifanya wakati ujao.

Nakumbuka senema moja hasa ambayo iliniacha katika hali hiyo kwa karibu siku tatu. Niliendelea kuishi tu katika uhalisia sambamba na singeweza kutoka ndani yake. Matukio yangecheza mara kwa mara akilini mwangu, na ningepitia hisia hizo tena na tena. Mchakato huu ni tofauti kabisa na kusoma Bibilia kwa uwazi na urahisi. Kamwe tusipoteze mwelekeo wa uhalisia na hali yetu ya sasa. Akili zetu hazishambuliwi na picha ishirini na tano hadi thelathini kwa sekunde, ukisababisha kupita kiasi kwa ujumbe na kulazimisha akili kuacha kila kitu kingine kinacho izunguka kitoweke. Hii ni kazi ya muangamizi.

Wale ambao hawawezi jitenga kutoka kwa hamu ya senema, TV soaps, vipindi vilivyo ratibiwa (serial programs) na kile kiitwacho uhalisia wa TV watapata karibu kutowezekana kusoma Bibilia kwa njia halisi bila kuwekwa wazi kwa uhalisia sambamba. Mbaya kabisa ya senema hizi ni zile zinamuonyesha Yesu mwenyewe. Kiwango cha mkanganyiko kinachojengwa kutoka kwa aina hii ya uhalisia sambamba, wachana na

kosa ambalo linadhihirishwa katika muswada na mtindo wa maisha ya watendaji wa kutamanisha kwa mara kwa mara, haiwezi kutabirika.

Unaweza fikiria kwamba vigezo hivi pekee vinaweza tosha, lakini pia nilikutana na matukio haya yenye uhalisia sambamba na michezo mbalimbali ya kompuyta kama vile kutafuta hazina (treasure hunting), jitihada (quest) au michezo ya kikazi (task based games) na hasa michezo ya mashindano ya gari (car racing games) ambayo ilihusisha kuvuka viwango ambavyo vingenifikisha kwenye uhalisia sambamba sawa na jinsi senema ingefanya. Baada ya kutumia saa nyingi katika kucheza, ningepata hisia hiyo ndogo ya kukanganyikiwa ni nini kilichokuwa halisi. Nakumbuka vizuri hisia baada ya kushinda mchezo na kukamilisha viwango vyake vyote. Nilishuhudia hisia ya kujivuna ambayo kisha ilitoa njia kwa huzuni ya jinsi fulani ambayo iliisha. Kanuni za masihara (principles of jest,[6]) ikiunganishwa na mafundisho ya visa vyenye misingi ya sinema, michezo na televisheni yalinivuta kutoka kwa uhalisia wangu uliokuwepo hadi kwa mwingine.

Hivi vikawa vyombo muhimu katika kumsaidia Mdanganyifu mkuu katika kunidumisha nje ya uzoefu wa Patakatifu pa Patakatifu na Mpendwa wangu. Vitu hivi vyote viliwekwa kugeuza uhalisia wa injili kuwa nyumba ya kadi iliyojengwa juu ya msingi wa mchanga. Kila sehemu ya malezi yangu ilikuwa imepigiwa hesabu kwa makini ili kuratibu mawazo yangu mbali na kile ambacho Mpendwa wangu alikuwa anajaribu kuniambia kwa haraka katika Bibilia.

[6]. Kanuni hizi za pale ambapo maana halisi ya maneno inadharauliwa na mara nyingi maana kinyume inapendelewa.

# 14. Nyumba ya Kadi



Nakumbuka moja ya wakati wa kwanza nuru ilinijia akilini mwangu, na kuanza kuona jinsi wanatheologia wanaweza toa kauli ya ajabu kama hiyo. Kwa miaka ilikuwa fumbo kwangu, jinsi wale ambao waliodai Bibilia wangekataa uumbaji kwa siku sita halisi, kukataa Sabbato au kuamini kwamba watu walienda mbinguni moja kwa moja walipokufa. Mbaya zaidi, zilikuwa kauli kutoka kwa wasomi wakikataa kazi ya Yesu katika Patakatifu pa Patakatifu na kusafishwa kutoka kwa dhambi kabla ya kurejea Duniani.

Nilikuwa nimeketi katika mhadhara juu ya kitabu cha Danieli na Ufunuo. Haikuwa imesemwa kama kweli lakini ilikuwa imependekezwa tu kwamba kile ambacho Danieli aliona katika maono katika sura ya 7 ilikuwa tashbihi. Tashbihi humaanisha:

> Umbo la usemi ambalo neno au kirai hutumika kwa kitu kingine ambacho **kihalisia hakihusiki** ili kupendekeza ufanano…[7]

Nilipopokea wazo hili la picha za Danieli 7 kuwa taashibi, nilihisi ardhi ikifunguka, na tukio lote la hukumu katika Danieli likiondolewa kabisa. Pendekezo lilikuwa kwamba Danieli na Ufunuo zilijaa mifano na kwamba kile ambacho Danieli aliona kuhusu Mwana wa Adamu akija kwa Mzee wa Siku pia kilikuwa mfano. Kulikuwa na mantiki katika hoja hii. Ilisikika kuwa na busara, lakini kutoka kwa utafiti ambao nilikuwa nimefanya, hili lingegeuza mafundisho ya hukumu na masomo yanayohusiana nayo (kutumia tashbihi) kuwa sitaha ya kadi juu ya msingi wa mchanga karibu na mstari wa mpasuko.

Matumizi ya tashbihi yanapatikana mahali kwingi katika Bibilia. Swali ni wakati upi wa kuchukulia kitu kama tashbihi ambapo maana haiwezi

---

[7]. Kamusi ya Kiswahili sanifu

kuchukuliwa kihalisia, na ni wakati gani tunasoma fungu wazi na maana halisi?

Kama tutakubali Bibilia kama Neno la Mungu basi tunapaswa kukubali kile ambacho inasema kihalisia kama kinaleta maana nzuri kama kinavyosimama na hakifanyi ukatili wowote kwa sheria rahisi za maumbile kama sivyo inaweza chukuliwa kimfano. Kwa mfano, Yesu anaposema "Mimi ndiye lango." Ni dhahiri huu ni mfano ambao unahitaji kutafsiriwa. Lango linafahamika kama sehemu ya kufikia kitu na kwa hivyo tunapambanua maana ya mfano huu.

Tashbihi inakuwa na nguvu tu wakati imefungwa kwa ukweli halisi. Kama ukiuchukua msingi huu na kutumia ufahamu wa kimfano kwao, basi mfumo wote utaharibika, kwa sababu hakuna chochote imara kwa tashbihi kujenga juu yake. Mtindo wa Bibilia wa kukubali maana halisi kwanza kama haileti madhara yoyote kwa kanuni rahisi za maumbile ni ulinzi wetu dhidi ya kugeuza misingi yetu kwa mchanga.

Athari asili ya kutumia tashbihi kwa kitu ambacho kinaweza eleweka kihalisia ni maana kinyume. Hila ndogo ya kutumia tashbihi kwa ufahamu halisi wa mafungu ulichochea furaha ya utoto wangu wote wa masihara na mafundisho vinyume kuvutia. Tashbihi hizi za mauti zilinipa lango la kuingia katika ukweli sambamba wenye maana tofauti. Nakumbuka mhadhiri mmoja akielezea jinsi Bibilia ilipata uhai alipofahamu nguvu za tashbihi.

Moja ya mifano rahisi ya jinsi tashbihi inaweza tumika kufanya kitu kuonekana kinyume cha kile ambacho kinatajwa ni kuhusu Sabato.

Bibilia inasema:

> Ikumbuke siku ya Sabato uitakase. Kutoka 20:8.

Tukichukua neno Sabbato na kulipa maana ya kupumzika, tunaweza onyesha jinsi Yesu anatupa pumziko kwa kunukuu:

> Njooni kwangu, ninyi nyote mnaotaabika na kulemewa na mizigo, nami nitawapumzisha. Mathayo 11:28.

Hitimisho inawasilishwa kwamba kama Yesu ni pumziko letu, anatimiza hitaji la kupumzika. Tunapumzika katika Kristo, na tunapopumzika katika yeye tunatimiza amri hii kiroho. Mchakato huu hugeuza neno halisi *Sabbato* kwa tashbihi ya kupumzika katika wokovu wa Yesu. Ila kama tukitumia mtindo wa tafsiri halisi kwanza tunapata kwamba inaleta maana kamili kama ilivyoandikwa, hivyo tunazuia maana ya kitashbihi ambayo itafanya kauli kuonekana kusema kinyume cha kile ambacho kiliamriwa.

Tukigeuka kwa Danieli 7 tunaingizwa kwa mifano mingi. Badala ya kudadisi kuhusu maana ya mifano hii, kuna kanuni nyingine muhimu na hiyo ni kwamba Bibilia inapaswa kujitafsiri yenyewe. Kama tukipokea Neno la Mungu kama mwalimu wetu basi lazima tunyenyekeshwe kwake badala yake kunyenyekeshwa kwa hamu yetu ya kuisoma kwa namna fulani.

Katika Danieli 7, hakuna haja ya kudadisi kuhusu maana ya Simba, Dubu, chui na mnyama, Bibilia inatwambia kile wanamaanisha.

> Wanyama hao wakubwa walio wanne ni wafalme wanne watakaotokea duniani. Daniel 7:17.

Kituo cha maono haya aliyopewa Danieli ni mtazamo wa hukumu kuu na umbo mbili kuu zinazoelezewa kama Mzee wa Siku na Mwana wa Adamu. Hapa kuna simulizi:

> Nikatazama hata viti vya enzi vikawekwa, na mmoja aliye mzee wa siku ameketi; mavazi yake yalikuwa meupe kama theluji, na nywele za kichwa chake kama sufu safi; kiti chake cha enzi kilikuwa miali ya moto, na gurudumu zake moto uwakao. (10) Mto kama wa moto ukatoka ukapita mbele zake; maelfu elfu wakamtumikia, na elfu kumi mara elfu kumi wakasimama mbele zake; hukumu ikawekwa, na vitabu vikafunuliwa. (11) Nikatazama wakati huo; kwa sababu ya sauti ya yale maneno makubwa iliyoyasema ile pembe; nalitazama hata mnyama yule akauawa, mwili wake ukaharibiwa, akatolewa ateketezwe kwa moto. (12) Na kwa habari za wale wanyama wengine, walinyang'anywa mamlaka yao; walakini maisha yao yalidumishwa kwa wakati na majira. (13) Nikaona katika njozi za usiku, na tazama, mmoja aliye mfano wa mwanadamu akaja pamoja

> na mawingu ya mbingu akamkaribia huyo mzee wa siku, wakamleta karibu naye. (14) Naye akapewa mamlaka, na utukufu, na ufalme, ili watu wa kabila zote, na taifa zote, na lugha zote, wamtumikie; mamlaka yake ni mamlaka ya milele, ambayo hayatapita kamwe, na ufalme wake ni ufalme usioweza kuangamizwa. Danieli 7:9-14.

Maelezo ya wanyama na pembe mdogo ni mifano wazi na yanapata maana yao katika sehemu zingine za sura hii na pia kwingine katika Danieli. Kila kitu kingine katika kisa hiki kinaweza somwa kihalisia bila uvunjanji wowote kutendeka kwa sheria za maumbile.

Eneo hili la hukumu inayohusisha Mzee wa Siku na Mwana wa Adamu ni simulizi ya msingi ya eneo la hukumu katika Danieli 7 ambayo inatendeka mwisho wa siku 2300 na kabla ya Marejeo ya Pili. Nikiwa nimeketi katika mhadhara wa Bibilia, pendekezo kwamba maono ya Danieli yalikuwa tu mfano wa haki ya Mungu na kuakisi uwezo wake wa kumaliza dhambi, ulifanya hali yote ya simulizi kuwa kinyume cha kile ilimaanisha. Kukosa kutumia kanuni ya kwanza ya kutafsiri, hufanya ukweli wa msingi wa Mwana wa Adamu kwa kweli kuja kwa Mzee wa Siku kupokea ufalme kugeuzwa kwa mavumbi. Mbona? Kwa sababu kwa kweli halikutendeka; ni mfano tu. Hili ndilo tokeo la kupuuza kanuni ya kutafsiri kihalisia kwanza.

Ni juu ya hoja hii hasa nilikuwa nimepotoshwa kuhusu fundisho la Bibilia la Baba na Mwanawe. Nashangazwa na jinsi ningeamini kwamba Yesu alikuwa Mwana wa Mungu na bado niamini katika Utatu kwa wakati uo huo. Mchakato huu unakuwa rahisi unapowasilisha istilahi *Baba* na *Mwana* kama tashbihi kwa upendo wa Mungu kwa ulimwengu.

Kama tukielewa kwamba ukweli dhabiti wa ulimwengu wote unamhusu Mungu na Mwanawe na kisha istilahi hizi zinafanywa tashbihi, uchumi wote wa Kikristo unakuwa nyumba ya kadi juu ya mchanga unaosogea.

Mara tu istilahi *Baba* na *Mwana* zitakapowacha kuwa na maana halisi, uti wa mgongo wa Maandiko unaweza furukutwa na kutengenezwa kulingana na kile tunataka uwe. Linakuwa jambo rahisi kumfanya Mungu kwa sura zetu. Dhana zima ya Mungu kuchukua majukumu kwa kutumia

istilahi Baba na Mwana kama mfano huwasilisha kwetu wazo kwamba mungu amejiumba kwa sura ya mwanadamu. Mungu, kama ilivyokuwa, anaingia kwa ukweli sambamba kutoa kauli yenye maadili. Maana ya kweli ya kauli zote zinazodhihirisha upendo wa Baba kwa Mwanawe hazifai kuchukuliwa kihalisia, kwa sababu kulingana na kanisa, Yesu kwa kweli sio Mwana wa Mungu; hili ni jukumu ambalo alichukua kwa madhumuni ya ukombozi.[8]

Ninapotazama nyuma juu ya maisha yangu na ninaona muunganiko wote wa masihara, senema, uhalisia sambamba, utambulisho uliobadilishwa na matumizi ya mafumbo ya mauti, pia ninaona kwamba vitu hivi vilikuwa vimeelekezwa kwa lengo moja muhimu, nalo lilikuwa kuangamiza uwezo wangu wa kuingia katika ushirika mzuri na Baba na Mwana katika Patakatifu pa Patakatifu pa mbinguni. Hadi nilipoanza kuelewa uongo huu na kuondoka kwao, haingewezekana kwangu kupata lango la kuingia Patakatifu pa Patakatifu na kuwa na Mpendwa wangu. Patakatifu pa Patakatifu ni pahali ambapo harusi hufanyika, na haingewezekana niwe sehemu ya bibi harusi kama kweli sikumjua Mume wangu mtarajiwa.

Njia pekee inayowezekana kuendeleza ushirika mzuri ni kujua ukweli kuhusu Mungu na Mwana kweli ni akina nani.

> Nao uzima wa milele ndio huu, wakujue Wewe uliye Mungu wa pekee, wa kweli na Yesu Kristo uliyemtuma. Yohana 17:3.
>
> Twawatangazia lile tuliloliona na kulisikia ili kwamba nanyi mwe na ushirika nasi na ushirika wetu hasa ni pamoja na Baba na Mwanawe Yesu Kristo. 1 Yohana 1:3.

Nilitaka ushirika huu pamoja na Baba na Mwana vibaya zaidi, hata ingawa maarifa yangu ya Yesu yalikuwa yamekanganywa na sauti na mafundisho

---

[8]. Itikadi nyingi za Kikristo hutoa wazo kwamba Yesu ni Mwana wa Mungu, lakini formyula ya watu wa tatu ndani ya Kiumbe mmoja huharibu tofauti ya kweli kati ya Baba na Mwana. Pili baadhi ya Wakristo humuona Yesu tu kama Mwana alipokuwa duniani. Hoja muhimu ni kwamba Mwana kwa kweli hakuwa wa pekee kutoka kwa Baba katika umilele hivyo kukanganya na kufanya siri Uwana wake

ya mshawishi. Mafundisho yangu katika senema, masihara na theologia ya mafumbo yaliniruhusu kuacha vitu hivi viwili vitenganishe mwendo wa wapenzi nami kama mtu mmoja. Kanuni ya kujitegemea, ilibadilisha utambulisho na kupokea heshima kupitia mafanikio ambapo kiumbe chenye hila kiliabudiwa katika uhalisia sambamba kwa Mkombozi mpole na mnyenyekevu wa ulimwengu. Mpendwa wangu hangeniruhusu kuingia ndani ya pahali pa siri pa Patakatifu pa Patakatifu nikiwa bado na upendo wa mpenzi wa utoto wangu. Lazima kungekuwa na njia ya kutoroka kutoka kwa vita hivi akilini mwangu.

## Kiingilio III

Wimbo Ulio Bora 5:7-9 Walinzi wazungukao mjini waliniona, Wakanipiga na kunitia jeraha, Walinzi walindao kuta zake Wakaninyang'anya shela yangu. (8) Nawasihi, enyi binti za Yerusalemu, Ninyi mkimwona mpendwa wangu, Ni nini mtakayomwambia? Ya kwamba nazimia kwa mapenzi. (9) Mpendwa wa namna gani ni mpendwa wako, Wewe uliye mzuri katika wanawake, Mpendwa wa namna gani ni mpendwa wako, Hata wewe utusihi hivyo?

Warumi 7:21-24 Hivyo naiona sheria ikitenda kazi. Ninapotaka kutenda jema, jambo baya liko papo hapo. (22) Kwa maana katika utu wangu wa ndani naifurahia sheria ya Mungu. (23) Lakini ninaona kuna sheria nyingine inayotenda kazi katika viungo vya mwili wangu inayopigana vita dhidi ya ile sheria ya akili yangu.Sheria hii inanifanya mateka wa ile sheria ya dhambi inayofanya kazi katika viungo vya mwili wangu. (24) Ole wangu, mimi maskini! Ni nani atakayeniokoa na mwili huu wa mauti?

Ufunuo 3:17-20 Kwa maana unasema, ‘Mimi ni tajiri, nimefanikiwa, wala sihitaji kitu cho chote.’ Hujui ya kwamba wewe ni mnyonge, wa kuhurumiwa, masikini, kipofu, tena uliye uchi. (18) Kwa hiyo nakushauri ununue kutoka Kwangu dhahabu iliyosafishwa kwa moto ili upate kuwa tajiri na mavazi meupe ili uyavae, upate kuficha aibu ya uchi wako na mafuta ya kupaka macho yako ili upate kuona. (19) Wale niwapendao, ninawakemea na kuwaadibisha. Hivyo uwe na bidii ukatubu. (20) Tazama, nasimama mlangoni nabisha. Kama mtu ye yote akisikia sauti Yangu na kufungua mlango, nitaingia ndani na kula pamoja naye, naye pamoja nami.

# Sehemu 4. Kuokolewa na Mpendwa Wangu

## 15. Eliya

Kama nilivyotaja katika Sura ya 9, wazo kwamba kweli Yesu alikuwa Mwana wa Mungu lilileta mtazamo wa kiumbe ambaye alipokea kila kitu kutoka kwa Baba yake na kwamba Baba yake alimpenda tu kwa sababu alikuwa Mwanawe na sio kwa karama ya nguvu na nafasi aliyokuwa nayo. Uhalisia huu ulifunua falme mbili wazi.[9]

| | **Ufalme wa Mungu** | **Ufalme wa Shetani/Ulimwengu** |
|---|---|---|
| Serikali | Familia | Wenye nguvu zaidi |
| Sarafu | Kupenda Mahusiano | Mali |
| Uraia | Wana wa Mungu | Utendaji na mafanikio kama unavyoyapima mwenyewe na wengine |

Licha ya ukweli kwamba nilikuwa nimesoma katika Sanaa ya masihara, mafumbo, na drama, ambayo kwa wakati huo iliniathiri zaidi kuacha usomaji halisi wa Bibilia na hamu ya kukimbilia ukweli mwingine, Neno la Mpendwa wangu kuhusu kile ambacho hutufanya kuwa wa thamani lilikuwa likikua polepole akilini mwangu. Nilianza kuona ukweli kwamba:

> Maana mawazo yangu si mawazo yenu, wala njia zenu si njia zangu; asema Bwana. (9) Kwa maana kama vile mbingu zilivyo juu sana kuliko nchi, kadhalika njia zangu zi juu sana kuliko njia zenu, na mawazo yangu kuliko mawazo yenu. Isaya 55:8-9.

---

[9] Tazama kitabu changu Vita vya Utambulisho sura ya nane kwa upanuzi wa falme hizi.

Bwana asema hivi, Mwenye hekima asijisifu kwa sababu ya hekima yake, wala mwenye nguvu asijisifu kwa sababu ya nguvu zake, wala tajiri asijisifu kwa sababu ya utajiri wake; (24) bali ajisifuye na ajisifu kwa sababu hii, ya kwamba ananifahamu mimi, na kunijua, ya kuwa mimi ni Bwana, nitendaye wema, na hukumu, na haki, katika nchi; maana mimi napendezwa na mambo hayo, asema Bwana. Jeremia 9:23-24.

Jiwe jipya la pembeni lilianza kudhihirisha mafundisho ambayo niliamini ndani yake nuru mpya kabisa.

| | **Ufalme wa Mungu** | **Ufalme wa Shetani/Ulimwengu** |
|---|---|---|
| Sheria | Karama ya ulinzi | Kifaa cha kuonyesha matendo mema |
| Sabbato | Karama yenye Baraka ya kuwa na muda pamoja | Wakati wa kujiliwaza kutoka kwa kazi ngumu au kifaa cha kuonyesha haki |
| Hukumu | Wakati wa kusongea karibu na Mungu, kuamini neema yake | Wakati wa kufanya bidii zaidi kutengeneza gradi |

Kuanza kwa mtazamo wangu kwamba Yesu alirithi vitu vyote kama karama ya upendo na Baraka kulisababisha kukua kwa ufahamu kwamba mafundisho mengi pia ni karama ya upendo kutoka kwa Baba kupitia kwa Kristo. Uwezo wa kuitunza sheria na Sabbato au kuikabili hukumu hautoki ndani bali juu. Hata hivyo kiakili nilifahamu hili awali, nilikuwa nimeshikilia Kristo kama Mkombozi wa maisha yangu, na kwa hivyo pasipo kujua nikaamua kwa mbinu hiyo ya kukabiliana na sheria, Sabbato na hukumu. Lakini kila wakati ningetafakari maneno haya: Nayo sauti kutoka mbinguni ikasema, "Huyu ni Mwanangu mpendwa, ambaye ninapendezwa sana naye.'' (Mathayo 3:17) ndivyo ningeweza kuona kwamba uwezo wa kufanya kile ambacho Mungu alihitaji ulitoka kwake kama karama.

Niliposonga kutoka kwenye fundisho la Bibilia hadi fundisho la Bibilia niliona upendo wa Baba kwangu kupitia kwa Mwanawe.

Siku moja wazo lilinigonga. *Vipi kuhusu Utatu? Hatuwezi Kusoma Maandiko katika nuru ya kile umejifunza kuhusu falme hizo mbili?* Wazo lilinijia mara moja. *Hautaki kuenda pale!* Kisha wazo lingine lilipenyeza zaidi — *Mkristo anaweza kataa wito wa kusoma maandiko kuthibitisha vitu vyote?* Ukweli hasa kwamba nilihisi hofu ya kuchunguza mada hii uliniambia kwamba nilihitaji kulisoma. Nilijua kwamba imani yoyote iliyofanya kuwadia kwa hofu haikuwa mwamba imara. Hivyo nilianza kuchunguza swala hilo.

Kwa sababu kadha maneno ya Yohana 5:26 yaliniingilia.

> Kama vile Baba alivyo na uzima ndani Yake, vivyo hivyo amempa Mwana kuwa na uzima ndani Yake; John 5:26.

Sikuwa nimeweza kusoma fungu hili kihalisia kabla kwa sababu kufanya hivyo kungeharibu kanuni ya kujitegemea. Kama kujitegemea ni kiini cha uungu basi haingewezekana kusoma fungu hili kama kumaanisha kwamba Baba alimtoa Mwanawe kuwa na uzima ndani yake, kupendekeza uzima wa kujitegemea. Sasa ilikuwa rahisi sana kusoma wazi. Sababu ya pili ningeamini kwamba Mungu alimtoa Mwanawe kwa sababu thamani ya Kristo kama Mwana Mtakatifu haikuwepo katika sifa alizorithi bali katika uhusiano wake na Baba yake. Nuru hii ya ghafla iliweka wazi kikamilifu muunganisho wa uongo wa Yesu ambao nilikuwa nao akilini kwa muda mrefu. Ghafla Kristo wa uongo ambaye alikuwa amehubiriwa kwangu, kupendwa nami na kuabudiwa nami aliwekwa wazi. Kristo hakuwa kielelezo cha kujitegemea kabisa, alikuwa Mwana ambaye alimpenda Baba na kupokea kila kitu kutoka kwake.

Ghafla mafungu kila mahali yalipasuka kwa nuru.

> Hakuna mtu ye yote aliyemwona Mungu wakati wo wote, ila ni Mungu Mwana pekee, aliye kifuani mwa Baba ndiye ambaye amemdhihirisha. Yohana 1:18.

Nao uzima wa milele ndio huu, wakujue Wewe uliye Mungu wa pekee, wa kweli na Yesu Kristo uliyemtuma. Yohana 17:3.

kwa kuwa maneno yale ulionipa nimewapa wao, nao wameyapokea na kujua kwamba kweli nimetoka Kwako, nao wameamini kuwa Wewe ulinituma. Yohana 17:8.

Mwanzo wa Injili ya Yesu Kristo, Mwana wa Mungu. Marko 1:1.

Lakini kwetu sisi yuko Mungu mmoja, aliye Baba, ambaye vitu vyote vyatoka Kwake na kwa ajili Yake sisi twaishi na kuna Bwana mmoja tu, Yesu Kristo, ambaye kwa Yeye vitu vyote vimekuwepo na kwa Yeye sisi tunaishi. 1 Wakorintho 8:6.

Simoni Petro akamjibu, "Wewe ndiwe Kristo a, Mwana wa Mungu aliye hai. (17) Naye Yesu akamwambia, ''Heri wewe, Simoni mwana wa Yona, kwa maana hili halikufunuliwa kwako na mwanadamu, bali na Baba yangu aliye mbinguni. Mathayo 16:16-17.

Bwana alikuwa nami katika mwanzo wa njia yake, Kabla ya matendo yake ya kale. (23) Nalitukuka tokea milele, tangu awali, Kabla haijawako dunia. (24) Wakati visipokuwako vilindi nalizaliwa, Wakati zisipokuwako chemchemi zilizojaa maji. Methali 8:22-24.

Zamani Mungu alisema na baba zetu kwa njia ya manabii mara nyingi na kwa njia mbalimbali, (29) lakini katika siku hizi za mwisho amesema nasi kwa njia ya Mwanawe, ambaye amemweka kuwa mrithi wa vitu vyote, ambaye kwa Yeye aliuumba ulimwengu. (3) Mwana ni mng'ao wa utukufu wa Mungu na mfano halisi wa nafsi Yake, akivihifadhi vitu vyote kwa neno Lake lenye uweza. Akiisha kufanya utakaso kwa ajili ya dhambi aliketi mkono wa kuume wa Ukuu huko mbinguni. (4) Kwa hiyo alifanyika bora kuliko malaika kama Jina alilorithi lilivyo bora kuliko lao. Waebrania 1:1-4.

Ikiwashwa na maneno yaliyotangazwa katika ubatizo wa Kristo na kuzushwa na umuhimu wa vita na Shetani juu ya Uwana wake, akili yangu ililipuka kwa kasi ya kuunganisha mapengo ya Bibilia ambayo yalianza kudhihirisha ukweli kwa uwazi kabisa. Mitiririko kadhaa ya mawazo

iliungana na kuja kupumzika juu ya ukweli huo mmoja na ukweli pekee wa jiwe la pembeni la Mwana wa pekee ukichochewa na maneno yaliyonenwa katika ubatizo wa Kristo na kuzushwa na–Mwana mbarikiwa, Mwana ambaye Mungu anapendezwa naye, Mwana ambaye Baba alipeana kila kitu alichokuwa nacho kwake, Mwana wa kuamini, kupenda utiifu kwa mamlaka mema ya Babaye. Nilihisi kama Isaac Newton akishika ukweli muhimu wa tufaha ikianguka ardhini.

Kwa ukamilifu wa kipindi cha wakati huo, nakumbuka wazi nikiinua kichwa changu kwelekea mbinguni na kulia kama wanafunzi:

> Kitu cha kwanza Andrea alichofanya ni kumtafuta Simoni nduguye na kumwambia, Tumemwona Masiya (yaani, Kristo). Yohana 1:41

Machozi yalitiririka kutoka machoni mwangu nilipofika kwa kushika ukweli kwamba nilikuwa nimempata! Ukweli ni kwamba alinipata, na jinsi nilikuwa na furaha kupatikana. Mwana wa pekee wa Mungu alisimama mbele yangu kama Mwamba mkuu, na niliamua hapo na hapo kujenga nyumba yangu juu ya jiwe hili la thamani la pembeni. Ukungu wa mjaribu ambao ulikuwa umemfunga Mpendwa wangu na kumzuia kutoka kwangu uliondolewa na mwanga tukufu wa Mwana huyu wa urithi. Sauti ya Eliya iliita kwa ndani katika moyo wangu:

> Angalieni, nitawapelekea Eliya nabii, kabla haijaja siku ile ya Bwana, iliyo kuu na kuogofya. (6) Naye ataigeuza mioyo ya baba iwaelekee watoto wao, na mioyo ya watoto iwaelekee baba zao, ili nisije nikaipiga dunia kwa laana. Malaki 4:5-6.

Hakika roho wa Eliya alikuwa amekuja na kuugeuza moyo wangu kwelekea kwa Baba na Mwanawe. Hamu yangu ya kutafuta uhuru kutoka kwa vipimo visivyokuwa na mwisho na matendo ilipata hitimisho katika Mwana wa pekee wa Baba ambaye husimama mbele yake kama furaha yake bila kutegemea nguvu, hekima au utajiri, bali tu neno lake lenye baraka ya kukubalika, upendo na furaha.

Kama tabia ya kweli na mtu wa Mpendwa wangu nilichukua sura katika nuru ya agano wazi la Andiko, hivyo kukuza hisia ya haya kutoka kwa utambuzi wa upendo wangu na uhusiano haramu na undanganyifu wa

kujitegemea ambao ulikuwa unanivutia maisha yangu yote. Kushikwa katika kushikilia ujenzi wa tatu katika moja uitwao Utatu, nilikuwa nimemchagua Barabba dhidi ya Mpendwa wangu bila kujua. Nilichukua haya ya kuuma ya ibada ya sanamu hii kwa Baba yetu na kuomba msamaha kupitia kwa damu iliyomwagika ya Mpendwa wangu. Amani, furaha na upendo viliujaza moyo wangu, ingawa nilivutiwa kukumbuka nilipokuwa nimetoka ili kwamba niwe mwenye fadhili kwa wengine ambao wamepitia hatma sawa nami.

Siku hizo nilihisi kama hisia za upendo wangu wa Kwanza kwote niliposimama mbele ya madhabahu ya kafara na kumtazama Mpendwa wangu akifa pale kwa ajili yangu. Sasa muktadha wa kafara hiyo uliwasilishwa kwangu kama karama ya kweli ya Baba ya kuwarejesha watoto wake wapotovu. Uzoefu wangu wa kujifunza katika Patakatifu na taa na mikate ikiunganishwa na uombezi ulioendelea wa Mpendwa wangu ilimwandalia Eliya njia ili kutengeneza njia nyoofu kwa miguu yangu na kupata kumbatio la upendo la Mpendwa wangu.

Nilitamani kuingia Patakatifu pa Patakatifu na Mpendwa wangu lakini kulikuwa na vikwazo vingi ambavyo vilihitaji kuondolewa na ufahamu zaidi wa kiwango ambacho ibada yangu ya sanamu ilikuwa imeniathiri.

> Bwana, ni nani atakayekaa Katika hema yako? Ni nani atakayefanya maskani yake Katika kilima chako kitakatifu? (2) Ni mtu aendaye kwa ukamilifu, Na kutenda haki. Asemaye kweli kwa moyo wake, (3) Asiyesingizia kwa ulimi wake. Wala hakumtenda mwenziwe mabaya, Wala hakumsengenya jirani yake. (4) Machoni pake mtu asiyefaa hudharauliwa, Bali huwaheshimu wamchao Bwana Ingawa ameapa kwa hasara yake, Hayabadili maneno yake. (5) Hakutoa fedha yake apate kula riba, Hakutwaa rushwa amwangamize asiye na hatia. Mtu atendaye mambo hayo Hataondoshwa milele. Zaburi 15:1-5.

Kwa miaka mingi nilikuwa nimejaribu kujenga nyumba yangu juu ya Mpendwa wangu na pia juu ya jaribio la kujitegemea. Kulikuwa na mbao na mabua katika msingi wangu ambayo yalihitaji kusafishwa ili niweze kutembea wima, kutenda haki na kunena ukweli moyoni mwangu.

Majaribu haya yangekuwa kutimizwa asili kwa hiari yangu ya kukiri upendo wangu kwa Mpendwa wangu mbele ya ndugu zangu. Ila kabla ya kushiriki nanyi baadhi ya majaribu haya, nataka kushiriki nanyi baadhi ya sababu mbona nafurahia katika Mpendwa wangu.

## 16. Vyote kwa Pamoja Vinapendeza

> Mpendwa wangu ni mweupe, tena mwekundu, Mashuhuri miongoni mwa elfu kumi; (11) Kichwa chake ni kama dhahabu safi sana, Nywele zake ni za ukoka, nyeusi kama kunguru; (12) Macho yake ni kama hua penye vijito, Wakioga kwa maziwa, wakiikalia mito iliyojaa; (13) Mashavu yake ni kama matuta ya rihani, Ambayo hufanyizwa manukato; Midomo yake ni kama nyinyoro, Inadondoza matone ya manemane; (14) Mikono yake ni kama mianzi ya dhahabu, lliyopambwa kwa zabarajadi; Kiwiliwili chake kama kazi ya pembe, Iliyonakishiwa kwa yakuti samawi; (15) Miguu yake ni kama nguzo za marimari, Zilizowekwa juu ya misingi ya dhahabu; Sura yake ni kama Lebanoni, Ni bora mfano wa mierezi; (16) Kinywa chake kimejaa maneno matamu, Ndiye mzuri sana pia pia. Ni huyu mpendwa wangu, ni huyu rafiki yangu, Enyi binti za Yerusalemu. Wimbo Ulio Bora 5:10-16.

Inakuja kama mshangao kufikiria kwamba haiwezekani kwa Mungu Baba yetu kuumba ulimwengu moja kwa moja. Samahani? Mungu anaweza fanya chochote, jibu linakuja. Sheria ya uzima wa ulimwengu inaamrisha kwamba yule ambaye anatupa uzima moja kwa moja, ndiye ambaye tunatamani kuwa kama yeye.

> Nasi sote, tukiwa na nyuso zisizotiwa utaji tunaakisi utukufu wa Bwana, kama kwenye kioo. Nasi tunabadilishwa ili tufanane naye, toka utukufu hadi utukufu mkuu zaidi, utokao kwa Bwana, ambaye ndiye Roho. 2 Wakorintho 3:18.

Kama serikali ya ulimwengu ilimtegemea Baba, nini kingekuwa tokeo? Viumbe wote wa malaika na sayari zote zilizoumbwa zingetafuta kumuiga Baba. Ndio, tunaweza tafuta kuwa kama yeye katika tabia, lakini katika kiwango cha kina cha kutaka kuwa kama yeye, tutajikwaa na kuanguka. Jinsi gani hivyo? Baba hamtii yeyote wala hafundishwi au kupewa maagizo na yeyote.

> Tazama jinsi kilivyo kina cha utajiri wa hekima na maarifa ya Mungu! Tazama jinsi ambavyo hukumu Zake, hazichunguziki na ambavyo njia Zake zisivyotafutikana! (34) Ni nani aliyeijua nia ya Bwana? Au ni nani ambaye amekuwa mshauri Wake? (35) Au ni nani aliyempa cho chote ili arudishiwe? (36) Kwa maana vitu vyote

> vyatoka Kwake, viko Kwake na kwa ajili Yake. Utukufu ni Wake milele. Amen. Warumi 11:33-36.

Kama Baba angewasilishwa kwetu kama jiwe la pembeni la jinsi ya kuishi, tungetafuta kuwa kama yeye na kuwa yule ambaye hatii au kupokea ushauri. Katika jitihada zetu za kuwa kama yeye, kiasilia tutakuwa kinyume na hili limedhibitishwa katika maisha ya Shetani ambaye alitafuta kuwa kama Aliye Juu.

Suluhisho kwa hili lilikuwa Baba aweke jiwe la pembeni kuwa msingi wa ulimwengu ambapo atajenga juu yake—Moja ambalo ulimwengu wote utalitazama kama mfano wa jinsi ya kuishi.

> kwa ajili ya hayo Bwana, MUNGU, asema hivi, Tazama, naweka jiwe katika Sayuni, liwe msingi, jiwe lililojaribiwa, jiwe la pembeni lenye thamani, msingi ulio imara; yeye aaminiye hatafanya haraka. Isaya 28:16.

Katika hekima isio mfano, Mungu alimzaa Mwanawe katika mfano wake wa moja kwa moja. Ni mawazo ya Mungu yalifanywa kusikika. Ukamilifu wote wa uungu wa Baba ulikaa ndani yake. Aliwekwa kuwa na uzima ndani yake kama Baba alivyo.

> Bwana alikuwa nami katika mwanzo wa njia yake, Kabla ya matendo yake ya kale. (23) Nalitukuka tokea milele, tangu awali, Kabla haijawako dunia. (24) Wakati visipokuwako vilindi nalizaliwa, Wakati zisipokuwako chemchemi zilizojaa maji. Methali 8:22-24.

Ingawa Mwana wa Mungu alimiliki uwezo wote wa Baba yake, bado tunagundua kwake:

> Yesu akawaambia, Amin, amin nawaambia, Mwana hawezi kufanya jambo lo lote peke yake, Yeye aweza tu kufanya lile analomwona Baba yake akifanya, kwa maana lo lote afanyalo Baba, Mwana pia hufanya hivyo hivyo. Yohana 5:19.

Ukweli kwamba Mwana wa Mungu anaweza mtazama Baba yake katika utiifu, akipenda kutii bila hamu ya kuiga nafasi yake ni moja ya ushahidi wa juu wa uungu wake. Kama Mwana angekuwa kiumbe wa kuumbwa na

hakuna mfano mwingine mtiifu wa kufuata, kiasilia angetafuta kuwa kama Aliye Juu katika uwezo na nafasi na pia vile vile kitabia. Ibada yake ya milele kwa Baba yake ni ushahidi wa kutosha kwamba ni wazo la Mungu likifanywa kusikika na kuwa utimilifu wote wa Baba unakaa ndani yake.

Juu ya jiwe hili la pembeni, Mungu angejenga ulimwengu. Kila kiumbe ambacho kilitoka katika mikono ya Mwanawe, kingejazwa na roho sawa wa utiifu na kuamini kama yule ambaye aliwaumba.

> Lakini tukiondoka kutoka kwa uwasilisho mdogo, tunamuona Mungu katika Yesu. Tukimtazama Yesu tunaona kwamba ni utukufu wa Mungu wetu kupeana. "Mimi sitendi jambo lo lote peke Yangu," Alisema Kristo; "Baba aliye hai amenituma Mimi, nami ninaishi kwa sababu ya Baba." "Mimi sitafuti utukufu Wangu mwenyewe," Lakini utukufu wa yule aliyenituma. Yohana 8:28; 6:57; 8:50; 7:18. Katika maneno haya kunatolewa kanuni kuu ambayo ni sheria ya uzima kwa ulimwengu. Vitu vyote Kristo alipokea kutoka kwa Mungu, lakini alichukua ili kupeana. Hivyo katika mahakama ya Mbinguni, katika Huduma yake kwa viumbe vyote vilivyoumbwa: kupitia kwa Mwana mpendwa, uzima wa Baba hutiririka kwa vyote; kupitia kwa Mwana hurejea, katika sifa na huduma ya furaha, wimbi la upendo, chanzo kikuu cha vyote. Na kwa hivyo kupitia kwa Kristo mzunguko wa wema unakamilika, ukiwasilisha tabia ya Mpaji mkuu, sheria ya uzima. *Desire of Ages*, page 21.

Mwana wa pekee ni ufunguo wa ulimwengu wote ukishikamanishwa pamoja. Ni roho wa utiifu na uaminifu wa Mwana ambaye Baba hutuma mioyoni mwa viumbe vyote vilivyoumbwa.

> Maana kwa ajili yetu mtoto amezaliwa, Tumepewa mtoto mwanamume; Na uweza wa kifalme utakuwa begani mwake; Naye ataitwa Jina Lake, Mshauri wa ajabu, Mungu mwenye nguvu, Baba wa milele, Mfalme wa amani. Isaya 9:6.
>
> Kwa sababu ninyi ni watoto wa Mungu, Mungu amemtuma Roho wa Mwanawe mioyoni mwetu, anayelia, Abbaa! Yaani, Baba. Wagalatia 4:6.

Ni Roho wa Mwana wa pekee ndiye ambaye hugeuza mioyo ya viumbe vyote kwelekea kwa Baba ambaye ni chanzo kikuu cha vyote. Ni imani yake katika Baba yake ambayo ni chemchemi ya imani yangu katika Baba. Kama alivyo mtakatifu na mwenye haki katika Baba yake, tunafuata mfano wa imani hii ya Yesu na inakuwa imani yetu. Hili ni jambo moja la thamani zaidi kumhusu Mpendwa wangu. Tabia yake ni moja ya uaminifu wa kupenda kutii kwa Baba.

Ninapomruhusu Mpendwa wangu kuyatawala maisha yangu, ninavutwa kwa Baba. Nahisi hitaji langu kwake la daima. Hivi vyote ni hazina, karama kutoka kwa Mpendwa wangu. Hii ndio maana Baba anamkweza Mwanawe na anampa jina juu ya majina yote. Hii ndio sababu Mpendwa wangu ni Baba wa milele kwa wale ambao wanamtii Mungu mmoja wa kweli. Haya ni maji ya uzima ambayo anatupa tunywe. Katika maji hayo kuna Roho wa imani ambayo humwamini Baba katika hali zote na ni Roho wa imani ambaye hushikamanisha ulimwengu wote pamoja kwa Mungu.

> Yeye ni mfano wa Mungu asiyeonekana, mzaliwa wa kwanza wa viumbe vyote. (16) Kwa Yeye vitu vyote vilivyoko mbinguni na juu ya nchi viliumbwa, vile vitu vinavyoonekana na vile visivyoonekana, kama ni viti vya enzi au falme, au wenye mamlaka au watawala, vitu vyote viliumbwa na Yeye na kwa ajili Yake. (17) Yeye alikuwapo kabla ya vitu vyote na katika Yeye vitu vyote vinashikamana pamoja. (18) Yeye ndiye kichwa cha mwili, yaani, Kanisa, naye ni wa mwanzo na mzaliwa wa kwanza kutoka kwa wafu, ili Yeye awe mkuu katika vitu vyote. (19) Kwa kuwa ilimpendeza Mungu kwamba ukamilifu Wake wote wa kimungu uwe ndani Yake; Wakolosai 1:15-19.

Ninapotafakari juu ya vitu hivi, moyo wangu unachangamka na siwezi saidia ila kutabasamu. Hazina ya Mpendwa wangu ni tamu. Huuhifadhi moyo wangu salama ukiamini katika Baba yake na kunijaza na ridhaa na amani.

Hazina nyingine ambayo nimepata katika Mpendwa wangu ni baraka zake. Baba amembariki Mwanawe na moyoni mwa Mpendwa wangu mna dumu uhakika kwamba Baba anapendezwa naye. Ni kiasi gani atakuwa tayari kulipia roho huyu wa kupumzika katika kupendezwa kwa Baba?

> Nayo sauti kutoka mbinguni ikasema, Huyu ni Mwanangu mpendwa, ambaye ninapendezwa sana naye. Mathayo 3:17.

Kupendezwa kwa Baba kuna kuwa kwangu kupitia kwa kuchumbiana kwangu na Mwanawe.

> Kwa hiyo tunamsifu Mungu kwa huruma zake kuu alizotumiminia kwa sababu sisi ni wa Mwanae Mpendwa. Waefeso 1:6.

Sihitaji kujitahidi, wala kutimiza, wala kuonyesha kwa Baba chochote ili kupata idhini yake. Katika kuwa na Mpendwa wangu, ninakupendezwa kwa Baba. Ninahisi upendo wa Baba kwa Mwanawe moyoni mwangu.

Oh mwana wa Adamu, ni jinsi gani ninajipata nikipendwa namna hiyo? Hakuna maneno ambayo yanaweza tolewa kuelezea hisia za moyo wangu. Baba anapendezwa nami! Ndio, anapendezwa nami, na nimekubalika kwake kwa sababu Mwanawe amekubalika kwake.

Swali linaulizwa:

> Mpendwa wa namna gani ni mpendwa wako, Wewe uliye mzuri katika wanawake, Mpendwa wa namna gani ni mpendwa wako, Hata wewe utusihi hivyo? Wimbo Ulio Bora 5:9.

Mpendwa wangu ni zaidi ya mwingine yeyote kwa sababu anashiriki nami kupendezwa kwa Baba katika yeye. Mpendwa wangu wa utotoni hangenipa hazina hii. Angeniahidi tu uhuru wa kufanya chochote kilichonipendeza bila kipimo, ila hivi vyote vimedhibitishwa kuwa uongo. Hana hazina yoyote kabisa, na mungu ambaye ananiwasilishia ni mgumu kama mchanga wa kuhama wa jangwani.

> Like the woman at the well I was seeking for things that could not satisfy and then I heard my Saviour speaking "draw from My well that never shall run dry."[10]

Katika vitu hivi viwili napata hazina tamu kabisa katika Mpendwa wangu. Cha kwanza ni roho wa kutii na kuamini ambaye huja kama urithi asili kwa

[10] Kutoka kwa wimbo "Fill my cup Lord" wa Richard Blanchard

yule ambaye ni wa pekee. Cha pili ni kupendezwa na kubarikiwa kwa Baba juu ya Mwanawe ambako Mwanawe hushiriki nami. Hili pia ni tokeo asili la urithi wake kutoka kwa Baba. Siri ya hazina hizi zote inakaa katika urithi wa Mpendwa wangu kutoka kwa Baba kama Mwanawe wa pekee tangu umilele.

Ni gharama gani unaweza weka katika hazina hizi? Zina thamani zaidi ya dhahabu na fedha zote ulimwenguni. Hii ni lulu ya bei kuu. Haustahili kuuza vyote ili kumpata?

> Umenizingira nyuma na mbele, Ukaniwekea mkono wako. (6) Maarifa hayo ni ya ajabu, yanishinda mimi, Hayadirikiki, siwezi kuyafikia. (7) Niende wapi nijiepushe na roho yako? Niende wapi niukimbie uso wako? Zaburi 139:5-7.

> Kinywa chake kimejaa maneno matamu, Ndiye mzuri sana pia. Ni huyu mpendwa wangu, ni huyu rafiki yangu, Enyi binti za Yerusalemu. Wimbo Ulio Bora 5:16.

## 17. Moto Usafishao

Mtu anapokuwa katika upendo, haiwezekani kuficha. Hata hivyo nilifahamu kwamba kushiriki mawazo yangu kuhusu Mpendwa wangu na kanisa langu kungekuwa na athari kubwa, ila kukosa kushiriki habari hii ya Mpendwa wangu ilikuwa na athari kubwa zaidi.

> Kila mtu atakayenikiri mbele ya watu, mimi nami nitamkiri yeye mbele za Baba yangu aliye mbinguni. (33) Lakini ye yote atakayenikana mimi mbele ya watu, mimi nami nitamkana mbele ya Baba yangu aliye mbinguni. Mathayo 10:32,33.

Nilikuwa nimevutiwa kiasi ya kwamba nilitaka kuwasilisha utafiti wangu kwa kanisa langu kwa upendo na pia kujaribu kama kuna uwezekano kwamba nilikuwa nimekosea kitu. Kuna wakati ambao mshawishi angenishawishi na maneno "Unadhani wewe ni nani kuchukua nafasi hii? Hakuna watu wanao ongoza au hata wasio ongoza wanao amini kwa Mwana huyu wa Mungu unaye abudu. Je, kama umekosea kitu? Je, kama yote ni kosa?"

Nahitaji kuruhusu ufahamu wangu utiwe katika changamoto kupitia kwa mchakato wa kutii wazee wangu. Nahitaji kusikiliza kile ambacho watasema na kukilinganisha na maandiko, kisha nitafute dhamiri yangu kama bado nitampenda Mpendwa wangu au kama alikuwa hazina tu katika akili zangu. Nilitaka kuwa na uhakika. Uzoefu wa mwanadamu uko katika hatari ya majaribu mengi na kasoro nyingi.

Nilikuwa na uaminifu kwamba mawazo haya yalitoka kwa Mpendwa wangu. Alijua kwamba nilikuwa nikiutia mguu wangu katika njia ambayo watu wachache husafiri. Nilihitaji kujaribiwa kama kweli nilikuwa tayari kutembea naye katika bonde hili la giza la kutengwa, kutofahamika na ubishi.

Nilichukua matokeo ya utafiti wangu kwa wazee wa kanisa na kuwaomba wayachunguze. Nakumbuka siku hiyo vyema; ilikuwa siku kabla ya siku yangu ya kuzaliwa mwaka wa arobaini. Nilikuwa nimehudumia Utatu kwa miaka arobaini, na katika kutii vitu hivi nilikuwa nikitakazama upendo na

hisia zangu kwa Mpendwa wangu. Alifaa tokeo langu kujiweka wazi kwa ndugu zangu.

Muda mfupi baadaye, nilipokea neno kwamba vyanzo vingine vilikuwa vikiripoti ya kwamba nilikuwa nimekataa Utatu na baadhi ya ripoti ziliashiria kwamba sikumwamini Roho mtakatifu tena. Baadhi waliwakaribia rafiki zangu na kuwafahamisha kuhusu "uasi" wangu. Nilihisi kuvunjika kabisa. Niliwapenda rafiki zangu, ila kujaribu kuwaelezea ingeonekana kana kwamba najaribu kudunisha kanisa. Niliwaambia wachache wa rafiki zangu wa karibu na kuwaelezea hali. Rafiki wengine wawili au watatu walinipigia simu ili kujua kilichokuwa kikiendelea.

Hili lilikuwa jaribu la kweli kwangu. Nilijua kwamba ripoti za uongo zilikuwa zikizunguka kuhusu imani yangu na nia yangu, ila singewapigia simu rafiki zangu niwaelezee kilichokuwa kikitendeka. Nillipiga magoti mbele za Mungu na kusema, "Rafiki zangu wote nakukabidhi, na kama kweli ni rafiki zangu watanitafuta wakati mmoja katika siku zijazo." Ilibidi niombe ombi hili mara nyingi hasa nilipopokea ripoti za kauli zinazoonekana kuwa dhidi yangu.

Polepole lakini kwa uhakika, ilikuja kuonekana kwamba sifa zangu na msimamo wangu kanisani zilikuwa zimesiagika. Kimya kilikata kwa kina moyoni mwangu. Kadri siku baada ya siku zilivyosonga bila neno, mtagusano au uchunguzi, nilikuwa na wakati wa kutafakari gharama ya kuwa na uhusiano na Mwana wa Mungu. Tena ningetafakari, *na je, kama umekosea?* Nilienda kwa Maandiko, na kuamini kulirejea kukiwa dhabiti zaidi kuliko awali. Najua hili ni sawa, ushahidi unatosha. Dhamiri yangu ilishika upesi kile ambacho Bibilia ilifundisha wazi. Nilijua kwamba ningepata furaha tu kwa kufuata dhamiri zangu na kutenda yale ambayo nilikuwa nimeamini kuwa sawa.

Chini ya miezi kumi na miwili tu niliwasilisha matokeo ya utafiti wangu, nilipokea majibu. Swali kuu ambalo niliulizwa lilihusiana na kama niliamini kwamba kuna wakati ambao Mwana hakuwepo. Nilijibu, kwamba Bibilia inatwambia kwamba Yesu ni wa pekee na pia wa milele. Nakubali yote

kuwa kweli; sitafuti kupenya katika siri ya umilele ili kukataa uwazi wa urithi wa Mwana wa Mungu.

Nilipopokea majibu rasmi ya wasilisho langu, niliambiwa kwamba kamati haikupata nuru katika mapendekezo yangu. Nilipereleza majibu yao kwa marejeleo yoyote ya Bibilia ambayo ningesoma na kufikiria kuyahusu. Sikupata hata fungu moja la Bibilia, hakuna nukuu kutoka kwa maandishi kuonyesha ambayo naweza kuwa nimekosea, matangazo tu kuhusu matokeo yangu.

Nilikuwa nimeweka moyo wangu tayari kikamilifu kusoma mwongozo wowote wa Bibilia ambao ulikuwa umetolewa kwangu, ila hakukuwa chochote, hakukuwa chochote kabisa. Ingawa sikuwa sijui kile ambacho kingewezekana, kama kuzaliwa kwa mtoto, tukio lilipofika, liligonga kwa nguvu zaidi. Nilihisi hisia kadha zote zikija kwa pamoja moyoni mwangu. Niliomba amani, neema na upendo moyoni mwangu. Hatimaye amani ilinijia na furaha ya Mpendwa wangu ilirejea. Niliomba "Baba, niko tayari kusoma chochote kutoka kwenye Bibilia ambacho wale walio kwenye utawala watanipa, lakini kama nimefanya kosa, jibu lazima litoke kwenye Bibilia."

Tena swali lilinijia mawazoni mwangu, na je, kama yote ni makosa, na kama umekosea? Niliwaza kuhusu wakati wangu katika huduma na kupoteza uhusiano wangu na washirikaj wangu wa awali. Sehemu yangu ilitaka tu kusahau kile ambacho nilikuwa nikisoma katika Bibilia na kukubali kwamba nilikuwa nimekosea. Ila, nilijua kwamba hii haikuwa njia ya uhuru. Singemkataa Mpendwa wangu. Alienda msalabani kwa hiari kwa ajili yangu. Alikabiliana na mambo ya kufedhehesha mno, ya aibu sana kwa ajili yangu, siwezi vumilia fedheha kidogo kwa ajili yake?

Nilichukua muda kutafakari na kuomba. Niliwaandikia tena waze wa kanisa nikiwaomba majibu ya bibilia kwa kazi yangu. Niliomba bila kukoma roho wa fadhili na utiifu. Niliomba kwamba nisiandike kwa njia yoyote itakayosababisha chukizo.

Uzoefu wangu wa kilele cha mlima wa kumpata Mpendwa wangu, sasa uliwasilisha uhalisia wa kurejea kwangu kuzuri katika bonde la maisha.

> Kisha alianza kwenda mbele; lakini Makini, Ucha Mungu, Upendo, na Busara waliandamana naye akiteremka hadi chini ya kilima. Hivyo walienda wote pamoja, wakielezea mjadala wao wa awali, hadi walipofika chini ya kilima. Kisha akasema Mkristo, kama ilivyokuwa vigumu kukwea, kadri nionavyo, ni hatari kuteremka. Ndio, alisema Makini, ndivyo ilivyo, kwa kuwa ni suala ngumu kwa mtu kuteremka katika bonde la udhalilishaji, kama tulivyo sasa, na kukosa kukutana na utelezi wowote njiani; kwa hivyo, walisema wao, tumekuja kuongozana nawe kuteremka. Hivyo alianza kuteremka, lakini kwa ushujaa mwingi, ila bado alitereza mara moja au mbili. *Pilgrim's Progress* Part One Stage 4.

Miezi sita baadaye, nilipokea jibu kwa ombi langu la majibu ya Bibilia. Katika jibu hili kuliwasilishwa kwangu orodha ya mafungu yenye maana wazi kwamba Yesu sio Mwana kwa urithi na kwamba "Wa pekee" humaanisha kipekee. Nilipotafakari na kuomba juu ya jibu hili, nilikabiliwa na tangazo kwamba hakuna chochote nilichosema kilibadilisha mtazamo wao kuhusiana na Utatu.

Swali pia liliulizwa kwangu kwamba naweza kuwa naonyesha roho wa kujitegemea. Mtu anaweza jibu aje madai kama hayo? Sikuwa nimetia katika changamoto viongozi na washauri wangu? Hii sio hamu tu ya kujulikana vibaya? *Unadhani wewe ni nani Adrian kuweka wazi ujasiri kama huo, kusababisha uchungu mwingi na mgogoro, sio kwako tu, bali kwa familia na marafiki? Huyu Yesu ambaye unapenda anatosha kweli kustahili haya yote?*

Mawazo haya yalifurukuta akili zangu mbele na nyuma, mbele na nyuma. Mara kwa mara nilijipata nikiota kuhusu utoto wangu na kudumu katika siku za kutojali wakati ambao maisha yalikuwa rahisi sana. Familia yangu ilihamia kwa chumba cha utoto wangu kwa kipindi, kidogo kwa faida ya hewa ya mlimani, lakini kidogo ili niweze kuota juu ya nyakati za furaha na kujaribu kukwepa mgogoro wangu wa hisia.

Kama nilijali kidogo kuhusu kanisa laangu na ndugu zangu, moyo wangu haungeteseka na mawazo ya kutoamua juu ya usahihi wa njia yangu. Mwana huyu, Mwana huyu kwa urithi, alistahili? Nilikuwa nimekosa kuhusu vitu vingine, kwenda kulala na kuamka jinsi nilikuwa miaka miwili au tatu ya awali, na kukosa kukumbuka chochote cha majaribu na migogoro ya sasa.

Kisha niliwaza kuhusu mke wangu na watoto na jinsi wangeathiriwa na njia ninayotembea. Nilipokuwa nikiwaza kuwahusu, nilikumbuka kwamba:

> Ndipo mtaijua kweli nayo kweli itawaweka huru. Yohana 8:32.

Niliwaza kuhusu Mpendwa wangu na yote aliyokuwa amenifanyia. Nilipotembea na kunena naye, nilijua kwamba siwezi mkataa. Alikuwa akinikiri mbele za Baba usiku na mchana, na jinsi ningeonyesha ukosefu wa shukurani kwake kwa kukataa kukubali aibu ambayo hufuata wale ambao humkiri Mwana wa pekee?

Nilifanya kazi bila kufanikiwa kuona usahihi wa kibibilia wa majadiliano yaliyowekwa kwangu. Singeweza kwa dhamiri wazi kukataa kile ambacho nilipata na kuenda dhidi ya dhamiri haikuwa sawa wala salama. Niliamua kufuata njia ya kweli kama nilivyoifahamu kwa ajili ya Bwana Yesu wangu na kwa ajili ya familia yangu ambayo ingeteseka sana kama ningefuata njia ya umaarufu na urahisi. Niliamua pamoja na Paulo:

> Lakini, ninakubali kwamba mimi namwabudu Mungu wa baba zetu mfuasi wa ‘Njia’ ile ambayo wao wanaiita dhehebu. Ninaamini kila kitu kinachokubaliana na Sheria na kile kilichoandikwa katika Manabii: Matendo 24:14.

Mwezi mmoja baadaye niliandika katika jibu kwa kanisa:

Nilijaribu kadri ya uwezo wangu kufunguka kwa vyovyote ndugu yangu alikuwa amewasilisha kwangu na kukizingatia kwa maombi. Nilijaribu niwezavyo, sikuweza kupatanishwa nalo. Ufahamu wangu wa Baba na Mwana katika istilahi halisi ulikuwa umekuwa kati hasa ya theologia yangu na kuruhusu kila suala la mfumo wa imani yangu na kwa hivyo kuweka msingi wa kila kitu nilichowasilisha. Niliwaambia waniombee

nikikumbuka kwamba dhamiri yangu ni bidhaa ya thamani kuu niliyomiliki nasingeikiuka kwa hali yoyote.

Wakati ambao singenyenyekesha dhamiri yangu kwa mtu yeyote, msimamo wangu na jina kanisani vilikuwa mikononi mwa uongozi wa kanisa kikamilifu. Nilifanywa kuamini kwamba njia salama ya kufuata ilikuwa kujinyenyekesha kwa kanisa kwa nidhamu yoyote walihisi kwamba nilihitaji. Nililipenda kanisa langu sana na kuamini kwamba Baba yangu ambaye hutawala juu ya vitu vyote ataruhusu mambo kutendeka kwa usahihi kama alivyoamua. Mpendwa wangu alijinyenyekesha kwa waliotawala juu yake kwa upole, ungwana na neema. Nilihisi kuvutwa kwamba nafaa kufanya vilevile.

Kuelekea mwisho wa mwaka huo nilipokea neno kwamba kanisa litakuwa likiangazia ondoleo langu kama mhudumu wa kanisa. Mara nyingine nilipiga magoti na kuomba bila kukoma kuhusu njia yangu. Nilisoma Bibilia tena, na akili zangu zilikuwa na uhakika kuliko wakati wowote ule kwamba nilikuwa nimemchagua Mwana wa kweli wa Maandiko. Nilipokuwa nikiomba, nilimuuliza Kwamba kama ingewezekana nafasi yangu idumishwe kwa vile nilikuwa naichukulia kuwa upendeleo mkubwa kuwa mhudumu wa kanisa. Ila kama huu ulihitajika kusalimishwa, ningefanya hivyo kwa furaha na bila malalamishi. Neno lilinijia:

> Watawatenga na masinagogi. Naam, saa yaja ambayo mtu ye yote atakayewaua atadhani kwa kufanya hivyo anamtumikia Mungu. (3) Nao watawatenda haya kwa sababu hawamjui Baba wala Mimi. Yohana 16:2-3.

Kama tu wangemjua Baba yangu wa mbinguni na Mpendwa wangu, basi wangejua mbona lazima ningetembea katika njia hii. Hivyo basi nilipokea neno mwisho wa mwezi wa Disemba mwaka huo kwamba sikuwa mhudumu wa kanisa tena. Habari ziliponifikia sikuhisi, uchungu, huzuni, na hakukuwa na machozi. Yote haya yalikuwa yamekabilianwa nayo awali. Katika anguko hili hadi kwa udhalilishaji na moto wa mateso kulisalia tu Mpendwa wangu na Baba yangu Mbinguni. Ni jinsi gani ushirika wao ulikuwa mzuri, ni jinsi gani nilihisi furaha kujua vitu ambavyo sasa nafahamu.

Nilikuwa nimeweka dhabiti kosi yangu licha ya majaribu na migogoro. Nilikuwa nimekabiliana na rafiki zangu na kanisa langu na kumkiri Bwana wangu Yesu. Mchakato huu ulikuwa umedhihirisha tabia kadha zenye dosari na sifa ambazo zilihitaji kuteketezwa katika moto usafishao. Ingawa nilikuwa nimeweka njia yangu dhabiti kuelekea kwa Mwana wa pekee, upendo wa utoto na ujana wangu haungezaa tu uamuzi huu bila upinzani.

# 18. Apollyoni

> APOLLYONI: Wewe umetoka wapi, na unadumu wapi? MKRISTO: Natoka kwenye mji wa uharibifu, ambao ni mahali pa uovu, na ninaenda kwenye mji wa Sayuni.
> APOLLYONI: Kwa hili nakuchukulia kuwa mmoja wa watu wangu; kwa kuwa nchi hiyo yote ni yangu, na mimi ndiye mfalme na mungu wayo. Niaje, basi, kwamba umekimbia kutoka kwa mfalme wako? Kama sio eti ninamatumaini kwamba unaweza nipa huduma zaidi, ningekupiga ngumi moja sasa hivi hadi ardhini.
> MKRISTO: Bila shaka, nilizaliwa katika utawala wako, lakini huduma yako ilikuwa ngumu, na mshahara wako mtu kama huyo hawezi ishi kwao; kwa maana mshahara wa dhambi ni mauti, Rom. 6:23; kwa hivyo, nilipofikia miaka, nilitenda, jinsi mtu mwingine mwenye kufikiria hufanya, angalia pengine naweza jirekebisha.
> APOLLYONI: Hakuna mkuu ambaye anaweza poteza mtawaliwa wake virahisi, wala pia mimi sitakupoteza hivyo; *Pilgrim's Progress* Stage Four.

Baada ya kupokea neno kwamba sikuwa mhudumu wa kanisa tena, niliamua kusalia kimya. Sikujiamini kupinga uwezekano wa kuonyesha kujihurumia na kujaribu kuvuta makini kwa hatma niliyojiumbia. Katika hali hii niliendelea kama mwezi mmoja, lakini asubuhi moja nilipatwa na imani kwamba mazingira ya umma ya ofisi yangu yalihitaji kuomba msamaha kwa umma kutoka kwangu kwa kosa langu la kuamini na kuendeleza Utatu. Katika nuru ya Mpendwa wangu na Baba yangu, kosa hili lilionekana chungu sana kwangu na niliamua kufanya chochote ambacho kilihitajika ili kurekebisha mwendo wangu. Niliandika barua ya kuomba msamaha na kukiri kuhusiana na Mpendwa wangu. Niliituma kwa watu wengi ambao walikuwa wameathiriwa na huduma yangu. Nilihisi kwamba nilihitaji kuwaomba msamaha. Pia niliyaandikia makanisa ambayo nilikuwa nimekuwa mchungaji wao kwa kuwafundisha mafundisho ya uongo.

Kwa ufahamu mpana wa umma juu ya nafasi yangu, nilihisi haja ya kuandika makala kadha nikielezea uamuzi wangu kwa Mpendwa wangu. Baadhi walikaribisha uamuzi wangu na wakamtukuza Bwana hadi nikaelezea kwamba bado niliamini kwamba Mungu bado alikuwa akiliongoza kanisa letu. Uamuzi wangu kwa Mpendwa wangu ulisababisha kupotea kwa marafiki wangu wengi kanisani, na uamuzi wangu kwa mapendeleo ya kanisa ulisababisha ukengeufu wa wengi ambao walikiri imani katika Mwana wa pekee.

Mara kadha nilijiuliza kwa hitaji la kukengeua kila mtu. Hakika lazima kuna nia ya siri ambayo pia hata haikujulikana kwangu! Kwa mtu ambaye alitamani amani, upendo na urafiki, mbona nilionekana kwenda upande kinyume na watu hawa wote? Nilihisi ningeweza kuwafahamu kikamilifu wale ambao walikuwa wakiangazia kesi yangu ambao walikuwa wakipitisha hukumu na kuhitimisha kwamba nilikuwa mfitini wa kugawanya tu na bila kitu cha maana cha kufanya. Ningesukuwa sana nisifikie hitimisho hiyo katika hali tofauti. Ingawa hili lilikuwa tokeo la furaha nzuri, amani na upendo nilioshuhudia na Mpendwa wangu. Sikutafuta njia ya mapigano; nilitamani tu kufuata wito wa kimziki wa Mpendwa wangu.

Wakati huu, changamoto ya mvulana wetu mchanga na Autism ilionekana kuongezeka. Akawa amezidi kuchafuka na kuwa na fujo. Kwa wakati uo huo ilianza kunikulia vigumu zaidi kusalia mtulivu machoni pa hali ngumu. Bila kujua, familia yetu ilikuwa imechukua kimelea kutoka kwa maji ya tangi na kilikuwa na athari kubwa hasa kwa kijana wangu mdogo nami. Wakati uo huo tuligundua kwamba chumba ambacho tulikuwa tumekomboa kilikuwa na shida ya mold. Hili lilisababisha mambo kadha kwetu kama familia. Tuliamua kuhamia kwa sehemu kavu, bado bila kufahamu kuhusu kimelea. Msongo wa kukabiliana na kanisha ukiunganishwa na athari za kimelea ulipambua mfumo wangu wa neva kabisa. Nikiwa katika hali hiyo, mvulana wangu mchanga alilemewa na hali sawia kwamba kukatishwa tamaa kwake na uchungu kulichemka kwa hasira ambayo ilipelekea kwa maonyesho kadha ya hasira kwa fujo.

Katika hali yangu ya afya pamoja na tabaka nyingi za utata zilizohusika katika kukabiliana na jinsi kanisa lilijibu upendo wangu kwa Mpendwa wangu, niliingia katika kipindi cha giza kuu kwa zaidi ya mwaka. Wakati huu, nililazimika kuomba nguvu za kufika siku nyingine bila kukoma. Nilijishikilia kwa Zaburi na kumsihi Mungu anisaidie. Kwa vile kila kitu kilionekana kuvunjika ndani yangu, na nilifika mahali ambapo nilihisi maisha hayana maana. Ila bado kukiwa na migogoro hii yote mikubwa, Roho mzuri wa kufariji wa Yesu alikuja, hasa Sabbato na kutusaidia. Oh ni jinsi gani faraja ya Yesu ilivyo ya thamani. Ni mfariji wangu mzuri wakati wa jaribio.

Mara nyingi nilipojaribu kuandika makala au kushiriki chochote kuhusu kile nilikuwa nimejifunza, ilionekana kwamba nyumba yetu ingegeuzwa juu chini. Tungepiga magoti na kuomba usaidizi, na kisha msaada ungekuja.

Baada ya miezi mingi ya hali hii ya mgongano, nilijihisi nimezama katika kukata tamaa kwa kina ambapo nilihisi kwamba singeweza kuepuka. Katika hali ya giza ya akili, nilisikia sauti ya mshawishi ikininenea. Aliashiria kwamba Mungu ameniacha, na kwa hivyo mbona nisimuache? Mara moja nilibaini sauti hii, nikadai Maandiko na kujishikilia kwa Yesu. Ni heri nife kuliko kuacha upendo wangu kwa Mpendwa wangu. Apollyoni, akiona hali yangu iliyodhoofika, sasa alipendekeza nimuache Mpendwa wangu. Uzani wangu ulikuwa umeshuka kwa kiwango cha chini kuliko wa mke wangu, lakini bado nilishikilia rehema za Mungu wangu, na nikashikilia ahadi:

> Nalimngoja Bwana kwa saburi, Akaniinamia akakisikia kilio changu. (2) Akanipandisha toka shimo la uharibifu, Toka udongo wa utelezi; Akaisimamisha miguu yangu mwambani, Akaziimarisha hatua zangu. (3) Akatia wimbo mpya kinywani mwangu, Ndio sifa zake Mungu wetu. Wengi wataona na kuogopa, Nao watamtumaini Bwana. Zaburi 40:1-3.

Mke wangu pamoja nami sote tulijaribiwa vyema zaidi ya vile tulidhani inawezekana, na bado tulikuwa katika upendo na Mwana wa Mungu. Muda mfupi baada ya matukio haya, tuligundua kimelea, tukapokea matibabu yaliyofaa na tukaanza kupata nafuu. Kila siku ikawa rahisi

kidogo na nzuri. Tulijifunza kwa kushuhudia kwamba kama tulimiliki chochote nyumbani mwetu ambacho hakikumheshimu Mungu, tutakuwa na wakati mgumu nyumbani mwetu. Tulichunguza kila kitu tulichomiliki kwa maombi na tukaondoa kila kitu ambacho kwa njia yoyote kingeakisi roho wa ulimwengu.

Ingawa wakati huu ulikuwa na changamoto sana, tulipata elementi nyingi za takataka zilichomwa kutoka maishani mwetu. Ingawa adui alijaribu kutugeuza kutoka kwa njia ya kweli, Mkombozi wetu Mpendwa alifanya hali yetu itendeke kwa ajili ya wema.

Kwa kila siku ambayo tuko na amani sasa, tunajua kwamba malaika wa Baba yetu wa mbinguni wanatulinda na kutukinga kutokana na madhara. Majaribu yetu yalitufanya kutambua papo hapo ulinzi huu wa kupendeza. Hatuchukulii vitu hivi kwa mzaha kama tulivyofanya wakati mmoja.

Tungeona mwanzoni, njia mbele yetu na mgogoro utakaopitiwa, mioyo yetu ingezimia kwa uchungu wa moyo. Kwa wingi wa rehema tulipitishwa katika majaribu haya ya kutisha bila kujua kilichokuwa mbele yetu. Kwa kuishi siku moja kwa wakati, tulijishikilia kwa Baba yetu mpendwa na Mwanawe, kusadiki, kuamini na kuhiari kwamba katika wakati ulioteuliwa, ukombozi utakuja.

> Kisha Apollyoni, akipeleleza fursa yake, alianza kukusanya karibu na Mkristo, na kupigana naye, akampa anguko la kutisha; na kwa hilo upanga wa Mkristo uliruka kutoka mikononi mwake. Kisha Apollyoni akasema, ni na uhakika nawe sasa: na kwa hilo alikuwa amemkaza kwa kifo, ili kwamba Mkristo alianza kukata tamaa ya maisha. Lakini, kama Mungu alipoipokea, wakati Apollyoni akiwa anateka pigo la mwisho, na kwa hivyo kufanya mwisho kamili wa mtu huyu mzuri, Mkristo kwa umahiri alinyosha mkono wake kuupokea upanga wake, na kuushika, akisema, Usifurahi juu yangu, Ee adui yangu; niangukapo, nitasimama tena; Mika. 7:8; na kwa hilo alimpa pigo la mauti, ambalo lilimfanya arudi nyuma, kama ambaye amepokea jeraha lake la mauti. Mkristo akitambua hilo, alilifanya kwake tena, akisema, Lakini katika mambo haya yote tunashinda, naam na zaidi ya kushinda,

kwa Yeye aliyetupenda. Rom. 8:37. Na kwa hilo Apollyoni alitandaza mabawa yake ya joka; na akakimbia, kwamba Mkristo hakumuona tena. Yakobo 4:7.

Katika pambano hili hakuna mtu anaweza fikiria, isipokuwa alikuwa ameona au kusikia, kama nilivyofanya, kunguruma na kishindo cha kutisha ambacho Appolyoni alifanya wakati wote wa vita; alinena kama joka: na kwa upande mwingine, ni pumuo lipi na uguo lilitoka katika moyo wa Mkristo. Kamwe sikumuona wakati huo wote akitoa mengi kwa mtazamo wa kupendeza, hadi alipotambua kwamba alikuwa amemjeruhi Apollyoni kwa upanga wake ukatao kuwili; kisha, bila shaka, alitabasamu, na kutazama juu! Lakini lilikuwa onyesho la kutisha zaidi nimewahi ona.

Hivyo vita vilipoisha, Mkristo alisema, hapa nitatoa shukrani kwake aliye nikomboa kutoka kwa kinywa cha simba, kwa yule ambaye alinisaidia dhidi ya Apollyoni. *Pilgrim's Progress*, Stage Four.

## 19. Msaidizi

Tunapotembea katika njia hii ya hija na kukubana na majaribu mbalimbali, kuna mfariji mmoja juu ya wengine wote ambaye wanatusaidia.

> Kwa sababu hii ilibidi afanane na ndugu Zake kwa kila hali, ili apate kuwa Kuhani Mkuu mwenye huruma na mwaminifu katika kumtumikia Mungu, ili pia apate kufanya upatanisho kwa ajili ya dhambi za watu. (18) Kwa kuwa Yeye mwenyewe aliteswa alipojaribiwa, aweza kuwasaidia wale wanaojaribiwa. Waebrania 2:17-18.

Bibilia inatwambia kwamba, kwa sababu Yesu aliteswa alipojaribiwa anaweza kusaidia (kumaanisha msaada au kupunguza) wanaojaribiwa. Ila kama sasa Yesu yuko mbinguni akituombea, anawezaje kuwa yeye ndiye anatusaidia? Yesu alielezea hili kwa makini zaidi kwa wanafunzi wake alipowaambia kwamba anaenda.

> Simoni Petro akamwuliza, "Bwana, unakwenda wapi?'' Yesu akamjibu, ''Ninakokwenda huwezi kunifuata sasa, lakini utanifuata baadaye.'' (37) Petro akamwuliza tena, "Bwana, kwa nini siwezi kukufuata sasa? Mimi niko tayari kuutoa uhai wangu kwa ajili Yako. Yohana 13:36, 37.

Petro alimpenda Bwana wake na hakutaka kutenganishwa naye. Alimuuliza Yesu kwa huzuni mbona hangemfuata. Katika sura inayofuata ya Yohana, Yesu anawaelezea jinsi bado atakuwa nao hata kama kimwili lazima atawaacha.

Yesu anawaambia wanafunzi wasifadhaike mioyoni; anaenda kuwaandalia makao na atarudi tena. Kisha kutoka Yohana 14:4-11, Yesu anaelezea uhusiano wake na Baba yake na jinsi yeye ni sura moja kwa moja Yake.

Katika fungu la sita Yesu anatoa kauli muhimu sana ambayo wengi wanaijua. Anasema kwamba yeye ndiye njia, ukweli na uzima. Ukweli kwamba Yesu anajirejelea kama uzima ni muhimu sana katika mafungu yafuatayo.

Yesu anapoelezea ukaribu wa uhusiano wake na Baba yake, kisha anawaambia wanafunzi wake wamwombe Baba lolote wanaweza hitaji kwa jina lake.

> Kama mkiniomba lo lote kwa Jina Langu nitalifanya. Yohana 14:14.

Tukumbuke kwamba majadiliano haya yote kati ya Yesu na wanafunzi wake yanatendeka kwa sababu wanafadhaika kuhusu yeye kuwaacha. Ni kwa sababu ya hoja hii ndio Yesu anaamua kudhihirisha mawazo yao: kisha anasema:

> Kama mnanipenda, mtazishika amri Zangu. (16) Nami nitamwomba Baba, naye atawapa Msaidizi mwingine akae nanyi milele. (17) Huyo ndiye Roho wa kweli ambaye ulimwengu hauwezi kumpokea, kwa sababu haumwoni wala haumjui. Ninyi mnamjua kwa kuwa yuko pamoja nanyi naye anakaa ndani yenu. (18) Sitawaacha ninyi yatima, naja kwenu. Yohana 14:15-18.

Yesu alinena kuhusu msaidizi mwingine ambaye angekuja kutoka kwa Baba. Zingatia kwa makini kile ambacho Yesu alisema:

1. Msaidizi ni Roho wa Kweli
2. Ulimwengu haumjui
3. Wanafunzi tayari wanamjua
4. Yuko pamoja nao
5. Atakuwa ndani yao
6. Yesu hatawaacha yatima
7. Yeye mwenyewe atakuja kwao.

Kama Yesu ni ukweli basi Roho wa kweli ni Roho wa Yesu. Yesu hakuwa ametaja Msaidizi awali na ila anasema kwamba wanafunzi tayari wanamjua kwa sababu yuko pamoja nao. Ni nani ambaye alikuwa pamoja nao? Alikuwa Yesu! Basi Yesu anaiweka wazi. Anasema kwamba hatawaacha yatima lakini badala yake yeye mwenyewe atakuja kwao.

Baadaye katika sura hiyo tu, Yesu anamuita Msaidizi, Roho Mtakatifu.

> Lakini huyo Msaidizi, yaani, huyo Roho Mtakatifu, ambaye Baba atamtuma kwenu kwa Jina Langu, atawafundisha mambo yote na kuwakumbusha yote niliyowaambia. Yohana 14:26.

Mbona wakati mwingine Yesu ananena kana kwamba anakuja kuwasaidia na kisha wakati mwingine anaonekana kuonyesha kwamba anamtuma mtu mwingine? Yesu mara nyingi alizungumza kujihusu katika nafsi ya tatu. Zingatia mafungu haya:

> Baada ya Yuda kutoka nje, Yesu akasema, Sasa Mwana wa Adamu ametukuzwa, naye Mungu ametukuzwa ndani Yake. Yohana 13:31.
>
> Ninawaambia, atawapatia haki upesi. Lakini je, Mwana wa Adamu atakapokuja ataikuta imani duniani? Luka 18:8.

Katika mafungu haya Yesu anamuita Mwana wa Adamu “yeye” na “naye” ingawa anajirejelea. Hili lilikuwa jambo la kawaida kwa Yesu.

Nini kingine tunaweza jifunza kuhusu Roho Mtakatifu? Zingatia mafungu haya sambamba.

> Kwa sababu si ninyi mtakaokuwa mkinena, bali ni Roho wa Baba yenu atakayekuwa akinena kupitia kwenu. Mathayo 10:20.
>
> Mtakapokamatwa na kushtakiwa, msisumbuke kuhusu mtakalosema. Semeni tu lo lote mtakalopewa wakati huo, kwa kuwa si ninyi msemao bali ni Roho Mtakatifu. Marko 13:11.

Angalia jinsi Roho mtakatifu katika Marko 13:11 anaitwa Roho wa Baba yetu katika Mathayo 10:20. Yesu aliwaelezea wanafunzi zaidi:

> Lakini atakapokuja huyo Msaidizi nitakayemtuma kwenu kutoka kwa Baba, yaani, huyo Roho wa kweli atokaye kwa Baba, Yeye atanishuhudia Mimi: Yohana 15:26.

Roho Mtakatifu hutoka kwa Baba na huleta uwepo wa kipekee wa Baba na Mwanawe. Nikupitia kwa uwakala wa Roho Mtakatifu ndio Yesu mwenyewe huja kwetu na kutusaidia. Zingatia jinsi Bibilia inatumia maneno Roho kwa uwepo sambamba.

> Niende wapi nijiepushe na roho yako? Niende wapi niukimbie uso wako? Zaburi 139:7.

Ni kwa sababu hii ndio Paulo anatumia maneno kadha kwa kuyabadilishana.

> Lakini ninyi, hamtawaliwi na mwili, bali na **Roho**, ikiwa **Roho wa Mungu** anakaa ndani yenu. Mtu ye yote ambaye hana **Roho wa Kristo**, yeye si wa Kristo. (10) Lakini kama **Kristo** anakaa ndani yenu, miili yenu imekufa kwa sababu ya dhambi, lakini **roho** zenu zi hai kwa sababu ya haki. Warumi 8:9-10.

Zingatia mshikamano:

Roho = Roho wa Mungu = Roho wa Kristo = Kristo = Roho

Vitu hivi vyote vinatwambia kwamba kupitia kwa Roho Mtakatifu, Yesu anaweza tusaidia moja kwa moja. Zawadi hii yakupendeza hutiririka kutoka kwa kiti cha enzi cha Mungu kama mto mkuu ambao hutiririka katika mioyo ya wale wenye kiu ya Kristo.

> Kisha yule malaika akanionyesha mto wa maji ya uzima, maangavu kama kioo yakitiririka kutoka kwenye kile kiti cha enzi cha Mungu na cha Mwana-Kondo. Ufunuo 22:1.
>
> Siku ile ya mwisho ya Sikukuu, siku ile kuu, wakati Yesu akiwa amesimama huko, akapaza sauti Yake akasema, "Kama mtu ye yote anaona kiu na aje Kwangu anywe. (38) Ye yote aniaminiye Mimi, kama maandiko yasemavyo, vijito vya maji ya uzima vitatiririka ndani mwake.'' (39) (Yesu aliposema haya alimaanisha Roho Mtakatifu ambaye wote waliomwamini wangempokea, kwani mpaka wakati huo, Roho alikuwa hajatolewa, kwa kuwa Yesu alikuwa bado hajatukuzwa.) Yohana 7:37-39.
>
> Lakini ye yote anywaye maji nitakayompa, hataona kiu kamwe. Maji nitakayompa yatakuwa ndani yake chemchemi ya maji yakibubujika uzima wa milele. Yohana 4:14.

Maji ya uzima ambayo Yesu alizungumzia kuyahusu kwa mwanamke kisimani yalikuwa zawadi ya kipekee ya uwepo wake kupitia uwakala wa Roho wa Mungu.

Tunaelewa jinsi hili hutenda kazi?

> Upepo huvuma po pote upendapo. Mvumo wake unausikia lakini huwezi ukafahamu utokako wala uendako. Ndivyo ilivyo kwa kila mtu aliyezaliwa na Roho. Yohana 3:8.

Hatujui jinsi Kristo hutusaidia kupitia Roho Mtakatifu; tunajua tu kwamba yeye ndiye huja kwetu. Mbona Yesu ni msaidizi wetu? Bibilia inatwambia:

> Kwa kuwa Yeye mwenyewe aliteswa alipojaribiwa, aweza kuwasaidia wale wanaojaribiwa. Waebrania 2:18.

Ukweli rahisi umekuwa wa thamani kwangu. Hivi ndivyo kweli naweza kuja kumjua Mpendwa wangu. Bila Roho wa Kweli singeweza kumjua ambaye ni Ukweli. Kama Roho wangekuwa viumbe tofauti kama inavyodaiwa katika Utatu basi kazi yote ya Roho ingekuwa mchakato wa Roho ungekuwa kujifunza kujua na kupenda kiumbe huyo. Na basi sio Kristo anatusaidi bali mwingine. Ila Yesu tu anajua jinsi nahisi na kwa hivyo yeye tu anaweza kweli nisaidia.

Utatu unafanya mchakato huu kutatiza zaidi. Yesu alisema:

> Atakapokuja huyo Roho wa kweli atawaongoza awatie katika kweli yote. Yeye hatanena kwa ajili Yake mwenyewe, bali atanena yale yote atakayosikia, naye atawaonyesha mambo yajayo. Yohana 16:13.

Roho haneni kwa ajili yake mwenyewe, kumaanisha kwamba chochote Roho atendacho, sio lengo letu kama mtu tofauti na Kristo, Kristo ni lengo letu, na Kristo ni msaidizi wetu.

Nakumbuka mara ya kwanza iliponigonga kwamba Yesu alikuwa yeye mwenyewe aliyekuwa nami badala ya mtu akiwa asiyejulikana ambaye hakutembea katika mwili wangu wala kuelewa majaribu yangu. Nililia kwa furaha kwa urahisi wake. Kama tu Yesu alivyokuwa amewaambia wanafunzi wasiruhusu mioyo yao kufadhaika kwa sababu atakuja kwao na kuwasaidia, hivyo hata sasa Kristo anakuja kwetu na kutusaidia ili kwamba tuweza kula naye na kushuriki naye.

Kupitia kwa jaribio langu la kusafisha ninapomkiri Mpendwa wangu na ninapokabiliana na Apollyoni, msaada wangu mzuri ulikuwa katika kujua

kwamba Yesu alikuwa pamoja nami, akinitia moyo, akinisaidia, akinitia nguvu, akinipenda na akinibariki. Oh ni mawazo ya thamani namna gani. Oh ni ukweli mtukufu namna gani.

Kuja kwa Eliya kuliashiria wapenzi wawili wakitafuta mkono wangu, na ninashukuru kwa jaribio la moto usafishao, vikwazo kwa safari yangu kwelekea Patakatifu pa Patakatifu viliondolewa. Yesu anasema:

> Nayajua matendo yako. Tazama, nimeweka mbele yako mlango uliofunguliwa, wala hakuna awezaye kuufunga. Ninajua kwamba una nguvu kidogo lakini umelishika neno Langu wala hukulikana Jina langu. Ufunuo 3:8.

Kwa wale ambao hawalikatai jina la Mwana wa Mungu, lango la Patakatifu pa Patakatifu linasalia wazi.

## Kiingilio IV

Moyo wangu utaimba, Mpendwa wangu, kwa kunipa ufahamu wa mbona nilizidi kumpoteza. Urithi wangu kutoka kwa Adamu na mambo ya uchumbiano wa udanganyifu wa mjaribu yalinishawishi, kunikanganya na kuhuzunisha moyo wangu. Ingawa nilikuwa nimekupoteza, nilitumaini.

> Mpendwa wako amekwenda wapi, Wewe uliye mzuri katika wanawake? Mpendwa wako amegeukia upande upi, Ili tumtafute pamoja nawe? (2) Mpendwa wangu ameshukia bustani yake, Kwenye matuta ya rihani; Ili kulisha penye bustani, Ili kuchuma nyinyoro. (3) Mimi ni wake mpendwa wangu, naye ni wangu, Hulisha kundi lake penye nyinyoro. Wimbo Ulio Bora 6:1-3.

Katika moto utakasao moyo wangu umebadilishwa, mawazo yangu yamefanywa upya. Kwa imani nayasikia maneno yako kwangu.

> Hua wangu, mkamilifu wangu, ni mmoja tu, Mtoto wa pekee wa mamaye. Ndiye kipenzi chake aliyemzaa, Binti wakamwona wakamwita heri; Malkia na masuria nao wakamwona, Wakamsifu, wakisema, (10) Ni nani huyu atazamaye kama alfajiri, Mzuri kama mwezi, safi kama jua, Wa kutisha kama wenye bendera? (11) Nalishukia bustani ya milozi, Ili kuyatazama machipuko ya bondeni; Nione kama mzabibu umechanua, Kama mikomamanga imetoa maua. (12) Kabla sijajua, roho yangu ilinileta Katikati ya magari ya wakuu wangu. (13) Rudi, rudi, Mshulami, Rudi, rudi, ili sisi tukutazame. Wimbo Ulio Bora 6:9-13.

Nimerudi, Mpendwa wangu, nikiamini kwamba bustani yangu ya tabia imenawili na kwamba unafurahia ndani yangu. Mwezi ni shahidi chini ya miguu yangu na mwanga wa Jua ni vazi langu; juu ya kichwa changu panakaa taji ya nyota kumi na mbili. Nyoka alitafuta kunimeza, ila watenda kazi wako na fimbo zilinifariji katika kivuli cha bonde la mauti. Niliketi katika meza ya karamu yako mbele ya macho ya adui zangu na "bendera yako juu yangu ilikuwa upendo." "Hakika wema nazo fadhili zitanifuata siku zote za maisha yangu."

Kupitia kwa miale ya mateso, hofu yangu ya ndani ya Baba yako ilitawala. Nilishangaa kama anaweza nikubali, anaweza bariki upendo ambao nahisi kwako? Najua ulitamani kunichukua nikamwone Baba yako katika Patakatifu mno, ila hofu yangu ilinilemea na kunibeba.

Niliposikia hatua za Baba yako zikielekea kwenye kiti cha hukumu, moyo wangu ulizama ndani yangu. Nilihofu kwamba angetutenga kwa sababu ya dhambi zangu! Ila kwa maneno ya kufariji ya sauti katika jangwa, nimejifunza kwamba Baba yako ni kama wewe tu; kwa kuwa ulirithi vitu vyote kutoka kwake.

Sasa hatua za Baba yako kwelekea hukumuni sio hatua za kuhukumu, bali hatua za kumsogea mpotovu wake. Mikono yake imefunguliwa kabisa kwangu, Mpendwa wangu! Baba yako ananipenda, Mpendwa wangu! Baba yako ananikubali, Mpendwa Wangu! Kwa kweli atabariki upendo wetu kwa kila mmoja, hakika atanichumbisha kwako.

> Mimi ni wake mpendwa wangu, Na shauku yake ni juu yangu. (11) Njoo, mpendwa wangu, twende mashambani, Tufanye maskani katika vijiji. (12) Twende mapema hata mashamba ya mizabibu, Tuone kama mzabihu umechanua, Na maua yake yamefunuka; Kama mikomamanga imetoa maua; Huko nitakupa pambaja zangu. Wimbo ulio Bora 7:10-12.

# Sehemu 5. Patakatifu Pa Patakatifu

## 20. Kuchumbiwa na Zama za Kale



Uwezo wangu kudumu kikamilifu katika upendo wa Mkombozi wangu ulitegemea sio tu ahadi zake kwangu, bali pia kwa kukubalika na kuthibitishwa na Baba yake. Katika miaka yangu yote ya kusoma Maandiko, nilikuwa nimejifunza kwamba ni katika hukumu ambapo lazima nitasimama mbele za Mungu na kukutana na Baba ya Mpendwa wangu halisi katika Patakatifu pa Patakatifu.

Kutoridhishwa kwangu kuhusu kukutana na Baba ya Mpendwa wangu mara nyingi kulifichwa kutoka kwa wengine na hata kwangu mimi mwenyewe, ila kulijionyesha kwa njia mbalimbali. Kila wakati ningeanguka katika dhambi, ningetubu, lakini pia wakati mwingine nilianza kuelea katika hali ya kukataa. Uoga wangu uliokaa ndani uliniongoza kwa nguvu zaidi kuelekea kwa burudani, anasa na kujihurumia.

Nilipoanza kusoma Bibilia na kumthamini Mkombozi wangu, njia ya kuelekea Patakatifu pa Patakatifu ilianza kuchukua sura. Kisha nilitambua kwamba tangu 1844 Mpendwa wangu alikuwa amechukua kazi ya kipekee ya kutuombea na hukumu katika Patakatifu pa Patakatifu.

Ningepata faraja katika wazo kwamba Yesu aliniwakilisha kwa Baba. Hata ningeona ushahidi kwamba Baba alinipenda. Ingawa mbegu iliyopandwa na mshawishi kuhusiana na hitaji la heshima na kuidhinishwa kupitia kwa

mafanikio yangu iligongana ana kwa ana na uhalisia wa Kiumbe huyu kuwa kwenye Enzi ambaye hupeana uzima na pumzi kwa wote.

Kadri kulivyokuwa na athari yoyote ya upendo wa miungu ya mshawishi moyoni mwangu, singeweza kusimama mbele ya Chanzo cha vitu vyote na Chemchemi ya sheria yote na kuhisi uwezo wa kupumzika. Hii ndio sababu mbona wengi wa Wakristo ulimwenguni hukataa kabisa kazi ya hukumu ilianza 1844. Wakristo wengi kihisia hawataki kukutana na Baba; wanatamani tu kuwa na sura yao ambayo wanamdhania Yesu kuwa.

Sababu tu ambayo tutataka kwenda katika Patakatifu pa Patakatifu ni kuwa kwa kweli tunampenda Mkombozi wetu. Kama Esta tunaweza sema:

> …nami na wajakazi wangu tutafunga vile vile; kisha nitaingia kwa mfalme, kinyume cha sheria; nami nikiangamia, na niangamie. Esta 4:16.

Mpendwa wetu mzuri anatuhimiza kukabiliana na kile ambacho lazima kikabiliwe ili kujishikilia kwake. Jambo lingine la kupendeza kuhusu kumkaribia Baba katika Patakatifu pa Patakatifu ni kwamba wakati tu tunampenda Yesu kwa kweli tutajua moyo wa Baba kweli na upendo wake kwetu. Mchakato mzima ni ithibati ya kipumbavu.

Eliya[11] aliponijia na kunionyesha tofauti wazi kati ya Utatu na Baba na Mwana, niliona kwamba umbo liitwalo Baba katika Utatu kwa kweli halingefikiwa katika moyo wangu. Hakuwa Baba wa kweli wa Yesu, na kwa hivyo hakumtoa mwanawe kweli. Aliponena maneno, "Wewe ndiye Mwanangu Mpendwa," sehemu yangu ilifurahia, lakini sehemu nyingine isiyozungumziwa ilitambua kwamba huu haukuwa ukweli wa ndani.

Nilipokuwa nikitazama Mwana halisi wa Mungu, alinifungulia njia ya kumkaribia Baba; mtazamo wake wa Baba ukawa jiwe la pembeni la

[11]. Eliya kuja kwangu, namaanisha ujumbe wa Eliya ambao unaweka tofauti wazi kati ya Baba na Mwana na Utatu.

mtazamo wangu. Upendo wa Baba kwa Mwanawe ukawa jiwe la pembeni la upendo wake kwangu. Katika uhusiano huu halisi tu wa Baba na Mwana ningeweza kujua kwamba Baba alinipenda na kunikubali kweli.

Kupitia kwa kanuni ya urithi pekee ninaweza pata faraja katika maneno:

> Mtu ye yote aliyeniona Mimi, amemwona Baba; Yohana 14:9.

Nilipotazama mfanano hasa wa Mpendwa wangu kwa Baba yake, moyo wangu ulipata ujasiri katika ahadi:

> Kwa hiyo tunamsifu Mungu kwa huruma zake kuu alizotumiminia kwa sababu sisi ni wa Mwanae Mpendwa. Waefeso 1:6.

Mara nyingi sana nilikuwa nimesoma maneno haya, nilijiambia kuyaamini, na kujishikilia kwayo. Ila nilijipata nikitereza kutoka kwa njia ya kwelekea Patakatifu pa Patakatifu na kuingia katika njia nyingine. Kama Eliya hangefichua upendo wangu wa siri kwa nafsi kupitia kwa upotoshaji wa Utatu, kamwe singewahi hisi ujasiri wa kumsogea Baba ya Mpendwa wangu.

Washiriki wengi wa makanisa tayari wametelekeza mchakato huu. Wanatangaza kwamba "Yesu alichukua hukumu yangu" au kwamba 1844 ni shere tu kidogo yenye maana ya kutumia faida ya upatanisho na kuudhihirishia ulimwengu kile ambacho Mungu alijua tayari. Yote haya humeza ukweli kwamba mioyo kama hiyo ya mwanadamu haiwezi salimisha mbegu ya joka ambayo hukataa ukweli kwamba Baba ndiye chanzo kikuu cha vyote.

Hakuna ya vitu hivi vya kitheolojia kinaondoa ukweli kwamba tunahitaji hisia ya kweli ya ukubali kutoka kwa Baba ya Bwana harusi. Ukweli wa Baba pekee kutoa Mwanawe kwa dhambi zetu unaweza teka roho vya kutosha kuvumilia uzoefu wa Patakatifu pa Patakatifu.

> Hivi ndivyo Mungu alivyoonyesha upendo Wake kwetu, kwa sababu Mungu alimtuma Mwanawe wa pekee ulimwenguni, ili tupate uzima kwa Yeye. (10) Huu ndio upendo, si kwamba tulimpenda Mungu, bali Yeye alitupenda, akamtuma Mwanawe, ili

> Yeye awe dhabihu ya kipatanisho kwa ajili ya dhambi zetu. 1 Yohana 4:9-10.

Machoni pa hakimu mkuu wa ulimwengu, uhalisia wowote sambamba unaoelekeza kwa dhana kwamba Mungu kweli ni viumbe watatu ndani ya mmoja utaua kiini cha ukweli kwamba Mungu alimtoa Mwanawe kwa sababu anatupenda. Zawadi ya fumbo humaanisha ukubali wa fumbo ambao unawekwa wazi kabisa chini ya uchunguzi wa hukumu.

Kwa roho ambayo imepata furaha katika Mwana wa pekee, nyayo za Baba kuelekea kwa kiti cha hukumu mbinguni ni nyayo za halisi. Kwa yule ajipendaye, hili tena ni fumbo lingine la upendo mkuu wa mungu wa Utatu ukionyeshwa kwa roho za wanadamu ili kutupa chanzo cha tumaini. Mawazo ya utatu mara nyingi huhitajika kufanya nyayo za Baba kuelekea Patakatifu pa Patakatifu kuwa kimafumbo kwa sababu hatua halisi kuelekea kwa hukumu zinaogopesha zaidi kutafakari.


Kwa wale ambao wametazama kwa muda mrefu katika macho ya Mkombozi wetu, nyayo za Baba hudhihirisha hamu yake ya kumuoza Mwanawe kwa bibi harusi. Mchakato wa hukumu hudhihirisha ni nani kweli humpenda Mwanawe na kwa hivyo nani anaweza mtia mhuri kuishi naye milele. Wale tu ambao wanamjua Baba kupitia Mwanawe wanaweza pata pahali pa siri pa Patakatifu pa Patakatifu.

Hatuhitaji kuhofu hukumu ya Mungu. Anahamu ya kudhihirisha kutukubali kwake kwa upendo. Ufunguo tu ni katika kutambua yeye na Mwanawe ni akina nani, na katika utambuzi huo tunao uzima wa milele.

> Nao uzima wa milele ndio huu, wakujue Wewe uliye Mungu wa pekee, wa kweli na Yesu Kristo uliyemtuma. Yohana 17:3.

Hatutasongea kiti cha enzi cha rehema kwa kujiamini na ujasiri tukijua kwamba mahitaji yetu yote yatashughulikiwa na kwamba Baba kweli anaidhinisha upendo wetu kwa Mwanawe?

## 21. Mbele ya Sanduku la Agano



Uhakika wa upendo wa Mungu kupitia kwa Kristo huwezesha roho kukaribia kiti cha hukumu. Tunapokaribia kiti cha hukumu, uwepo wa sheria hutufanya kuhisi hitaji letu kuu. Hitaji letu kuu hutufanya kuagiza nguvu za kushinda; maisha yanatengenezwa zaidi kwa maombi kuliko mazungumzo. Kazi ya mpatanishi inakuwa mada kuu kwa mdhambi. Imani yetu kuwa maombi yetu yanasikika inakaa dhabiti kwa imani katika Kristo kama mpatanishi wetu.

Kama tulikuwa tukipanga safari ya kwenda kwenye msitu wa Afrika kukutana na mfalme wa taifa flani, tunaweza hisi tukiwa salama katika kumuuliza jirani yetu ambaye ameomba kitabu kuhusu taifa hilo kutoka kwenye maktaba kuwa kama mkalimani? Ni dhahiri, ujuzi wa jirani yetu wa kuelewa tabia na mahakama ya mfalme mgeni hauwezi tupa imani ya namna yoyote.

Kama tukisafiri katika taifa hili la mbali na kumwamini mmoja wa afisa wa mfalme kuwa kama mkalimani, tunaweza kuwa na imani zaidi? Hapana, kwa sababu mtu huyu ambaye anajua njia za mfalme vyema zaidi, hajui chochote kuhusu taifa letu, desturi au mahitaji. Imani yetu kuwa mkalimani huyu anaweza fahamu ombi letu itakuwa ya kiwango cha chini zaidi.

Tunapokuja kwenye enzi ya Mungu, tunalo hitaji la dharura la kujua kwamba mwombezi wetu kweli anafahamu njia zote za Mungu na za mwanadamu. Ujumbe wa Waebrania wa kwanza na wa pili unapeanwa haswa kwa lengo la kumdhihirisha Yesu kama mpatanishi ambaye anaweza patanisha kweli.

Wacha tuzingatie hili kwa makini:

> Zamani Mungu alisema na baba zetu kwa njia ya manabii mara nyingi na kwa njia mbalimbali, (2) lakini katika siku hizi za mwisho amesema nasi kwa njia ya Mwanawe, ambaye amemweka kuwa mrithi wa vitu vyote, ambaye kwa Yeye aliuumba ulimwengu. (3) Mwana ni mng'ao wa utukufu wa Mungu na mfano halisi wa nafsi Yake, akivihifadhi vitu vyote kwa neno Lake lenye uweza. Akiisha kufanya utakaso kwa ajili ya dhambi aliketi mkono wa kuume wa Ukuu huko mbinguni. (4) Kwa hiyo alifanyika bora kuliko malaika kama Jina alilorithi lilivyo bora kuliko lao. Waebrania 1:1-4.

Katika kifungu cha hapo juu, tunaweza kuwa na imani kwamba Yesu anajua mawazo na moyo wa Mungu? Tunapotambua kwamba Yesu ni sura ya moja kwa moja ya Baba yake na kwamba urithi wake kutoka kwa Baba unamfanya kuhitimu zaidi kuliko malaika, tunaweza sema, "Mungu Atukuzwe!" Tunaweza kuwa na imani kwamba Yesu anaweza kuwakilisha Baba kwetu na kunena hasa kilicho mawazoni mwake.

Kisha tunapoigeukia sura ya pili ya Waebrania tunasoma:

> Basi kwa kuwa watoto wana nyama na damu, Yeye pia alishiriki katika ubinadamu wao, ili kwa kifo chake, apate kumwangamiza huyo mwenye nguvu za mauti, yaani, Shetani, (15) na kuwaweka huru wale waliokuwa utumwani maisha yao yote kwa sababu ya kuogopa mauti. (16) Kwa kuwa ni dhahiri kwamba hakuja kusaidia malaika, bali uzao wa Abrahamu. (17) Kwa sababu hii ilibidi afanane na ndugu Zake kwa kila hali, ili apate kuwa Kuhani Mkuu mwenye huruma na mwaminifu katika kumtumikia Mungu, ili pia apate kufanya upatanisho kwa ajili ya dhambi za watu. (18) Kwa kuwa Yeye mwenyewe aliteswa alipojaribiwa, aweza kuwasaidia wale wanaojaribiwa. Waebrania 2:14-18.

Katika maneno haya tunajifunza kwamba Yesu alichukua hali yetu halisi juu yake. Alifanywa kuwa kama sisi katika vitu vyote. Anajua jinsi ilivyo kuhisi uchovu zaidi na kusukumwa na watu wengi wenye hasira. Anajua jinsi ilivyo unapohisi kukataliwa. Alijaribiwa katika hali zote kama tunavyo ila bila dhambi. Tunapoelewa kwamba Yesu kweli ni Mwana wa Mungu, tunaweza kuwa na imani kamili kwamba atafikisha maombi yetu kwa Baba na kisha atarejesha uwezo, faraja na himizo kutoka kwa Baba.

Makanisa mengi ya kiprotestanti hufundisha kwamba Yesu anatuombea mbinguni. Ila kwa kuwa hakuna imani kwamba Yesu huenda Patakatifu pa Patakatifu kufanya kazi ya mwisho ya upatanisho, hakuna haja ya kusaki roho na kuweka dhambi zote kando. Hili linaweza fananishwa na kutembea kwa burudani katika Daraja la Malango ya Dhahabu "Golden Gate Bridge." Kama tunaamini kwamba Yesu ataendelea kuombea dhambi bila kukomesha kazi hii, basi tunaweza jiingizia wazo kwamba tujaribu kuishi maisha mema, lakini hatuhitaji kuwa na bidii kwa sababu daima tunaweza omba msamaha; hauwezi isha.

Hata hivyo, hitaji la kuweka kando dhambi zote huja tunapoona kwamba upatanisho wa dhambi utakoma kabla ya Kristo kurejea mara ya pili. Hitaji la hudumu ya Patakatifu pa Patakatifu linaweza elezewa kwa njia hii. Hili linaweza fananishwa na kusafiri katika maporomoko ya "Niagara Falls" juu ya waya. Mara tunapoelewa kwamba kuombewa kwa dhambi kutakoma kabla ya marejeo ya pili, tunakuwa kama mtu ambaye kwa hiari aliruka kwenye toroli na kuruhusu mwanasarakasi anayetumia kamba, Charles Blondin, kumvusha korongo ya maporomoko ya Niagara Falls. Kisa kinapoelezewa, waya ilianza kucheza walipokuwa kando. Blondin alimwambia mtu huyo asimame katika toroli. Akiwa ameketi karibu kwenye toroli kwa mda mchache, alikuwa karibu vya kutosha kwa Blondin kutazama ujuzi wake wa kwanza. Blondin kwa ujanja alimbeba mtu huyo kwa makini kwenye mgongo wake na kubeba katika safari iliyosalia.

Kama unaamini kuwa njia ya kuelekea mbinguni ni kutembea tu katika Daraja la Malango ya Dhahabu "Golden Gate Bridge", utahitaji kujishikilia kwenye mgongo wa mpatanishi wako wa maisha yako muhimu? Hapana! Unaweza tembea hata hatua 30 kutoka kwake bila kuumia. Unaweza kosa kuhitaji kuwa karibu na Mkombozi wako, hivyo hautakuwa na ufahamu wa dhambi zako au kujifunza zaidi kumhusu Baba kupitia kwa Mwana. Uzoefu wa Patakatifu pa Patakatifu huweka mbele yetu waya ambayo Mkombozi wetu atatubeba iwapo tutakuwa tayari. Uzoefu wa Patakatifu pa Patakatifu hautaruhusu chochote cha binafsi kuingia katika Kanani ya Mbinguni. Uzoefu wa Patakatifu pa Patakatifu huhitaji tujiweke kikamilifu

kwa mpatanishi wetu, tukimwamini kutuombea na kutupa uwezo tunaohitaji kushinda. Kama Bibilia inavyosema:

> Nami nitawakaribieni ili kuhukumu; Malaki 3:5.

Mungu atawakaribia ili kuwahukumu kusaidia wanaotafuta ukweli na kutambua kazi ya uongo ya wale wanao dharau njia ya wokovu. Bibilia inatwambia:

> Lakini kwetu sisi yuko Mungu mmoja, aliye Baba, ambaye vitu vyote vyatoka Kwake na kwa ajili Yake sisi twaishi na kuna Bwana mmoja tu, Yesu Kristo, ambaye kwa Yeye vitu vyote vimekuwepo na kwa Yeye sisi tunaishi. 1 Wakorintho 8:6.

> Kwa maana kuna Mungu mmoja na mpatanishi mmoja kati ya Mungu na wanadamu, yaani, mwanadamu Kristo Yesu; 1 Timotheo 2:5.

Tunaona kwamba kuna Mungu mmoja, Baba, na kuna mpatanishi mmoja kati ya Mungu na mwanadamu, mwanadamu Kristo Yesu. Kama nitakubali mafundisho ya utatu, basi nitalazimika kuamini kuwa kuna Mungu Mmoja ikiwemo Baba, Mwana na Roho na mpatanishi mmoja Yesu Kristo. Hili humfanya Yesu kuwa mpatanishi na yule ambaye upatanisho unafanyika kwake. Inawezekana mtu kweli kupatanisha wakati huo huo ni mmoja wa chama kinachohitaji upatanisho? Hali hii haitakuwa wazi kwa mapendeleo?

Kama Yesu ni Mungu kwa njia sawa na Baba, basi mbona Baba anahitaji upatanisho zaidi wa Mwana? Yesu anawezaje mwakilisha Baba kweli kama hatoki kwa Baba? Upatanisho unaweza kuwa tu wa mfano kwa sababu hakuna tofauti kati ya Baba na Mwana isipokuwa ya jina.

Mpatanishi wa kweli na fanisi huhitaji cheo chenye tofauti wazi kutoka kwa vyema viwili vinavyohitaji upatanisho. Urithi ambao Kristo alipokea kutoka kwa Baba unaweka wazi tofauti kati yao. Pia inamruhusu Kristo kuwakilisha Mungu kikamilifu kitabia. Yeye ni tofauti na Mungu, ila yuko na Mungu na kwa hivyo ni Mungu kweli kwa urithi. Kama Mwana wa Mungu ambaye alichukua juu yake mwili wetu, ni tofauti nasi, ila ni mmoja wetu kwa urithi wake. Ni tofauti ya Kristo kupitia kwa uwili wa

urithi wake kutoka kwa Mungu na mwanadamu ambao unamfanya kuhitimu kuwa mpatanishi wa kweli kati ya Mungu na mwanadamu.

Tunapojua mambo haya kuhusu Mkombozi wetu, tunaweza weka uzani wetu wote juu yake na kuamini kwamba atatupa msaada tunaohitaji ili kuvuka waya nyembamba. Mpatanishi halisi hutoa upatanisho halisi kwa wokovu halisi. Mpatanishi wa mfano wa Utatu hutoa uwakilishi wa mfano wa Baba wa mfano ambaye hutoa uwezo wa mfano na wokovu wa mfano ambao ni sawa na kifo.

Hii ni sababu nyingine muhimu mbona nimemchagua Mpendwa wangu juu ya Utatu. Mwana wa pekee wa Mungu tu ndiye anaweza tupa upatanisho wa kweli kwa uwakilishi wa kweli. Imani yangu kwa mpatanishi wangu mzuri inatia nguvu imani yangu ya kuja mbele za Baba katika hukumu.

> Bwana hatamwacha mkononi mwake, Wala hatamlaumu atakapohukumiwa. Zaburi 37:33.

Mpendwa wangu tu ambaye nimemchagua ameniruhusu kutembea njia yote kupitia Patakatifu kwa kuwa kweli ndiye njia ya kuelekea kwa Baba.

> Ni nani huyu apandaye kutoka nyikani, Akimtegemea mpendwa wake? Nalikuamsha chini ya huo mpera; Huko mama yako alikuonea utungu, Aliona utungu aliyekuzaa. (6) Nitie kama muhuri moyoni mwako, Kama muhuri juu ya mkono wako; Kwa maana upendo una nguvu kama mauti, Na wivu ni mkali kama ahera. Mwako wake ni mwako wa moto, Na miali yake ni miali ya Yahu. (7) Maji mengi hayawezi kuuzimisha upendo, Wala mito haiwezi kuuzamisha; Kama mtu angetoa badala ya upendo Mali yote ya nyumbani mwake, Angedharauliwa kabisa. Wimbo wa Ulio Bora 8:5-7.

## 22. Furaha ya Mpendwa Wangu

Kuna mawazo mengine mengi ambayo naweza shiriki nanyi kuhusu mbona nafurahia katika Mpendwa wangu lakini hakutakuwa na nafasi ya kutosha vitabu hivyo vingi kuonyesha mambo hayo kama Yohana alivyosema:

> Lakini kuna mambo mengine mengi ambayo Yesu alifanya, kama yote yangeliandikwa, nadhani hata ulimwengu wote usingekuwa na nafasi ya kutosha kuweka vitabu vyote ambavyo vingeandikwa. Amen. Yohana 21:25

Ila kuna kitu ambacho ninahitaji kushiriki nawe kwa nini nimemchagua Mpendwa wangu na kwa nini ni mzuri kuliko ulimwengu wote.

Kuna Wakristo wengi leo ambao wanajiunga na wazo lifuatalo wanapozungumza kuhusu upendo wa Mungu.

> "Upendo ni wa mtu ambaye anapenda, na kwa upendo kitu kinapendwa." Augustine. De Trinitite "On the Trinity" Book VIII

Kutokea kwa dhana hii ya upendo ambao unafahamika kuwepo katika Utatu, tunapata yafuatayo:

> Kama Mungu ukweli ni —katika kiini chake chote—Mungu wa "upendo" (Yohana 3:16 and 1 Yohana 4:8), basi tunahitaji kuzingatia matokeo yafuatayo. Anaweza yeye ambaye amekuwepo tangu milele yote na ambaye alitufanya kwa sura yake ya kupendeza—Mungu huyu kweli anaweza itwa upendo kama alikuwepo peke yake kama kiumbe? Si upendo hasa upendo mtakatifu, unawezekana tu kama yule ambaye aliumba ulimwengu wetu kama angekuwa kiumbe wa wingi akionyesha "upendo" katika wingi wake mtakatifu kuanzia milele yote?... [Sasa ananukuu kutoka kwa Bruce Metzger] "Waunitaria wanakiri kukubaliana na kauli kwamba 'Mungu ni upendo.' Lakini maneno haya 'Mungu ni upendo,' hayana maana halisi isipokuwa Mungu awe tu watu wawili. Upendo ni kitu ambacho mtu anakuwa nacho kwa mtu mwingine. Kama Mungu alikuwa mtu mmoja, basi kabla ulimwengu kuumbwa, hakuwa upendo. **Kwa kuwa, kama upendo ni kiini cha Mungu, angemiliki kitu cha milele cha upendo, zaidi ya**

> **hayo, upendo kamili unawezekana tu kati ya walio na usawa**. Jinsi tu mtu hawezi tosheleza au kutambua nguvu zake za upendo kwa kupenda wanya wa chini, **ndivyo Mungu hawezi tosheleza au kutambua upendo wake kwa kumpenda mtu au kiumbe chochote. Kuwa asiye na mwisho, lazima amemiliki kitu kisicho na mwisho cha upendo**, baadhi hubadilisha utu wa ndani, au, kutumia lugha ya theolojia ya Mkristo wa jadi, Mwana aliyestahili, aliye milele, na Mwana aliye sawa. *The Trinity*, Whidden, Moon na Reeve, ukurasa 115,116.

Hoja ya mwisho ya kuzingatia ni marejeleo kwa 1 Yohana 4:8 ambayo inatwambia "Mungu ni upendo." Wale ambao wanaunga mkono Utatu watatufanya kuaini kwamba marejeleo haya "Mungu ni upendo." Inarejelea watu watatu wa hali sawa ambao wanapendana, ila kama tukisoma fungu hili katika muktadha wake tunapata jambo tofauti.

> 1 Yohana 4:7-12 Wapenzi na tupendane, kwa kuwa upendo watoka kwa Mungu. Kila apendaye amezaliwa na Mungu naye anamjua Mungu. (8) Yeye asiyependa hamjui Mungu, kwa sababu **Mungu ni upendo. (9) Hivi ndivyo Mungu alivyoonyesha upendo Wake kwetu, kwa sababu Mungu alimtuma Mwanawe wa pekee ulimwenguni, ili tupate uzima kwa Yeye. (10) Huu ndio upendo, si kwamba tulimpenda Mungu, bali Yeye alitupenda, akamtuma Mwanawe, ili Yeye awe dhabihu ya kipatanisho kwa ajili ya dhambi zetu.** (11) Wapenzi, kama Mungu alitupenda sisi hivi, imetupasa na sisi kupendana. (12) **Hakuna mtu ye yote aliyemwona Mungu wakati wo wote.** Kama tukipendana, Mungu anakaa ndani yetu na upendo Wake umekamilika ndani yetu.

Kama ninavyoelewa kifungu hiki, Yohana anaelezea upendo wa Mungu kwa kumtoa Mwanawa afe kwa ajili yetu. Hivyo katika fungu la nane anamwelezea Mungu kama upendo na kisha anapanua maelezo haya katika udhihirisho wa Mungu kumtuma Mwanawe. Msimamo wa matumizi katika kifungu hiki hayawezi elekeza kwa ukweli ambao Mungu alitaja katika fungu la 8 ni Mungu yule yule katika fungu la 9-12? Hili halipendekezi kwamba Mungu katika fungu la 8 ni Baba na kwamba upendo wake unadhihirishwa katika kumtoa mwanawe?

Jambo la pili ambalo ningependa kutaja ni kwamba neno la Kiyunani la *upendo* katika 1 Yohana 4:8 ni *agape*. Ufahamu wangu kutoka kwa kusoma kwangu ni kwamba *agape* ni upendo ambao huongeza thamani badala ya kuitafuta. Mungu kumtoa Mwanawe kwetu huongeza thamani ndani yetu na ukweli ni *agape*. Ila tunapotazama upendo unaoelezea Utatu, tunaona kwamba Mungu huyu anahitaji kitu ambacho kinatoshana naye kwa nguvu zake kamili kudhihirishwa. Aina hii ya upendo hutafuta thamani na kutosheleza hitaji. Haya sio maelezo ya *agape* bali ya aina nyingine ya upendo.

> Agape mara nyingi unalinganishwa na eros, ambao haupatikani katika Agano Jipya ingawa maarufu katika falsafa ya Wayunani. Eros unaweza rejelea upuuzi, upendo wa mwili, lakini katika muktadha wa wazo la Hellenic unachukua muundo wa upendo wa kiroho ambao hutaka kupata uzuri wa hali ya juu. **Eros ni hamu ya kumiliki na kufurahia** [hitaji au hamu ya kingine]; **agape ni kuwa tayari kuhudumia bila kutoridhishwa.... Eros huvutiwa kwa kile chenye thamani kuu** [hitaji la hali sawa au usawa]; **agape huwafikia wale wenye thamani ya chini kabisa. Eros hutambua thamani** [hutafuta usawa] **ilhali** [sic] **agape huumba thamani** [hufanya sawa]. **Agape ni upendo wa karama ilhali eros ni upendo wa hitaji. Eros hububujika kutoka kwa upungufu ambao lazima utoshelezwe. Agape ni mfuriko wa wingi wa neema takatifu.** *God the Almighty: Power, Wisdom, Holiness and Love*, Donald Bloesch, 2006, page 147.[12]

Ingawa inaweza kuja kwa mshangao kwa Waadventista wengi kufikiria kuwa yeyote anaweza shikamanisha eros na upendo wa Mungu, hili linafahamika vyema na Kanisa Katoliki la Roma.

> Mungu ndiye chanzo kuu cha viumbe vyote; lakini kanuni hii ya jumla ya maumbile—nembo, tabia asili—ni kwa wakati uo huo mpendwa aliye na hamu ya upendo wa kweli. **Eros kwa hivyo unasaidiwa kikuu, ila kwa wakati uo huo umesafishwa kiasi cha kuwa moja na agape**. Pope

[12] Maoni kwenye parandesi yameongezwa.

Benedict IX Encyclical Letter, 2005, Deus Caritas Est “God is Love.”

Hapa kuna tofauti moja muhimu kati ya Utatu na Baba na Mwanawe na hakika nataka kusisitiza hoja hii muhimu.

Utatu hutafuta usawa ila Baba hufanya sawa.

Ukweli wa kuhuzunisha kusio na kifani kuhusu utatu ni kwamba kama upendo kamili unaweza patikana tu katika kutafuta yule ambaye yuko sawa na basi yeyote asiye sawa na Mungu hawezi kuwa mpokezi wa upendo kamili. Kama wazo letu kumhusu Mungu ni watu watatu wenye uwezo sawa ambao wanapendana basi hatuwezi faa upendo wao mkamilifu. Tukiwa na dhana hii ya Mungu, tunakuwa wahusika katika kutafuta njia za macho yetu kufunguliwa na kuwa kama miungu (Mwanz 3:5) ili tufae upendo mkamilifu wa Mungu. Utatu huniweka katika jukwaa ambalo hunilazimisha kujaribu na kuwa kama aliye juu zaidi ili niweze kuupokea upendo huo mkamilifu.

Ukweli mtamu wa Mpendwa wangu ni kwamba vitu vyote vilipeanwa mikononi mwake na Baba yake.

> Kama vile Baba alivyo na uzima ndani Yake, vivyo hivyo amempa Mwana kuwa na uzima ndani Yake; Yohana 5:26

Kama Mungu alimpa Mwanawe kuwa na uzima ndani yake yeye mwenyewe, hivyo basi hili sio onyesho la agape? Mungu Baba huwekeza thamani kwa Mwanawe na humfanya kuwa sawa. Sio hili ambalo 1 Yohana 4:8 inaonyesha? Kwa kuwa Mpendwa wangu alipewa kila kitu na Baba yake, ninapomtazama Mwana wa Mungu, ninatazama yule ambaye kila kitu kimewekezwa ndani yake. Kamwe sitazami tena sura ya yule ambaye hutafuta kukubalika kwa kuwa sawa, ila, natazama yule ambaye alifanywa sawa kwa sababu alikubalika.

Ninajua kwamba Bwana Yesu Kristo alirithi vyote ambavyo Baba alivyo navyo na anauungu kamili kupitia kwa urithi, na katika urithi huo ninaweza sikia maneno ya upendo ya Baba wa kweli aliye nena na

mwanawe. Maneno Baba na Mwana hupata maana tu kupitia kwa urithi ambao agape huruhusu na eros huukataa.

Katika maneno haya yenye thamani ya Baba kwa Mwanawe wa pekee, ninapata thibitisho la uwana. Agape ya Mungu hutiririka kupitia kwa Mwana na hunena kwangu.

> Nayo sauti kutoka mbinguni ikasema, "Huyu ni [agapētos] Mwanangu mpendwa, ambaye ninapendezwa sana naye. Matt 3:17
>
> Na neno ambalo lilinenwa kwa Yesu katika Yordani, "Huyu ni Mwanangu mpendwa, ambaye ninapendezwa sana naye," yanakumbatia ubinadamu. Mungu alinena kwa Yesu kama mwakilishi wetu. Pamoja na dhambi zetu zote na udhaifu, hatuwekwi kando kama wasiofaa. "Kwa hiyo tunamsifu Mungu kwa huruma zake kuu alizotumiminia kwa sababu sisi ni wa Mwanawe Mpendwa." Waefeso 1:6. Utukufu ambao ulikaa ndani ya Kristo ni kiapo cha upendo wa Mungu kwetu. Unatwambia juu ya nguvu za maombi,--jinsi sauti ya mwanadamu inaweza fikia sikio la Mungu, na maombi yetu hukubalika katika vyumba vya mbinguni. Kwa dhambi, ulimwengu ulikatwa kutoka mbinguni, na kukengeushwa kutoka kwa ushirika; lakini Yesu ameuunganisha tena na nyanja ya utukufu. Upendo wake ulitajirisha mtu, na ukafikia urefu wa mbingu. Mwanga ambao ulianguka juu ya Mkombozi wetu kupitia kwa mianya wazi utatuangukia tunapoomba na msaada wa kuyashinda majaribu. Sauti iliyonena kwa Yesu inasema kwa kila aaminiye, Huyu ndiye mtoto wangu Mpendwa, ambaye napendezwa naye. "Wapenzi, sasa tu watoto wa Mungu, lakini bado haijadhihirika tutakavyokuwa, lakini twajua ya kwamba, Yeye atakapodhihirishwa, tutafanana naye, kwa maana tutamwona kama alivyo." 1 Yohana 3:2. *Desire of Ages*, page 113.

Ni urithi kamili wa Kristo ambao hudhihirisha kwamba Baba ana agape kwa Mwanawe. Kama Kristo hangepokea urithi, basi hatuwezi kuwa na uhakika kwamba Mungu ana *agape* kwa Mwanawe. Kama Mwana alimiliki uwezo wote kutoka kwake na akajipa tu basi Baba katika kutambua kile

ambacho Mwana anacho tayari, angekuwa na *phileo*[13] kwa Mwana. Ila Baba alisema alikuwa na *agape* kwa Mwanawe. Hili linaweza kuwa kweli tu kupitia kwa urithi wa Kristo. Kupitia tu kwa kupeana vyote kwa Mwanawe, Baba angeweza kumpa *agape*, wakati huo tu ndio tunaweza kuwa na uhakika kuwa upendo wa Mungu hautegemei asili yoyote ya ubora wa Mwana, na ni upendo huu ndio hutuweka huru.

Kupitia kwa agape iliyopeanwa kwa Kristo, naweza yashikilia maneno haya katika Mathayo 3:17 kwa sababu *agape* huweka thamani ndani yangu na huniruhusu kuamini kwamba mimi ni mwanawe kupitia kwa Kristo, wakati ambao *Eros* hunihukumu kwa sababu hutafuta thamani ambayo mimi sina yoyote. *Agape* huninenea kwa wingi wa uthabiti ninaposoma:

> …Lakini nenda kwa ndugu zangu ukawaambie, 'Ninapaa kwenda kwa Baba yangu ambaye ni Baba yenu, kwa Mungu wangu ambaye ni Mungu wenu. Yohana 20:17

Baba ya Yesu ni Baba yangu, na Mungu wa Yesu ni Mungu wangu. Yote haya ninamiliki kupitia kwa Kristo, Mwana wa kipekee wa Mungu, ambaye ni onyesho kuu la *agape* ambao ulimwengu daima unaweza tazama. Hii ndio sababu Mungu anamuenzi Mwanawe na anampa jina juu ya majina yote. Kristo ni ufunuo mkuu wa upendo wa *agape* wa Mungu.

Kwa miaka mingi hila ya Utatu ilininyima furaha ya kujua naweza pendwa kweli na Mungu. Hali ya usawa, umilele wa wahusika wake ulikumbusha mawazoni mwangu uongo wa kuhuzunisha kwamba Mungu anatafuta thamani na anatamani wale ambao tayari wako sawa. Sasa kwa wingi wa furaha, naweza kutangazia kwamba ufahamu wangu wa Mwana wa pekee umeniweka huru kutoka kwa uongo huu wa kutisha, na sasa naweza muona Baba yangu wa mbinguni akiwa na upendo mkamilifu kwangu na kwamba amewekeza ndani yangu utajiri wote wa mbinguni, kwa kuwa alimtoa Mwanawe kunifilia. Kamwe sitafuti tena kuwa "kama aliye juu

[13] Vizuri mpenzi, hiyo ni, rafiki; wenye upendo kamili, ambayo ni, kwa upendo (bado kama nomino, mshirika, jirani, n.k.): - rafiki. *Strongs Concordance* G5384.

zaidi." Upendo wake mkamilifu wa *agape* ndio tu ambao nahitaji ili kusalia kama nimeridhika katika nyanja ambayo niliumbiwa.

Hivyo katika Kristo Yesu, furaha yangu imekamilishwa. Ninapotazama mfalme wangu mkuu na kumuona akivikwa katika upendo wa *agape* wa Baba yake, ninalemewa na furaha. Napata pumziko kwa nafsi yangu na hakika napata nira yake laini na mzigo wake mwepesi.

## Hitimisho

Baba mpendwa uliye Mbinguni, na kutukuza, nakuheshimu na kukuabudu kwa wingi wa neema na upendo usio kuwa na mipaka katika kutupa Mwanao kama suluhu, Kuhani na Mfalme. Nakushukuru kwa kunikomboa kutoka kwa mauti yakini na kunidhihirishia hatari na hila za mshawishi. Ulinionyesha wazi kuwa ahadi zake ni za uongo na msingi wake ni kama mchanga wa kuhama.

Nakushukuru kwa kuniongoza hatua baada ya nyingine kuelekea kwa Patakatifu Pa patakatifu pako. Umechukua mitazamo yangu ya ukweli wa shaba na kuisafisha na kunifanya kama dhahabu safi. Sasa naona kupitia kwa ukuta huu takatifu, uzuri wa maua yaliyochanua na mti wa mtende (1 Wafalme 6:20). Ulimtuma Eliya kunikabili, na uliruhusu majaribu ya moto kunisafisha. Ila kupitia kwa vitu hivi vyote, Ulituma Roho wa Mwanao moyoni mwangu akilia, "Abba Baba."

Baba Mpendwa, nashikilia hakikisho la Neno lako. Hisia zangu zinanilemea kwa kuwaza mambo haya. Hivyo basi nimetia nanga kwa mdhamini wa Maneno yako. Nani anaweza waza kuwa mtu masikini, mnyonge na mpumbavu kama nilivyo, anaweza pata upendeleo wa Bwana wangu na karama ya Mwanawe?

Enzi yako inatawaliwa kwa utukufu, haki na ukweli. Ila zaidi ya haya yote umevikwa taji ya rehema, uvumilivu na upendo – upendo wa Agape ambao huwekeza na kujenga thamani badala ya kujitafutia thamani.

Baba, niruhusu nikae nawe katika Patakatifu Pa Patakatifu hapa; wacha takataka yangu yote iondolewe. Wacha Roho wa Mwanao akae nami daima na anifunze Amri zako. Nataka Sheria yako iandikwe moyoni mwangu na kutamani iwe wazo langu mchana na usiku.

Naamini kwamba Mpendwa wangu ananiandalia chumba katika jumba lako kubwa. Nasukumwa kwa machozi kwamba utanikaribisha kwa upendo katika makao yako na kutamani niweko pale.

Vitu hivi kutoka moyoni mwangu nawasilisha kwako kwa jina la Mpendwa wangu, Mwanao wa pekee. Amina.

Nasikia hatua zake, mapigo yangu ya moyo yanaenda kwa kasi kwa matarajio. Naisikia sauti yake kama mlio wa maji mengi. Ni kama zeri tamu nafsini mwangu. Mpendwa wangu anaita; inaweza kuwa ni kwa ajili yangu anaita? Ni vipi tumaini la thamani kama hilo linaweza kuzwa kifuani mwangu? Dhana hii inaibuka kutoka wapi? Mbona nihesabiwe kwamba nastahili utambuzi wake—Mfalme huyu mkuu, Mwana Mpendwa wa Baba? kwa huwahi ya patakatifu, Wimbo ulio bora na Mwendo wa Safari (Pilgrim's Progress) tunaelezea safari ya mtu mmoja kupitia kwa vizingiti, majaribu na changamoto, kutambua, kuuza vyote na kuwa na upendo na Yesu, Mwana wa Baba.

fatheroflove.info